



EAST AND  
HORN OF  
AFRICA  
HUMAN RIGHTS  
DEFENDERS  
PROJECT  
(EHAHRDP)

# Kutetea Haki za Binadamu

Kitabu cha Marejeo kwa watetezi wa Haki za Binadamu

Toleo la pili

## Kutetea Haki za Binadamu: Kitabu cha Marejeo kwa watetezi wa Haki za Binadamu (Toleo la pili) 2012

East and Horn of Africa Human Rights Defenders Project  
Human Rights House, Plot 1853, Lulume Rd., Nsambya  
P.O Box 70356 Kampala Uganda  
Phone: +256-312-256-820  
Fax: +256-312-256-822  
Email: program@defenddefenders.org, hshire@yorku.ca  
Web : <http://www.defenddefenders.org>

Kitabu hiki kinapatikana katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kiamhari, Kiswahili, na Kisomali katika mtadao  
<http://www.defenddefenders.org/resource-book>

Sifa ziende kwa East and Horn of Africa Human Rights Defenders Project

Kimetolewa kwa msaada wa kifedha wa Swedish International Development Cooperation Agency (SIDA) na Ministry of Foreign Affairs of the Kingdom of the Netherlands.

Toleo la kwanza lilitayarishwa na Norah Rehmer  
Toleo la pili limetayarishwa na Neil Blazevic



This work is licensed under a  
Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivs 3.0 Unported License.

You are free to **Share** — to copy, distribute and transmit the work under the following conditions:

**Attribution:** You must attribute the work in the manner specified by the author or licensor (but not in any way that suggests that they endorse you or your use of the work).

**Noncommercial:** You may not use this work for commercial purposes.

**No Derivative Works :** You may not alter, transform, or build upon this work.



EAST AND  
HORN OF  
AFRICA  
HUMAN RIGHTS  
**DEFENDERS**  
PROJECT  
(EHAHRDP)

# Kutetea Haki za Binadamu

Kitabu cha Marejeo kwa watetezi wa Haki za Binadamu

Toleo la pili

# Yaliyomo

<b>Shukrani:</b>	iii
<b>Dibaji</b>	1
<b>Sura ya 1:</b> Vyombo vya Kimataifa na Kikanda kwa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu	2
<b>Sura ya 2:</b> Watetezi wa Haki za Binadamu katika Vitisho: Mtazamo wa Usalama Ugani kwa Kazi yao	11
<b>Sura ya 3:</b> Kiwewe na Mikakati ya Kukikabili kwa Watetezi wa Haki za Binadamu	19
<b>Sura ya 4:</b> Kampeni za Utetezi wa Haki za Binadamu	28
<b>Sura ya 4.5:</b> Vyombo vya Habari vya Kijamii kwa ajili ya Haki za Binadamu	32
<b>Sura ya 5 :</b> Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu – Haja ya Utekelezaji wa Kimkakati	34
<b>Sura ya 6 :</b> Kutetea Kundi la Wachache katika Tabia ya Mwenendo wa Kufanya Mapenzi	40
<b>Kiambatanishi cha 1:</b> African Commission: Resolution on the Protection of Human Rights Defenders in Africa (2004)	48
Azimio Kuhusu Haki Na Wajibu Wa Mtu Binafsi, Vikundi Na Jumuiya Mbalimbali Katika Kusimamia Na Kulinda Haki Za Binadamu Na Uhuru Wa Msingi Zinazotambuliwa Kimataifa (1998)	50
European Union Guidelines on Human Rights Defenders (2008)	54
<b>Kiambatanishi cha 2:</b> Rejea kuhusu Taratibu za Kimataifa na Kikanda	59
<b>Kiambatanishi cha 3:</b> Rasilimali kwa Watetezi wa Haki za Binadamu Ulinzi na Usalama kwa Watetezi wa Haki za Binadamu	63
<b>Kiambatanisho cha 4:</b> Mashirika yanayofanya kazi na watetezi wa Haki za Binadamu	70

# Shukrani

Chapisho la kitabu hiki lisingewezekana bila msaada wa kifedha wa SIDA, Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi. Tunatoa shukrani pia kwa Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Maendeleo cha Kanada ambacho kiligharamia toleo la kwanza.

Mwisho tunatoa shukrani kwa wote waliochangia kitabu hiki, ambao wametajwa katika sura mbalimbali, na kwa Nora Rehmer na Neil Blazevic ambao walitayarisha toleo la kwanza na la pili kwa mfuatano huo.

# Dibaji

Miaka mitano imepita tangu Mradi wa Watetezi wa Haki za Binadamu Afrika ya Mashariki na Pembe ya Afrika ulipochapisha toleo la kwanza la *Kutetea Haki za Binadamu: Kitabu cha Rejea kwa Watetezi wa Haki za Binadamu*. Baada ya hapo changamoto mpya zimeendelea kukua na kutengeneza mazingira ambayo watetezi wa haki za binadamu wanafanya kazi.

Nchi mbalimbali zinaendelea kutumia sheria zenyetikwa vinyoziwa uhuru wa kuendesha kazi ya haki za binadamu. Hatua dhidi ya vitisho zilizofikiria zaidi kuimarishta utekelezaji wa sheria ya uhuru wa kuamua na kutumia mabavu, pamoja na kupitiwa kwa mahakama katika upunguzaji uzito au ucheleweshaji wa kesi zinazidi kutumika ili kuzuia mbinu halali za uchunguzi na upinzani kutoka wa watendaji wa asasi za kiraia. Ushirkiano na nchi za nje ina maana watetezi wa haki za binadamu waliolazimishwa kuingia kizuijini wanaweza kuendelea kunyanyasika hata katika nchi zao za hifadhi. Sheria zisizothibitishwa kwa ajili ya asasi zisizo za kiserikali zimekuwa zikitumika katika baadhi ya kesi, kuzuia fursa za fedha na pia shughuli za haki za binadamu, wakati sheria za vyombo vya habari mara nyingi hutafsiriwa na kutumiwa kiholela na kunyima uhuru wa kujieleza. Watetezi wa kundi la wachache katika mwenendo wa kufanya mapenzi wanaendelea kupigania wapate kutambuliwa kwamba haki za wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimpenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili na wa jinsi tata ni haki za binadamu, wakati vitisho kutoka kwa watendaji wa serikali na wasio wa serikali vimejenga pengo la uhasama kwa watetezi hawa.

Wakati changamoto hizi zinabadilika, nyenzo ambazo zipo kwa ajili ya watetezi wa haki za binadamu pia zimeendelezwa na kuwa za kisasa na za ufanisi zaidi. Matumizi kamili ya nyenzo hizi kwa njia ya kimkakati ni changamoto na uwezekano wa kuwapa nguvu watetezi madhubuti wa haki za binadamu.

Kujihusisha na mifumo ya kimataifa na kikanda ya haki za binadamu ni moja ya njia bora zaidi za kujenga utumbuzi wa masuala ya haki za binadamu na hata kuhitaji wadau wabeba majukumu kushughulika rasmi. Sura ya 1 ina mjadala wa njia hizi na matumizi yake ya ufanisi.

Matunzo binafsi na usalama wa kitaalamu kwa watetezi wa haki za binadamu ni muhimu ili

juhudii zao ziwe endelevu. Sura ya 2 na 3 zinahusu usimamizi wa usalama na kupunguza mfadhaiko kwa watetezi wa haki za binadamu kwa mtiririko huo.

Mikakati kwa ajili ya kuendesha kampeni inajadiliwa katika Sura ya 4, ambayo imerekebishwa kwa majadiliano ya nyenzo za vyombo vya habari vya kijamii kwa ajili ya kufikia malengo ya utetezi katika Sura ya 4.5.

Changamoto na mikakati maalum ya kutetea haki za wanawake na haki za kundi la wachache katika tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi zinashughulikiwa katika Sura ya 5 na 6 kwa mtiririko huo.

Hatimaye viambatanisho vya rejea vimerekebishwa kujumuisha machapisho yanayohusiana zaidi na mashirika yanayoshughulika na watetezi wa haki za binadamu.

Tumefurahi kuweza kufanikisha kitabu hiki kupatikana kwa Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kiswahili, Kiamhari, na Kisomalia, hivyo kufanya kiwafikie watu wengi katika kanda hii. Tunamshukuru mfadhlili wetu mkuu katika mradi huu, Shirika la Ushirkiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi.

Mradi wa watetezi wa Haki za Binadamu Afrika ya Mashariki na Pembe ya Afrika unawashukuru kwa dhati wote waliochangia kitabu hiki cha rejea kwa maoni yao, hali kadhalika kwa kazi yao endelevu katika huduma ya haki za binadamu.

Mradi wa watetezi wa Haki za Binadamu Afrika ya Mashariki na Pembe ya Afrika unatoa kitabu hiki kwa heshima ya wale wote waliopoteza maisha yao katika kupigania haki za binadamu. Tuungane katika kujenga maisha bora ya baadaye.



Hassan Shire Sheikh

Mkurugenzi Mtendaji / Mwenyekiti

Mradi/Mtandao wa watetezi wa Afrika ya Mashariki na Pembe ya Afrika.

# Sura ya 1:

## Vyombo vya Kimataifa na Kikanda kwa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu

Sura hii inatoa historia ya nyuma ya Azimio la *Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Wajibu wa Watu binafsi, Makundi na Vyombo vya Jamii ili Kukuza na Kulinda Haki za Binadamu Zinazotambuliwa Kiulimwengu na Uhuru wa Kimsingi* (kwa kawaida linajulikana kama “Azimio juu ya watetezi wa haki za binadamu”) na maelezo ya jumla ya Azimio lenyewe. Pia inaelezee taratibu maalum zifuatazo za ulinzi kimataifa na kikanda kwa ajili ya watetezi wa Haki za Binadamu, madaraka na mbinu zao za kazi:

1. Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu
2. Mwandishi Maalum kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu barani Afrika
3. Miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu

Wasomaji wanahimizwa kuendeleza utekelezaji wa viwango vya kimataifa vilivyomo katika Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu ambazo zinawalinda watetezi wa haki za binadamu duniani kote na kutumia na kuimarisha taratibu zilizoelezwu katika mada hii.<sup>1</sup>

### **Historia ya nyuma ya Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

Siku hizi, uendelezaji na ulinzi wa haki ya kuteta haki za binadamu hufanya mada yenye ongezeko la shauku duniani kote. Hata hivyo, kampeni ya kimataifa ya kuteka mawazo kimataifa juu ya hali ya watetezi wa haki za binadamu ilikuwa ikiandaliwa vizuri na kuwekewa malengo zaidi na zaidi wakati wa miaka ya 1980.

Barani Afrika, mfululizo wa mashauriano umekuwa na matokeo mazuri sana katika ufanuzi

wa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu. Kampeni za kanda ndogo na Afrika nzima zilizofanyika mwaka 1998 kabla ya kupitishwa kwa azimio hilo, zilikuwa udhihirishaji wazi wa shauku na dhamira ya asasi zisizo za kiserikali katika kuteta haki ya kuteta haki za binadamu, na kuendesha kampeni ya kuweka mazingira bora ya kufanya kampeni kwa ajili ya watetezi barani kote. Matokeo ya kampeni hizo katika Afrika yalitolewa katika Mkutano wa Paris

wa Desemba 1998 na katika maandiko ya Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu.

Katika kushughulikia hali mbaya inayowakabili watetezi, kwa azimio 53/144 la tarehe 9 Desemba 1998, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa kauli moja walipitisha Azimio kuhusu watetezi wa haki za binadamu. Hii ilikuwa baada ya zaidi ya muongo mmoja wa kushawishi, kufanya kampeni na mazungumzo. Utaratibu wa kupanga miaka na matukio katika mchakato wa kuandaa rasimu ulianza mwezi Februari 1980 na kumalizika mwezi Februari 1997, na Mkutano Mkuu ulipitisha Azimio hilo tarehe 9 Desemba 1998, yaani miaka 18 ya majadiliano, zoezi la aina yake lililokwenda taratibu zaidi katika historia ya Umoja wa Mataifa!

### **Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

#### **(A) Maoni ya jumla**

Kupitishwa kwa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu mwaka 1998 lilikuwa tukio muhimu. Kwa kupitisha Azimio hilo, nchi wanachama walitambua:

- hali mbaya ya watetezi wa haki za binadamu duniani kote;
- kuwepo kwa haki ya watetezi wa haki za binadamu katika kuteta haki za binadamu, na
- haja ya ushirikiano wa kimataifa katika kulinda haki hii ya kuteta haki za binadamu.

Azimio si mkataba au desturi, hivyo si chombo kinachofunga kisheria. Hata hivyo:

- Linawakilisha ushirikiano wa kimataifa wa kulinda haki za watetezi wa haki za binadamu duniani kote;
- Linatambua uhalali wa shughuli za haki za binadamu na haja ya shughuli hizi na wale wanaotekeliza shughuli hizi kulindwa;
- Linatoa mfumo wa kisheria wa kuwalinda

<sup>1</sup> Makala asilia ya Musa Gassama, na marekebisho na michango na Rachel Nicholson.

watetezi wa haki za binadamu;

- Linapanga viwango vya kimataifa vinavyolinda shughuli za watetezi wa haki za binadamu duniani kote;
- Linathibitisha kwamba watu binafsi, vikundi, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali wana wajibu mkuu, na jukumu la kuchangia uendelezaji wa haki ya kila mtu kwa agizo la kijamii na la kimataifa ambalo, haki na uhuru ulioelezwa katika Azimio la Haki za Binadamu na vyombo vingine vya haki za binadamu vinaweza kutambuliwa kikamilifu;
- Linaelezea kwa ufasaha haki zilizopo kwa namna ambayo inaleta urahisi zaidi wa kuzitumia kwa vitendo na hali ya watetezi wa haki za binadamu. Inaeleza bayana jinsi haki zilizomo katika vyombo vikuu vya haki za binadamu zinavyotumika kwa watetezi wa haki za binadamu;
- Lina kanuni na haki zinazozingatia viwango vya haki za binadamu vinavyolindwa katika vyombo vingine ya kimataifa, kama vile haki ya uhuru wa kujieleza, vyama na mikusanyiko na haki ya uhuru wa kwenda mahali.

### **(B) Wajibu wa Madola na wa Kila Mtu**

Azimio hili linaelezea wajibu maalum wa Nchi na majukumu ya kila mtu kuhusiana na kulinda haki za binadamu, pamoja na kueleza uhusiano wake na sheria za nchi. Nchi zina wajibu wa kutekeleza na kuheshimu masharti yote ya Azimio. Vifungu 2, 9, 12, 14 na 15 vinatoa maelekezo maalum ya wajibu wa Nchi na kuonyesha kuwa kila Nchi ina jukumu na wajibu:

Kifungu cha 2: Kila Nchi itatumia sheria hiyo, utawala na hatua nyingine kwa kadri itakavyolazimu ili kuhakikisha kuwa haki na uhuru viliviyotajwa katika Azimio la sasa vinakubaliwa kikamilifu.

Azimio hili linasisitiza kwamba kila mtu ana wajibu kwa jamii na ndani ya jamii na linatuhimiza sisi sote kuwa watetezi wa haki za binadamu. Vifungu vya 10, 11 na 18 vinatoa muhtasari wa majukumu ya kila mtu katika kuendeleza haki za binadamu, kulinda demokrasia na taasisi zake na si kukiuka haki za binadamu za watu wengine. Kifungu cha 11 kinatoa rejea maalum ya majukumu ya watu wanaotumia fani ambazo zinaweza kuathiri haki za binadamu za watu wengine, na zinawahusu hasa maafisa wa

polisi, wanasheria, majaji, nk.

### **(C) Wajibu wa sheria ya kitaifa**

Kwa upande wa wajibu wa sheria ya kitaifa, kifungu cha 3 na 4 vinaeleza kwa muhtasari uhusiano wa Azimio hili na sheria za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhakikisha utumiaji wa viwango vya kisheria vya juu zaidi iwezekanavyo vya haki za binadamu.

Kwa tafsiri ya wazi ya Azimio hili, ni muhimu kutambua kuwa kifungu cha 3 lazima daima kisomwe na kifungu cha 4.

Kifungu cha 3: Sheria ya ndani inayokubaliana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa na wajibu mwininge wa kimataifa wa Nchi katika mada ya haki za binadamu na uhuru wa kimsingi, ni mfumo wa kisheria ambamo haki za binadamu na uhuru wa kimsingi vinapaswa kutekelezwa na kufaidiwa na ambamo, shughuli zote zilizotajwa katika Azimio la sasa kwa uendelezaji, ulinzi na matokeo yenye ufanisi ya haki hizo na uhuru lazima zitekelezwe.

Kifungu cha 4: Hakuna chochote katika Azimio la sasa ambacho kitatafsiriwa kama kinachodhoofisha au kupingana na madhumuni na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa au kama vinavyouzia au kuhitilafiana na masharti ya Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu, Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu na vyombo vingine vya kimataifa na misimamo inayohusika na mada hii.

### **(D) Haki na ulinzi wanaopewa watetezi wa haki za binadamu**

Vifungu vya 1, 5, 6, 7, 8, 9, 11, 12 na 13 vya Azimio hili hutoa ulinzi maalum kwa watetezi wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki zao:

Kifungu cha 1: Kila mtu ana haki, kama mtu binafsi na kwa kushirikiana na watu wengine, kuendeleza na kupigania ulinzi na ufanikishaji wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi katika ngazi za kitaifa na kimataifa:

- Kutafuta ulinzi na utambuzi wa haki za binadamu katika ngazi ya kitaifa na kimataifa;
- Kuendesha kazi ya haki za binadamu kwa mtu mmoja mmoja na kwa kushirikiana na watu wengine;
- Kuunda vyama na mashirika yasiyo ya kiserikali;
- Kufanya mikutano au mikusanyiko kwa amani;

- Kutafuta, kupata, kupokea na kuhifadhi taarifa zinazohusiana na haki za binadamu;
- Kujenga na kujadili mawazo na kanuni mpya za haki za binadamu na kutetea kukubalika kwake;
- Kuwasilisha maoni na mapendekezo kwa mabaraza na wakala wa serikali na mashirika yanayohusika na masuala ya umma kwa ajili ya kuboresha utendaji wake wa kazi na kuleta umakini kwa kipengele chochote cha kazi yao ambao unaweza kuzorotesha utekelezaji wa haki za binadamu;
- Kutoa malalamiko kuhusu sera rasmi na vitendo vinavyohusiana na haki za binadamu na malalamiko hayo kuchunguzwa;
- Kutoa mapendekezo na msaada wa kisheria wenyre sifa za kitaalamu au ushauri na msaada mwingine katika utetezi wa haki za binadamu;
- Kuhudhuria kesi za hadhara, mashtaka na hukumu ili kutathmini uzingativu wao wa sheria ya kitaifa na wajibu wa haki za binadamu kimataifa;
- Kupata fursa na mawasiliano na mashirika yasiyo ya kiserikali na serikali mbalimbali bila kipingamizi;
- Kunufaika na ufumbuzi thabiti;
- Kutumia kihalali kazi au taaluma ya mtetezi wa haki za binadamu;
- Kuweka ulinzi wa uhakika chini ya sheria ya kitaifa katika kuonyesha hisia dhidi ya au kupinga, kwa njia ya amani, vitendo au makosa yanayodhaniwa na Serikali kwamba yanasaababisha ukiukaji wa haki za binadamu;
- Kutafuta, kupokea na kutumia rasilimali kwa lengo la kulinda haki za binadamu (pamoja na kupokea fedha kutoka nje ya nchi).

### **(E) Hoja nyininge**

Azimio linaonekana kwa baadhi ya wakosoaji kama matokeo yasiyoridhisha, kwa kuzingatia muda uliochukua nchi wanachama kukubaliana na maandiko na ukweli kwamba ina vifungu fulani ambavyo bado vinazorotesha haki za watetezi.

### **Madaraka ya Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

Mwaka 2000, chini ya miaka miwili baada ya kupitishwa kwa Azimio hili, Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu kwa pamoja ilipitisha Azimio 2000/61 ambalo lilitaka Katibu Mkuu kuteua Mwakilishi Maalum wa watetezi wa haki za binadamu. Huu ulikuwa utaratibu wa kwanza kuundwa katika ngazi ya kimataifa katika kulinda haki za binadamu kwa mujibu wa haki zilizotajwa katika Azimio. Bi Hina Jilani, mwanasheria maarufu wa haki za binadamu kutoka Pakistan, aliteuliwa kuwa Mwakilishi Maalum wa kwanza. Mrithi wa Tume ya Haki za Binadamu, baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, liliamua kuendelea na madaraka hayo kwa muda wa miaka mitatu mfululizo mnamo mwaka 2008 (azimio 7/8) na mwaka 2011 (Azimio 16/5). Mwezi Machi mwaka 2008, Bi Margaret Sekagya, hakimu wa Uganda na Mwenyekiti wa zamani wa Tume ya Haki za Binadamu ya Uganda, aliteuliwa kwenye madaraka, ambayo hapo ilibadilisha cheo na kuwa Mwandishi Maalum wa hali ya watetezi wa haki za binadamu.

Mwandishi Maalum hufanya shughuli katika uhuru kamili wa nchi yoyote, si mfanyakazi wa Umoja wa Mataifa na hapati mshahara. Madaraka ya Mwandishi Maalum ni kufanya shughuli kuu zifuatazo:

- Kutafuta, kupokea, kuchunguza na kushughulikia taarifa juu ya hali ya watetezi wa haki za binadamu;
- Kuanzisha ushirikiano na kufanya mazungumzo na Serikali na watendaji wengine wenyre nia ya kuendeleza na kutekeleza kwa ufanisi Azimio hili;
- Kutoa mapendekezo ya mikakati madhubuti iliyobora kwa kuwalinda watetezi wa haki za binadamu na kufuatilia mapendekezo hayo;
- Kuingiza mtizamo wa kijinsia katika kazi yake yote.

Baraza la Haki za Binadamu lilizisitiza Serikali zote kushirikiana na Mwandishi Maalum na kutoa taarifa zote zinazoombwu. Mwandishi Maalum anaombwa kuwasilisha taarifa ya kila mwaka kwa Baraza hili na Baraza Kuu.

### **(A) Mtazamo mpana wa utekelezaji wa Azimio**

Madaraka rasmi ya Mwandishi Maalum ni ya ujumla sana, yanayohitaji utambuzi wa mikakati, vipaumbele na shughuli za kuitekeleza. "Ulinzi" wa watetezi wa haki za binadamu ndio suala kuu

la Mwandishi Maalum. Ulinzi unaeleweka kuwa pamoja na ulinzi wa watetezi wenyewe na ulinzi wa haki yao ya kutetea haki za binadamu.

Mkakati wa ulinzi na hatua ya kuwaunga mkono watetezi wa haki za binadamu ileweke kama zile juhudzi zote ikiwa ni pamoja na za kisiasa, kisheria na kiutendaji, ambazo husaidia kuboresha mazingira ambayo watetezi wa haki za binadamu hufanya kazi.

Hatua za ulinzi zenyenye ufanisi zaidi ni zile ambazo zina matokeo ya pamoja na zile zinazoendeshwa kwa utashi wa kisiasa. Kuendeleza na kulinda haki ya kutetea haki za binadamu kimsingi hailindi tu haki ya kufanya kazi ya haki za binadamu bali pia kulinda wale wanaofanya kazi hii na kuilinda kazi yenye. Kwa maneno mengine, ni kuhusu kulinda haki za kisheria hali kadhalika heshima ya maumbile ya mtu na mazingira ya kazi.

#### **(B) Mtazamo mpana wa ufanuzi wa istilahi ‘watetezi wa haki za binadamu’**

Azimio halitaji mahali popote katika maandiko haya istilahi ‘mtetezi wa haki za binadamu’. Linataja” Watu binafsi, Vikundi na Vyombo vya Kijamii”. Bila shaka, hiki ni kigezo cha shida iliyokuwepo wakati wa mchakato wa mzungumzo na wa kuandika rasimu. Si kwamba tu kipindi ilichochukua kupitisha Azimio hili kilikuwa kirefu sana bali pia jina la Azimio linadhihirisha ugumu ulioukabili mchakato mzima. Hata hivyo, kukosekana kwa ufanuzi wa sentensi moja kungweza kumaanisha kwamba kuna fursa kwa mshika madaraka kutumia mtazamo wa jumla na mpana kwa kundi lengwa.

Kila itakavyokuwa, masuala yafuatayo yanahitaji kubaki kwa kumfikiria atakayekuwa chini ya ulinzi wa Azimio hili.

Watetezi wa haki za binadamu hutambuliwa zaidi ya wote kutoptana na kile wanachofanya na istilahi hii inaweza ikaelezewa vizuri zaidi kwa njia ya maelezo ya matendo yao na ya baadhi ya mazingira wanayofanya kazi.

Watetezi wa haki za binadamu lazima wafafanulike na kukubalika kwa mujibu wa haki wanazotetea na kwa mujibu wa haki yao ya kufanya hivyo, ilimradi wafanye hivyo kwa njia ya amani. Jambo muhimu zaidi katika kumpambanua mtu kama mtetezi wa haki za binadamu si cheo cha mtu au jina la shirika analofanya kazi, bali sifa bainifu ya kazi ya haki za binadamu inayofanyika. Watu wengi hutumikia kama watetezi wa haki za binadamu hata kama kazi zao za kila siku zinazelezwu katika istilahi tofauti, kwa mfano kama “maendeleo”. Watu wengi hufanya kazi

kama watetezi wa haki za binadamu nje ya mazingira ya taaluma au ajira yoyote.

Katika Afrika, watetezi wa haki za binadamu ni pamoja na watu ambao wenyewe wanawenza wasijieleze hivyo, lakini ambao matokeo ya shughuli zao katika uhamasishaji au taaluma au vinginevyo huendeleza heshima ya haki za binadamu barani Afrika.

“Watetezi wa haki za binadamu” ni istilahi inayotumika kuelezea watu ambao, mtu binafsi au pamoja na watu wengine, huendeleza au kulinda haki za binadamu. Imekuwa ikitumika zaidi tangu kupitishwa kwa Azimio kuhusu watetezi wa haki za binadamu mwaka 1998. Hadi wakati huo, maneno kama vile “mwanaharakati” wa haki za binadamu, “mtaalamu”, “mfanyakazi” au “kufuatinilia” yamekuwa ya kawaada. Istilahi “watetezi wa haki za binadamu” inaonekana kama istilahi husika na inayofaa zaidi. Mifano ya shughuli za watetezi wa haki za binadamu ambayo kwa kawaada hutolewa si orodha kamili. Jaribio muhimu ni kama mtu anatetea haki za binadamu au la.

#### **(C) Mtazamo wa kikanda wa utekelezaji wa Azimio**

Mshika madaraka ya Umoja wa Mataifa daima alikuwa akieleza haja ya kutekeleza Azimio la Umoja wa Mataifa kwa mtazamo wa kikanda na huu ulikuwa ujumbe wa Bi Hila Jilani kwa Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu, kikao kilichofanyika Pretoria mwezi Mei, 2002. Mwitikio kutoka Amerika, Umoja wa Nchi za Ulaya na Afrika unatia moyo. Katika suala hili, changamoto ni Mashariki ya Kati na Asia ambako hakuna chombo cha kikanda kinachofanana.

Ili kuweka mtazamo huu katika vitendo, Bibi Margaret Sekaggya na mwenzake Bibi Reine Alapini-Gansou katika Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu (angalia chini) walifanya ziara ya pamoja nchini Togo mwaka 2008. Waandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa na Afrika pia walitoa taarifa ya pamoja katika vyombo vya habari. Matendo haya hufanya mapendekezo yao yajulikane na kuyapa uzito zaidi, na jitihada zinaendelea ili kuhamasisha ushirikiano kama huo kwa mapana zaidi kati ya Umoja wa Mataifa na taratibu maalum za Afrika.

#### **(D) Mawasiliano na watetezi wa haki za binadamu**

Kwanza kabisa, Mwandishi Maalum anajaribu kupatikana na watetezi wa haki za binadamu

wenyewe kwa:

- Kupatikana ili apokee taarifa kutoka kwa watetezi, ikiwa ni pamoja na madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu uliofanywa dhidi yao na kutumia taarifa hii katika kubaini masuala yatakayoibuliwa na Madola;
- Kuhudhuria mara kwa mara matukio ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya haki za binadamu(ikiwa ni pamoja na moja ya vikao vitatu vya Baraza la Haki za Binadamu kila mwaka), ambayo hutoa fursa ya kuwasiliana na watetezi toka duniani kote.

#### **(E) Mawasiliano na Madola**

Mwandishi Maalum hudumisha mawasiliano ya mara kwa mara na Madola kwa njia ya mikutano kama vile vikao vya Baraza la Haki za Binadamu jijini Geneva na Mkutano Mkuu jijini New York, wakati ambapo Mwandishi Maalum hutoa ripoti ya mwaka kwa Madola, hujibu maswali yao na huweza kukutana na ujumbe wa Nchi moja moja kujadili matatizo, ikiwa ni pamoja na kesi za watu binafsi. Mawasiliano maalum zaidi hufanywa kwa pande mbili katika mikutano au kwa maandishi na hii hutumika na Mwandishi Maalum kuzungumzia matatizo maalum na Nchi binafsi na kutafuta msaada wa Nchi. Kwa mfano, katika kushughulikia kesi au kupata mwaliko wa kutembelea nchi hizo.

#### **(F) Mawasiliano na watendaji wengine muhimu**

Katika mwaka, Mwandishi Maalum hukutana na watendaji wengine wengi walio muhimu kwa madaraka na shughuli zake, ikiwa ni pamoja na Mabunge ya kitaifa; mashirika baina ya serikali kikanda, na makundi ya nchi zilizo na dhamira ya kuboresha wajibu na hali ya watetezi wa haki za binadamu.

#### **(G) Kesi za watu binafsi**

Mwandishi Maalum huzungumza na Nchi, kuhusu kesi za watu binafsi za ukiukwaji wa haki za binadamu uliofanywa dhidi ya watetezi wa haki za binadamu. Taarifa juu ya kesi kama hizo hupatikana kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mamlaka za Madola, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya Umoja wa Mataifa, vyombo vya habari na watetezi mmoja mmoja wa haki za binadamu.

Taarifa inapofika, Mwandishi Maalum kwanza anajaribu kuangalia kama iko ndani ya madaraka

yake. Pili, kila juhudhi hufanywa ili kuamua uhalali unaowezekana wa madai ya ukiukaji wa haki za binadamu na utegemeaji wa chanzo cha habari. Tatu, Mwandishi Maalum huwasiliana na Serikali ya Nchi ambamo madai ya ukiukaji huo inasemekana ultokea. Mawasiliano kwa kawaida hufanywa kwa njia ya hatua ya haraka au barua ya madai hutumwa kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na nakala kwa Ujumbe wake wa Kidiplomasia kwa Umoja wa Mataifa jijini Geneva. Barua hiyo hutoa maelezo ya mwathirika, masuala ya haki za binadamu na matukio ya madai. Lengo kuu la barua hii ni kuhakikisha kwamba mamlaka za Nchi inapewa taarifa ya madai hayo mapema iwezekanavyo na kwamba wanapata nafasi ya kulifanya uchunguzi na kukomesha au kuzuia ukiukaji wowote wa haki.

Barua za hatua ya haraka hutumika kutoa taarifa kuhusu ukiukaji unaodaiwa kuendelea au kuelekea kutoke. Lengo ni kuhakikisha kwamba mamlaka stahiki za Nchi zinajulishwa haraka iwezekanavyo juu ya hali hiyo ili waweze kuingilia kati kukomesha au kuzuia ukiukaji. Kwa mfano, tishio la kifo lilitosemekana kufanywa dhidi ya mwanasheria wa haki za binadamu katika kukabiliana na kazi yake ya haki za binadamu yangeweza kushughulikiwa kwa njia ya barua ya hatua ya haraka.

Barua ya madai hutumika kuwasilisha habari kuhusu ukiukaji ambao unasemekana tayari umeshatokea na ambao athari yake kwa mtetezi wa haki za binadamu aliyeathirika haiwezi tena kubadilika. Aina hii ya barua hutumika, kwa mfano, pale ambapo taarifa humfikia Mwandishi Maalum muda mrefu baada ya ukiukaji wa haki za binadamu kufanyika na kufikia hitimisho. Kwa mfano, ambapo mtetezi wa haki za binadamu ameuawa, suala hili litawasilishwa na Nchi kwa njia ya barua ya madai. Barua za madai hulenga hasa katika kuomba mamlaka za Nchi kuchunguza matukio hayo na kuendesha mashitaka ya jinai ya wale waliohusika.

Katika aina zote mbili za barua, Mwandishi Maalum huiomba Serikali husika kuchukua hatua zote zinazofaa katika kuchunguza na kushughulikia matukio hayo ya madai na kuwasilisha matokeo ya uchunguzi na hatua zake.

#### **(H) Ziara za Nchi**

Mwandishi Maalum amepewa madaraka ya kufanya ziara rasmi katika Madola. Baadhi ya Nchi zimetoa mialiko ya kudumu kwa Taratibu Maalum zote za Umoja wa Mataifa, na wakati mwingine Mwandishi Maalum huiandikia Serikali kuomba mwaliko urefushwe. Ziara hizi hutoa fursa ya kuchunguza kwa kina wajibu na hali ya watetezi wa haki za

binadamu nchini, kutambua matatizo maalum na kutoa mapendekezo juu ya jinsi matatizo hayo yanavyoweza kutatuliwa. Kwa msingi wa madaraka yake, Mwandishi Maalum anatakiwa kuangalia kwa makini hali ya watetezi wa haki za binadamu nchini. Hata hivyo, mchakato huu unadhamiriwa kutoa tathmini huru na isiyo na upendeleo, ambayo itakuwa ya msaada kwa watendaji wote katika kuimarisha mchango wa watetezi wa haki za binadamu hali kadhalika ulinzi wao.

#### **(I) Taarifa ya Mwaka kwa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa**

Mwandishi Maalum huwasilisha taarifa ya mwaka kwa Mkutano Mkuu hali kadhalika kwa Baraza la Haki za Binadamu akielezea shughuli yake ya mwaka, ugunduzi, na mapendekezo, ikiwa ni pamoja na kesi zote alizoshughulikia na majibu yoyote kutoka kwa Mataifa tokana na hatua za haraka au barua za madai.

Tangu kuanzishwa kwa madaraka haya, wakati wa vikao vya Mkutano Mkuu na vilevile Baraza la Haki za Binadamu, washika madaraka hawa wawili hadi sasa wamekuwa na taarifa madhubuti za umma zikilaani tabia ya Madola kwa watetezi wanaofanya kazi katika ngazi ya kitaifa, zikitilia mkazo juu ya ukweli kwamba baadhi ya watetezi huwa hatarini zaidi wakati wa vipindi vya uchaguzi wa kitaifa wanapajaribu kushiriki katika mchakato wa uchaguzi wa kitaifa.

Mshika madaraka wa sasa, Bibi Margaret Sekaggya, pia ametoa taarifa juu ya masuala muhimu kuhusiana na mada hii. Mwaka 2010, taarifa yake juu ya hali ya watetezi wanawake wa haki za binadamu iligusa masuala makubwa ya tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi na utambulisho wa kijinsia. Taarifa ya hivi karibuni inachukua muundo wa ufanuzi juu ya Azimio hili, ikitoa uchambuzi wa haki zilizomo humo. Chombo hiki chenye manufaa cha kumbukumbu za watetezi wa haki za binadamu kinapatikana kwenye tovuti ya OHCHR katika:

[http://www.ohchr.org/  
Documents/Issues/Defenders/  
CommentarytoDeclarationondefendersJuly2011.pdf](http://www.ohchr.org/Documents/Issues/Defenders/CommentarytoDeclarationondefendersJuly2011.pdf)

Maeleo ya anwani kwa kupeleka mapendekezo na kwa mawasiliano zaidi Mwandishi Maalum juu ya hali ya watetezi wa haki za binadamu, Bibi. Margaret Sekaggya k/k Ofisi ya Ubalozi wa Haki za Binadamu – Palais Wilson Ofisi ya Umoja wa Mataifa, Geneva CH 1211 Geneva 10 Switzerland

Kuwasilisha madai ya uvunjaji sheria dhidi ya mtetezi wa haki za binadamu:  
Barua pepe: urgent-action@ohchr.org au faksi: +41(0) 22.917.90.06

#### **Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu - Mwandishi Maalum kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

Katika kikao chake cha kawaida cha 35, kilichofanyika tarehe 21 Mei – 4 Juni 2004 huko Banjul, Gambia, Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu kiliamua kumteua Kamishna Janaiba Johm, kama Mwandishi Maalum mpya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu barani Afrika . Nafasi yake ilichukuliwa na Bibi Reine Alapini-Gansou mwezi Desemba, mwaka 2005, mwanasheria kutoka Benin, ambaye alishika nafasi hiyo hadi mwaka 2009. Mheshimiwa Mohamed Khalfallah alishika nafasi hii mwaka 2010, na kufuatiwa na Bibi Lucy Asuagbor kutoka mwezi Novemba mwaka 2010 hadi mwezi Novemba mwaka 2011. Kwa sasa nafasi hii imeshikwa tena na Bibi. Reine Alapini-Gansou. Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu ni chombo cha kwanza cha haki za binadamu kikanda kuunda utaratibu maalum wa kushughulikia ulinzi wa haki za watetezi.

Uamuzi wa kumteua Mwandishi Maalum wa watetezi wa haki za binadamu ni hatua ya kushughulikia hatari kubwa inayowakabili watetezi katika Afrika na haja ya kujenga msisitizo maalum ndani ya Tume ili kuchunguza, kutoa taarifa na kuchukua hatua juu ya taarifa kuhusu hali ya watetezi barani.

Tume iliamua kumkabidhi Mwandishi Maalum madaraka yafuatayo:

- Kutafuta, kupokea, kuchunguza na kuchukua hatua juu ya taarifa ya hali ya watetezi wa haki za binadamu katika Afrika;
- Kuwasilisha taarifa katika Kikao cha Kawaida cha Tume ya Afrika juu ya hali ya watetezi wa haki za binadamu barani Afrika;
- Kushirikiana na kuanzisha mazungumzo na nchi wanachama, Taasisi za Taifa za Haki za Binadamu, mabaraza baina ya serikali husika, mifumo ya kimataifa na ya kikanda ya ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu, watetezi wa haki za binadamu na wadau wengine;
- Kuendeleza na kupendekeza mikakati madhubuti

ya ulinzi bora kwa watetezi wa haki za binadamu na kufuatilia mapendekezo yake;

- Kuongeza ufahamu na kuhimiza utekelezaji wa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu barani Afrika.
- Ili kutekeleza madaraka yake, Mwandishi Maalum hypokea na kuchunguza taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, na masuala ya rufaa za haraka kuhusu uvunjaji sheria dhidi ya watetezi wa haki za binadamu katika kanda.

Tangu kuanzishwa kwa madaraka haya, Waandishi Maalum pia wamedumisha mawasiliano ya mara kwa mara na watetezi wa haki za binadamu kuitia ushiriki wao katika mikutano ya kimataifa na kikanda. Washika madaraka hawa pia walifanya ziara kadhaa za nchi, ikiwa ni pamoja na ziara ya pamoja na taarifa kwa vyombo vya habari na Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa (tazama hapo juu).

Vilevile Mwandishi Maalum amewahamasisha watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasilisha kesi kuhusiana na watetezi wa haki za binadamu kwa Tume ya Afrika. Chini ya Mkatiba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu, Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu inapewa madaraka ya kupokea na kushughulikia mawazo kutoka kwa watu binafsi na mashirika (Kifungu cha 55). Mtu ye yeyote anaweza kuwasilisha ujumbe kwa Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu kukemea ukiukwaji wa haki za binadamu. Mlalamikaji au mwandishi wa ujumbe huo si lazima ahusiane na mtendewa kinyume cha haki, lakini mwathirika huyo lazima atajwe. Mawazo yote lazima yaandikwe, na kutumwa kwa Katibu au Mwenyekiti wa Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu. Hakuna fomu au muundo maalum ambao lazima ufuatwe katika kuandika mawazo hayo.

Maelezo ya anwani kwa kupeleka mapendekezo na mawasiliano zaidi:

Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu  
31 Bijilo Annex Layout, Wilaya ya Kaskazini ya Kombo  
Mkoo wa Magharibi  
S.L.B. 673

Banjul, Gambia

## **Miongozo ya Umoja Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

Umoja wa Nchi za Ulaya kwanza ulipitisha  
“Kuhakikisha Ulinzi - Miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu”  
mwezi Juni 2004, na toleo jipyia lilisambazwa katika

mwaka 2008. Miongozo<sup>2</sup> hii inatoa mapendekezo yanayotekelzeza kwa ajili ya kuimarisha hatua za Umoja wa Nchi za Ulaya kuunga mkono mawasiliano ya watetezi wa haki za binadamu katika balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na nchi zinazoendelea katika ngazi zote pamoja na katika mikutano ya haki za binadamu ya vyombo mbalimbali, kama vile Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Miongozo hii ni sehemu ya jitihada za Umoja wa Nchi za Ulaya kuhimiza heshima ya haki ya kutetea haki za binadamu. Hutoa mwongozo kwa vitendo kwa ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya katika nchi zinazoendelea juu ya hatua wanazoweza kuchukua kwa niaba ya watetezi wa haki za binadamu walio hatarini, na kupendekeza njia za kuunga mkono na kusaidia watetezi wa haki za binadamu, katika mukhtadha wa Sera ya Pamoja ya Nje na Usalama ya Umoja wa Nchi za Ulaya.

Miongozo hii pia hutoa msaada kwa ajili ya Taratibu Maalum za Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ikiwa ni pamoja na Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu, na mifumo mingine ya kikanda (kama vile Mwandishi Maalum wa Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu kuhusu watetezi wa haki za binadamu). Umoja wa Nchi za Ulaya husaidia kanuni zilizomo katika Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu.

## **Hatua za vitendo**

### **a) Ufuatiliaji, utoaji taarifa na tathmini.**

Wakuu wa Balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya tayari wanaombwa kutoa taarifa za mara kwa mara juu ya hali ya haki za binadamu katika nchi ambazo zimeteuliwa. Balozi mbalimbali zinatarajiwa kushughulikia hali ya watetezi wa haki za binadamu katika taarifa zao, zikibainisha hasa tukio la vitisho au mashambulizi yoyote dhidi ya watetezi wa haki za binadamu.

### **b) Wajibu wa Balozi za Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya katika kuwasaidia na kuwalinda watetezi wa haki za binadamu.**

Ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya (yaani, balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya) wanafanya kazi kubwa katika kutekeleza sera za Umoja wa Nchi za Ulaya kwa watetezi wa haki za binadamu. Balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na

2 Inapatikana katika <http://www.consilium.europa.eu/uedocs/cmsUpload/GuidelinesDefenders.pdf>

ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya wanatarajiwa kwa kadri inavyowezekana, kupitisha sera makini kwa watetezi wa haki za binadamu, wakati wote wakinambua kuwa katika mazingira fulani hatua ya Umoja wa Nchi za Ulaya inaweza kusababisha vitisho au mashambulizi dhidi ya watetezi wa haki za binadamu. Kabla ya kuchukua hatua, balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya wanapaswa kushauriana na watetezi wa haki za binadamu. Taarifa mrejesho itolewe kwa watetezi wa haki za binadamu na familia zao kufuatia hatua yoyote iliyochukuliwa. Hatua ambazo balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya wanaweza kuchukua, kulingana na mazingira maalum, japo si zote, ni pamoja na:

- Kuandaa mikakati ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miongozo hii, kwa kuzingatia hasa watetezi wanawake wa haki za binadamu. Balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya wanatarajiwa kuzingatia kuwa Miongozo hii inahusu watetezi wa haki za binadamu ambao huendeleza na kulinda haki za binadamu, ziwe ni za kiraia, kitamaduni, kiuchumi, kisiasa au kijamii. Balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya lazima wahusishe watetezi wa haki za binadamu na mashirika yao katika maaandalizi na ufuutilaji wa mikakati ya ndani. Watetezi wa haki za binadamu lazima washinikize ili kuhakikisha kuwa mikakati hii ya utekelezaji ya ndani huonyesha mazingira maalum ya nchini na ina mwenendo stahiki kwa mazingira yao ya kazi;
- Kuandaa mikutano wa watetezi wa haki za binadamu na wanadiplomasia angalau mara moja kwa mwaka ili kujadili mada kama vile hali ya haki za binadamu nchini, sera ya Umoja wa Nchi za Ulaya katika mada hii, na matumizi ya mikakati wa ndani katika utekelezaji wa Miongozo ya Umoja wa Nchi za Ulaya kuhusu watetezi wa haki za binadamu;
- Kuratibu kwa karibu na kupeana taarifa juu ya watetezi wa haki za binadamu wakiwemo wale walio hatarini;
- Kudumisha mawasiliano stahiki na watetezi wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kuwapokea katika balozi na kutembelea maeneo yao ya kazi (Balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za

Ulaya zinaombwa kuzingatia uteuzi wa Maafisa Ushirikiano maalum kushiriki mzigo wa jukumu hili);

- Kuwasifu wazi, watetezi wa haki za binadamu, kama na pale inapostahili, kwa njia ya kuwatangaza, ziara au mialiko stahiki;
- Pale inapofaa, kuwatembelea watetezi wa haki za binadamu walio kifungoni au kifungo cha nyumbani na kuhudhuria kesi zao kama watazamaji.

**c) Kukuza heshima kwa watetezi wa haki za binadamu katika mahusiano na nchi zinazoendelea na katika mikutano ya mataifa mbalimbali.**

Lengo la balozi za nchi wanachama wa Umoja wa Nchi za Ulaya na ujumbe wa Umoja wa Nchi za Ulaya lililoelezwa, ni kuzishawishi nchi zinazoendelea kutimiza wajibu wao wa kuheshimu haki za watetezi wa haki za binadamu na kuwalinda kutopteka na mashambulizi na vitisho kutoka kwa watendaji wasiokuwa wa Serikali. Inapobidi, Umoja wa Nchi za Ulaya unatarajiwa kueleza umuhimu wa nchi zote kuzingatia na kufuata kanuni na viwango husika vya kimataifa, hasa Azimio la Umoja wa Mataifa, kwa lengo zima la kujenga mazingira ambayo watetezi wa haki za binadamu wanaweza kufanya kazi kwa uhuru.

Hatua zinazofaa ni pamoja na:

- Mikutano kati ya ngazi ya juu ya wawakilishi wa Umoja wa Nchi za Ulaya na watetezi wa haki za binadamu wakati wa ziara zao za nchi, na kujadili kesi za watetezi mmoja mmoja wa haki za binadamu na mamlaka zinazohusika pale inapobidi;
- Pale inapofaa, pamoja na hali ya watetezi wa haki za binadamu katika kipengele cha haki za binadamu cha mazungumzo ya kisiasa kati ya Umoja wa Nchi za Ulaya na nchi zinazoendelea na mashirika ya kikanda. Umoja wa Nchi za Ulaya utasisitiza msaada wake kwa watetezi wa haki za binadamu na kazi yao, na kujadili matatizo binafsi inapobidi;
- Kufanya kazi kwa karibu na nchi nyingine zenye mwelekeo unaofanana hasa katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa na Mikutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa;
- Kuendeleza uimarishaji wa mifumo ya kikanda

iliyopo kwa ajili ya ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu na uundaji wa mifumo stahiki katika kanda ambazo hakuna.

**(d) Msaada wa vitendo kwa watetezi wa Haki za Binadamu ukiwemo kupitia Sera ya Maendeleo.**

Kuna aina mbalimbali za mifumo ya msaada wa vitendo wanaopata watetezi wa haki za binadamu kupitia programu ya Umoja wa Nchi za Ulaya na Nchi zake wanachama kwa lengo la kusaidia maendeleo ya michakato na taasisi za kidemokrasia, na uendelezaji na ulinzi wa haki za binadamu katika nchi zinazoendelea - kama vile Chombo cha Ulaya cha Demokrasia na Haki za Binadamu.

Msaada wa vitendo kama ulivytarajiwa chini ya Miongozo hii si msaada wa kifedha pekee. Mifano ifuatayo imejumuishwa katika Miongozo hiyo:

- Programu za haki za binadamu na kuleta demokrasia, za Umoja wa Nchi za Ulaya na nchi wanachama zinapaswa kuzingatia zaidi haja ya kusaidia maendeleo ya michakato na taasisi za kidemokrasia, na uendelezaji na ulinzi wa haki za binadamu katika nchi zinazoendelea, kati ya mambo mengine yanayowasaidia watetezi wa haki za binadamu, kupitia shughuli kama vile kampeni za kujenga uwezo na kuhamasisha umma;
- Kwa kuhimiza na kuunga mkono uimarishaji, na kazi ya vyombo vyaya kitaifa kwa ajili ya uendelezaji na ulinzi wa haki za binadamu, zilizoundwa kwa mujibu wa Kanuni za Paris, ikiwa ni pamoja na Taasisi za Taifa za Haki za Binadamu, Ofisi za Ombudsman na Tume za Haki za Binadamu;
- Kusaidia uimarishaji wa mitandao ya watetezi wa haki za binadamu katika ngazi ya kimataifa ikiwa ni pamoja na kuwezesha mikutano ya watetezi wa haki za binadamu;
- Kujaribu kuhakikisha kuwa watetezi wa haki za binadamu katika nchi zinazoendelea wanaweza kupata nyenzo, zikiwemo fedha, kutoka nje ya nchi;
- Kwa kuhakikisha kwamba programu za elimu ya haki za binadamu zinaendeleza, kati ya mambo

mengine, Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu.

**Hitimisho**

Licha ya ulinzi wanaopewa na Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya watetezi wa haki za binadamu, na zaidi ya miaka kumi ya utekelezaji kwa vitendo, hali ya watetezi wa haki za binadamu hajaboreka. Mazingira ambayo watetezi wa haki za binadamu hufanya kazi katika nchi nyingi yanakuwa ya uhasama zaidi na zaidi, yakikwamisha nafasi ya mazungumzo. Wale wanaotetea haki za binadamu wanaendelea kuwa katika hali ngumu kwa ujasiri wao. Kazi yao inawaweka katika hatari kubwa kibinaksi na kitaaluma, ikiwa ni pamoja na hatari kwa familia zao, rafiki zao na washirika wao.

Vyama vya kiraia havijanufaika kikamilifu kwa maudhui ya Azimio hili. Mamlaka za taifa kuendeleza utekelezaji wa Azimio bado ni changamoto kubwa.

Kuna haja ya chama cha kiraia cha Afrika kuendeleza na kukubali dhana pana ya pamoja na ufanuzi wa istilahi ‘mtetezi wa haki za binadamu’ kujumuisha na wale wanaoendeleza na kulinda haki za kiraia na kisiasa, na pia wale wanaoendeleza na kulinda haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwa ni pamoja na harakati za kijamii, harakati za kupambana dhidi ya utandawazi wa kiuchumi, wanaharakati wa amani, wanaharakati wanaounga mkono demokrasia na kupambana na rushwa, harakati za haki za wanawake, wale wanaopigania kundi la wachache (ikiwa ni pamoja na wasagaji, mashoga, wafanyao mapenzi na watu wa jinsi zote mbili, wenye jinsi mbili na wenye jinsi tata) na haki za wazawa, wale wanaofanya kazi fursa sawa za afya, elimu, maji na mazingira ya afya na haki ya maendeleo.

Kushirikiana na kujenga mtandao katika ngazi ya kitaifa, kanda ndogo na ya kanda imekuwa ikichukuliwa na watu wengi kama moja ya vyombo vyaya kuleta ufanisi zaidi ambavyo vyama vya kiraia vinapaswa kuvitumia katika kufanya kampeni kwa ajili ya mazingira bora ya haki za binadamu.

Juhudi za ufuutiliaji wa mikakati hiyo, pamoja na ushirikiano na mifumo ya kikanda na kimataifa kwa ajili ya watetezi wa haki za binadamu ni muhimu kwa kufanikisha ulinzi mkubwa zaidi, kutambulika na uhalali kwa watetezi wa haki za binadamu barani Afrika, ili kuwawezesha kufanya kazi ya haki za binadamu kwa ufanisi zaidi, na hivyo, kupuanua mazingira ambayo watetezi wa haki za binadamu wanaweza kutumia haki yao ya kutetea haki za binadamu.

# Sura ya 2

## Watetezi wa Haki za Binadamu katika Vitisho: Mtazamo wa Usalama Ugani kwa Kazi yao

Changamoto zinazowakibili watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi katika vitisho, zinafanya haja ya kuwa na mifumo madhubuti na inayoweza kubadilika kulingana na mahitaji ya usalama. Kufahamu mukhtadha wa kazi zao au “kujali”, hakuwezi kujibu maswali yote: lazima tuchukue hatua zaidi na kujadili mfumo wa usimamizi wa usalama. Katika kitabu hiki, tunapendekeza muundo wa jumla kwa ajili ya mchakato wa usimamizi wa usalama na mtazamo wa ziada kwa usimamizi wa usalama pamoja na vigezo juu ya dhana za msingi kama vile hatari, uwezekano wa kudhurika na vitisho. Tunajumuisha pia mapendekezo ya kuboresha na kukuza kiwango cha usalama kwa ajili ya watetezi wa haki za binadamu kufanya kazi. Mada zote hizi lazima ziyawezeshe mashirika yasiyo ya kiserikali na watetezi kuunda mikakati bora inayoendana na ongezeko la changamoto za usalama wa kazi ya haki za binadamu.<sup>3</sup>

### Kutoa mawazo muhimu

Katika miaka kadhaa iliyopita, utambuzi wa jumla kuhusu hatari kubwa inayowakibili watetezi wa haki za binadamu kutokana na kazi yao umeongezeka. Hatari hiyo inaweza kugundulika kwa urahisi wakati watetezi wanapofanya kazi katika mazingira ya uhasama (hii hutokea wakati sheria za nchi zinapotoa adhabu kwa baadhi ya vipengele vya kazi ya haki za binadamu); vilevile watetezi huonekana kuwa hatarini pale sheria katika nchi yao inapoidhinisha kikamilifu kazi ya haki za binadamu, lakini kutoadhibiwa kwa wale wanaowatishia au kuwashambulia watetezi wa haki za binadamu huwa jambo la kawaida. Hali huwa mbaya zaidi mahali pakiwa na mgogoro wa kutumia silaha.

Nje ya hali chache zenyе machafuko (ambapo maisha ya mtetezi yanaweza kuwa mikononi mwa maaskari katika kituo cha ukaguzi), hatuwezi kusema kuwa utumiaji nguvu dhidi ya watetezi hauna utaratibu; katika matukio mengi utumiaji nguvu kama huo huhusishwa na malengo ya jeshi la kawaida au jeshi la kisiasa kwa wavamizi. Kufahamu hali ya migogoro kiasi cha kutosha na kuelewa mantiki ya jeshi la kisiasa ni vipengele muhimu vya kusimamia usalama wa watetezi wa haki za binadamu kwa usahihi.

Kitabu hiki hakitoi “ufumbuzi wa marekebisheso

kulingana na malengo” tayari kwa kutumika, bali kinachunguza mikakati ilio muhimu katika kuboresha usimamizi wa usalama wa mtetezi. Katika miaka kadhaa iliyopita, mashirika yasiyo ya kiserikali ya ufadhilli ya kimataifa, yameunda mikakati na taratibu zao za usalama kwa kuzingatia usimamizi wa usalama. Kwa kuwa yote hutokea mara nyingi sana, mikakati hii hajarekeblishwa na kuhamishiwa katika ulimwengu wa mtetezi wa haki za binadamu, na hii ni kazi inayosubiri kutekelezwa.

Kwa vyovypote inabidi tufahamu kuwa, chanzo kikuu cha hatari kwa watetezi ni ukweli kwamba vitisho hivyo mara nyingi hutokea kuwa mashambulizi halisi, yaliyofanywa kwa utashi wa mshambulizi na mbinu na uhuru wa kutoadhibiwa wanaoutumia. Kwa ajili hiyo, chombo muhimu zaidi kwa kulinda watetezi ni hatua ya kisiasa kwa sababu, nje ya ushauri wa kiufundi, suala kubwa ambalo bado linahitaji kushughulikiwa ni haja ya serikali mbalimbali na vyama vya kiraia kutumia shinikizo linalohitajika na kuchukua hatua muhimu dhidi ya wale ambao siku baada ya siku huwapa vitisho, huwanyanyasa na kuwaua watetezi wa haki za binadamu.

Hata hivyo, watetezi wangeweza kupata mafanikio makubwa katika usalama wao iwapo wangefuata mikakati na taratibu fulani ambazo zimefanyiwa majoribio na zinfaa. Ili kujua kwamba hii ina udhaifu, lakini ni ya manufaa, ni juhud, sasa tunataku kuangalia mapendekezo ya kuboresha usalama wa watetezi.

### Usimamizi wa salama dhidi ya taratibu za usalama

Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa watetezi wa haki za binadamu wengi walio katika vitisho hawana mikakati ya usalama. Hata wale wachache walio nayo (kwa kawaida katika mukhtadha wa kazi zao za mashirika yasiyo ya kiserikali), mpango wao wa usalama unaweza kuwa na mlolongo wa hatua za ulinzi, mipango ya dharura na kanuni za usalama, ambazo zinaweza kuwa na manufaa kama miongozo ya usalama bila kufahamu ukweli kuwa usalama unahitaji usimamizi wa kutosha wa ujumla, na ina maana zaidi ya mpango wa usalama. Usalama hushughulikia vipengele vyote vya kazi ya shirika lisilo la kiserikali: inahusu shughuli (oyote inayodhamiria kuwa shirika linaweza kudhurika inaweza kuwa matokeo ya shughuli zake), pamoja

<sup>3</sup> Makala iliyoandikwa na Luis Enrique Eguren.

na kutathmini hali inayobadilika (na hali za migogoro zinaweza kubadilika haraka), pamoja na mtiririko wa taarifa (kuweka kumbukumbu na kutathmini matukio ya usalama), na utumishi (toka kuajiri hadi kutoa mafunzo na kujenga timu), pamoja na kuandaa bajeti na kugharamia na kadhalika.


Swali linalobaki ni: jinsi gani tunaweza kufanikisha uunganishaji muhimu wa usalama katika masuala yote ya usimamizi wa kazi ya mashirika yasiyo ya kiserikali? Tunafahamu kwamba mapungufu yapo na mapungufu hayo kuhusu usalama ni sawa na yale yahusuyo kazi ya haki za binadamu: uhaba wa nyenzo, uchache wa wafanyakazi, kufanya kazi bila kuijandaa, kiwango kikubwa cha shinikizo na udhalimu, nk

### **Mikakati ya usalama na uhuru wa kazi: idhini/ushauri wa pembetatu**

Mikakati yote ya usalama inaweza kufupishwa katika sentensi moja: kuweka uhuru wa kazi wazi. Hivyo tunahitaji kutafuta, kwa kiwango cha chini, idhini (ya serikali, ya watendaji wanaotumia silaha na vyama vya kiraia) na kukubalika kikamilifu (hatua zaidi).

Kusema kweli kwa kigezo cha usalama, uhuru wa kazi ya watetezi unahitaji ridhaa fulani toka kwa pande zinazohusika na mgogoro, hasa wale wenye silaha, na inafaa zaidi liwe ombi kutoka sehemu fulani ya sekta zilizoathirika na mgogoro huo. Ridhaa hii inaweza kuwa dhahiri (kibali rasmi kutoka kwa mamlaka) au itajitokeza bila kutajwa bayana, na itakuwa thabit zaidi ikiwa mtendaji wa kutumia silaha ataona manufaa kutokana na kazi ya watetezi, au kuidharau kama ataona itamgharimu. Kwa hali hii, ridhaa itatolewa kwa gharama za kisiasa zilizofanywa na mashambulizi dhidi ya watetezi. Yote haya ni muhimu watetezi wanapofanya kazi katika mazingira yenye zaidi ya mtendaji mmoja anayetumia silaha.

Uhuru wa kazi unaweza kuwakilishwa kama pembetatu ambayo inahusiana na makubaliano ya idhini na ushawishi wa silaha za kuzuia mashambulizi:



Ukuzaji wa uhuru wa kazi unaweza kupatikana kwa muda (kufuatia kukubali kwake kwa njia ya mkakati wa ushawishi, ambao unapaswa kuzingatia kupanga kwa ajili ya mahitaji ya watu, taswira, taratibu, muungano, nk), au kwa kukubali kwa upande wa watendaji wenye silaha (uwiano mgumu, unaowakilishwa katika eneo "b"). Lakini kwa kawaida katika maeneo ya migogoro eneo huwa dogo kwa lile linalofuata kutokana na ridhaa ya watendaji wa kutumia silaha, mchanganyiko wa ushawishi wa kuzuia na ushawishi wa kutenda (uliopunguzwa kuwa eneo "a").

### **Hatari, vitisho na uwezekano wa kudhurika: Uwezo katika usalama**

Hatari ni sehemu ya msingi ya kazi katika mazingira ya mgogoro. Hakuna ufanuzi wa hatari unaokubalika sana, lakini tunaweza kusema kuwa hatari inahusu "matukio yanayoweza kutokea, hata kama hayana uhakika, ambayo yataleta madhara".<sup>4</sup>

Katika mazingira ya aina yoyote, watetezi hawana uwezekano sawa wa kudhurika katika ile **hatari** ya jumla kwenye tukio hilo hilo la mgogoro.

**Uwezekano wa kudhurika** (uwezekano ambao mtetezi atapata shambulio na madhara ya aina yoyote) hutofautiana kutegemeana na mambo kadhaa, hivyo shirika la Umoja wa Mataifa haliwezi kudhurika sawa na shirika dogo la taifa lisilo la kiserikali.

Kiwango cha hatari ya shirika lisilo la kiserikali kinategemea **vitisho** liliyopata na uwezekano wa kudhurika kwa vitisho hivyo, kama vinavyoweza kuonekana katika mlinganyo<sup>5</sup> ufuatao:

### **Hatari = vitisho x uwezekano wa kudhurika**

**Vitisho** ni uwezekano ambao mtu atamdhuru mtu mwagine (mwili wake, uadilifu wa mawazo yake au mali yake), kwa kitendo cha kutumia nguvu mara kwa mara kwa makusudi<sup>6</sup>. Tathmini ya tishio ni uchambuzi wa uelekeo wa tishio kuwa kitendo.

Shirika lisilo la kiserikali linaweza kukabiliwa na vitisho vingi vya aina mbalimbali katika mazingira ya mgogoro. Vitisho vikuu ni vile vinavyodhamiria kuweka kipingamizi au kubadilisha kazi ya shirika lisilo la kiserikali au kushawishi mwenendo wa wafanyakazi wake ('kulenga'). Kulenga inahusiana kwa karibu na kazi inayofanywa na watetezi na kwa utashi wa watendaji wenye silaha; kwa maneno

4 López y Luján (2000), uk..23

5 Ver Koenraad van Brabant REDR en la bibliografía seleccio-nada.

6 Dworken (1999).

mengine, iwapo mtetezi anakuwa mlengwa au la hutegemea matokeo ya kazi yao kwa watendaji wa kutumia silaha.

**Uwezekano wa kudhurika** (kiwango ambacho watetezi ni rahisi kukabiliwa na hasara, uharibifu, mateso, na kifo, katika tukio la mashambulizi) hutofautiana kwa kila mtetezi au shirika lisilo la kiserikali, na pia hutofautiana kutokana na muda. Uwezekano wa kudhurika ni kipimo husika, kwa kuwa watu wote na makundi yote yana uwezekano wa kudhurika, lakini kila moja, kulingana na mazingira na hali zao na hili lina **kiwango na aina** yake lenyewe ya uwezekano wa kudhurika. Kwa mfano, mtetezi wa haki za binadamu ana uwezekano zaidi wa kudhurika anapokuwa nje, barabarani kuliko anapokuwa ofisini kwake (iwapo imelindwa vizuri).

Uwezekano wa kudhurika kwa shirika lisilo la kiserikali linaweza kuonekana kuathirika kwa sababu mbalimbali, kama vile kuachwa wazi (kiwango ambacho mfanyakazi na mali ya shirika lisilo la kiserikali inakuwa katika mahali hatari au pasipolindwa), athari ya mpango wa kazi (ikiwa kazi ya shirika lisilo la kiserikali ina athari mbaya kwa mtendaji yeyote anayetumia silaha, huliweka shirika hilo lisilo la kiserikali katika uwezekano wa kudhurika) n.k.<sup>7</sup>

**Uwezo** ni nguvu na rasilimali zilizopo kwa kundi au mtu binafsi ili kufikia kiwango cha kuridhisha cha usalama (au heshima kwa haki zao/zake za binadamu). Mifano ya uwezo ni mafunzo (katika usalama, katika masuala ya kisheria, nk), kazi ya kikundi kama timu, nk.

Hatari iliyosababishwa na tishio na uwezekano wa kudhurika vinaweza kupungua ikiwa watetezi wana uwezo wa kutosha (kadri kunapokuwa na uwezo zaidi, ndivyo kadri hatari inavyopungua):

#### **Hatari = vitisho x uwezekano wa kudhurika**


#### **UWEZO**

Kwa kuweka muhtasari wa aya zilizotangulia katika kielelezo tunachofanya kazi, ili kupungua hatari kwa viwango vinavyokubalika inabidi:

- Kupungua vitisho
- Kupungua/kuboresha mambo yanayofanya uwezekano wa kudhurika

<sup>7</sup> Kikomo muhimu cha urefu wa makala hii kinatufanya tusiingize kielelezo chenye maelezo ya kina kuhusu aina na kazi ya sababu kuu za uwezekano wa kudhurika.

- Kuongeza uwezo wa usalama kwa mafunzo ya usalama katika usalama, tathmini ya hatari nk



Lazima tuzingatie kuwa hatari ni dhana inayobadilika na hubadilika kulingana na wakati, ikifuata mabadiliko katika vitisho, uwezekano wa kudhurika na uwezo. Inafanya haja ya kutathmini hatari mara kwa mara, na hasa ikiwa kuna mabadiliko katika mazingira ya kazi, katika vitisho au katika uwezekano wa kudhurika. Kwa mfano, hatari huongezeka zaidi mtendaji anaposikia kuzungukwa; uwezekano wa kudhurika huongezeka mfanyakazi mpya wa kutumia silaha anapoanza kufanya kazi bila mafunzo stahiki.

Hatua za usalama kama kamera ya video au gari lenye kinga zinaweza kupungua hatari kwa kuyavunja nguvu mambo yanayoleta uwezekano wa kudhurika, lakini hatua hizo hazikabiliani na chanzo kikuu cha hatari, ambacho hutokana na vitisho na shauku ya kuzitumia, ikiwa hatua dhidi ya watetezi hazitolewi adhabu. Kwa sababu hizi, hatua zote kubwa katika ulinzi zinapaswa zilenge kupungua vitisho hivyo, pamoja na mambo yanayopunguza uwezekano wa kudhurika.

#### **Kupanga mipango ya kazi na usalama**

Usimamizi wa usalama lazima uingizwe katika kila hatua iliyofanyiwa uchambuzi wakati wa kuunda mpango wa kazi.

Usalama una pembe maalum unapofanya uchambuzi wa mazingira na kuweka malengo na madhumuni ya kazi, vile vile wakati wa kuunda mpango wa kazi, kufuatilia na kutathmini matokeo yake. Miongozo ya usalama ina mahali maalum (katika hatua ya kupanga) katika mchakato mzima, ambapo zinakuwa nyaraka hai ambazo hupata

taarifa mrejesho tokana na hatua za ufuatiliaji na tathmini.

## Kukabiliana na changamoto za usalama: usimamizi wa usalama kama mchakato wa ziada

Usimamizi wa usalama kamwe haukamiliki, na daima una upendeleo na ubaguzi. Kuna mipaka inayolazimisha mfumo<sup>8</sup> huu; mipaka inayotambulika (si mambo yote yanayoathiri usalama huweza kuwekwa pamoja na kushughulikiwa kwa wakati mmoja) na mipaka katika mchakato (upangaji muda na mtiririko wa masharti muhimu kwa kujenga ufahamu, kufanya makubaliano, kuwapa watu mafunzo, kuhakikisha kuna wafanyakazi wa kutosha, kutekeleza shughuli, nk). Ni mara chache Usimamizi wa usalama huweza kujaribu kuwa na mtazamo madhubuti, wa muda mrefu: Mchango wake hutegemea uwezo wake wa kuzuia matukio na kuashiria haja ya ushirikiano na uratibu kwa asasi ili kukabiliana na matukio hayo. Labda hii si juhudu kubwa sana, lakini pia inabidi kuzingatia kuwa kwa kawaida rasilimali chache hutengwa kwa ajili ya usalama, hivyo hatuwezi kamwe kuwa madhubuti. Umakini ni jambo la lazima katika usimamizi wa usalama.

Kama tulivyosema kabla, tunapopitia matendo ya usalama wa mashirika yasiyo ya kiserikali unaweza kuona aina fulani ya miongozo au mipango au hatua za usalama au mielekeo ya tabia zinazoendelea. Kuna vikundi vingi vilivyo hatarini, kutoptana na mtindo usiobadilika kuhusu utaratibu wa usalama kukataa kuongeza uzito wa kazi uliopo kwa kuchanganya na shughuli mpya za usalama. Utaratibu wa usalama kama kawaida umegawanyika, una mabadiliko na unaeleweka sana. Kwa upande wa usimamizi wa usalama ni muhimu kuendelea hatua kwa hatua, kufanya mabadiliko ya ziada ili kuboresha utendaji. Mikakati na "taratibu za usalama hutokea kwenye mifumo midogo ya mkakati", ambapo kila mmoja unashughulikia eneo maalum la kazi (mipango, timu ya ugani hasa inayohusika na usalama wake, meneja wa makao makuu katika shinikizo la masuala ya mfadhili ya usalama, nk.). Uongezekaji<sup>9</sup> katika usimamizi wa usalama unafungua njia isyo rasmi na kutoa nafasi kwa ajili ya msingi wa mawakala wa mabadiliko mahali pa kazi. Matukio ya haraka (kama vile matukio ya usalama) hushawishi maamuzi ya

haraka na ya muda ambayo hurekebisha utaratibu wa usalama na kwamba, kama itasimamiwa vizuri, huwa sehemu ya makubaliano yaliyoshirikisha wengi kwa ajili ya kuchukua hatua mionganoni mwa wanachama wa ugani na timu ya usimamizi.

## Dhana muhimu kwa ajili ya usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu

*Watetezi wa haki za binadamu ni watu wa kawaida ambao hujitolea kuijingiza hatarini*

Hakuna mtu aliyezaliwa kuwa mtetezi wa haki za binadamu. Watetezi ni watu wa kawaida ambao hujitolea kuijingiza hatarini, ama katika kazi zao au katika shughuli zao mbali na kazi zao. Kwa ujumla wao hufanya hivyo katika muktadha wa maisha yao ya kawaida, pamoja na familia na rafiki zao. Mambo yote haya yana ushawishi wazi juu ya mtazamo wa watetezi wa hatari, na hivyo katika mikakati yao ya usalama. Kwa wakati wowote ule uliotolewa ambao mtetezi huanza kupata vitisho kwa mara ya kwanza, na katika kuendelea na kazi yake anaendelea kupata vitisho hivyo, inaweza kuwa ni mwanzo wa hali ya wasiwasi mkubwa kwa mtetezi huyo. Huo wasiwasi na utaratibu wa mtetezi kumudu hali hii lazima vizingatiwe wakati tunaposhughulikia mahitaji yao ya usalama.

Wakati watetezi wanakabiliwa na hatari, hufanya hivyo kama wanavyofanya wengine: Huendeleza tabia inayorekebishiwa na kujaribu kurahisisha mchakato wa kufanya maamuzi, katika kanuni za hali za kurekebisha jamii na kundi. Masomo ya kisaikolojia juu ya jinsi watu wanavyokabiliwa na hatari umeonyesha kuwa hatari hukubaliwa vizuri zaidi inapochukuliwa kwa hiari, wakati mtu anapotambua kwamba anaweza kuidhibiti hatari hiyo, na hatari hii inapokuwa imezoeleka<sup>10</sup>. Katika mtazamo wa kisisiolojia, hatari ni dhana za kijamii, ambazo zinahusiana na mambo ya utamaduni wa kijamii uliohusishwa na miundo ya kijamii<sup>11</sup>. Kwa ajili hiyo, kila sekta ya jamii huonyesha baadhi ya hatari na kusahau nytingine. Hivyo, utafiti wa anthropolojia ya utamaduni umeonyesha<sup>12</sup> kwamba kila mtu ana tabia fulani ya kukubali hatari, na tabia hii hutegemea na malipo yanayohusiana na hatari hizo na mitizamo ya mtu binafsi juu ya hatari hizo. Ni muhimu sana kutambua kuwa kukwepa hatari kwa binadamu hakukabiliani tu na uwezekano

8 Quinn, James B.: "Strategic change: logical incrementalism". Sloan Management Review Summer 1989 (uk.. 45-60)

9 Kuna tafti nyinyi kuhusu uongezekaji na mipango ya kimkakati. Mwelekeo huu ulioonyeshwa katika makala hii unatumia uzoefu wa C.E. Lindblom na James B. Quinn, na wengineo.

10 CrouchnaWilson(1982;uk..85-6),imenukuliwakatika López na Luján (2000; uk. 71)

11 López na Luján (2000; uk..72)

12 López and Luján (2000; uk.72)

uliotambuliwa kwamba utasababishwa na madhara hayo, lakini pia utayari wa kujiweka wazi katika hatari, fidia inayopatikana kwa ajili ya kukubali kuwa wazi hivi katika hatari, au haki katika uenezaji wa hatari.

Kujiweka wazi katika hatari kila siku kunaweza kujenga "tabia ya kutojihusisha" kwa uwazi, ikihiushisa na kukataa hatari, na ambayo humfanya mtu binafsi kufanya kazi ya kawaida bila kuchukua hatua za usalama na hata kukataa kuizungumzia mada hii.<sup>13</sup>

Kwa kuzingatia ukweli huu, wakati wa kushughulikia masuala ya usalama na watetezi, ni muhimu sana kuzingatia mtazamo hatari wa watetezi (unaohusishwa na sababu za kijamii na za kikundi, na tabia ya mtu binafsi) na kuzingatia pia dhana kama kujituma kwa mtu binafsi na kwa kikundi, haki za kijamii, uwezo wa uchambuzi, kufanya kazi kwa ushirikiano, nk

### **Athari za matukio yanayotia uchungu na kiwewe**

Watetezi wa haki za binadamu ama hushuhudia matukio ya kutia uchungu na kiwewe au wao huwa wahanga wa matukio hayo: Athari zake huathiri utimamu wa akili na tabia ya watetezi ya kikundi na ya mtu binafsi. Matokeo ya kawaida ni kuzidiwa na kazi kutokana na ongezeko la mahitaji ya kihisia yanayohusishwa na matukio ya kutia uchungu na kiwewe (hasira, kuchanganyikiwa, huzuni, nk). Wakati mwengine watetezi hujisikia kuwa na hatia kubwa (kwa kutoweza kuzuia tukio la kutia uchungu na kiwewe) na kisha wanaweza kujenga tabia ya hatari kubwa,<sup>14</sup> ambayo haiwezi kukabiliwa na mikakati ya usalama ambayo haizingattai kipengele cha kisaikolojia kinachohusiana na tabia kama hizo.

### **Uchambuzi wa mazingira ya kazi**

Ni muhimu sana kujua na kuchambua mazingira ya kazi ili kufafanua ni mikakati na miongozo ipi ya usalama inayofaa kutumika. Vile vile, ni muhimu pia kubashiri matukio yanayoweza kutokea siku zijazo, ili kuzuia matendo ya watendaji wanaotumia silaha ambaeo huwaweka watetezi katika hali ya hatari.

Hii inatuleta katika kipengele cha pili: haitoshi kuchambua mazingira tu, kwani kuna haja ya kufanya *uchambuzi wa kubashiri*, kuona jinsi kila uhusishaji unavyofaa katika mazingira na kuchunguza matendo wanayoweza kutenda watendaji kuonyesha hisia zao katika hali hii kabla

13 Beristain (1999; uk. 48-9)

14 Beristain (1999)

ya hili kutokea ("jinsi wengine wanavyotuona") na kabla ya hizi shughuli.

Ni muhimu pia kuzingatia vipimo vyta mazingira. Tunaweza kufanya uchambuzi katika kiwango kikubwa (kuchunguza nchi au kanda), lakini pia inabidi kuchambua jinsi nguvu hizo zinavyofanya kazi katika eneo ambamo sisi tunafanya kazi, hii ni kusema, kujua nguvu ndogo ndogo. Kwa mfano, wanamgambo katika eneo wanaweza kutenda kwa njia tofauti na ile ambayo tunatarajia, kufuatia uchambuzi wa kikanda au kitaifa, na ni muhimu kuwa na ufahamu wa tabia hizi za asili.

Ni muhimu pia kuepuka kuwa na mtazamo wa kudumu wa mazingira, kwa sababu huendelea na kubadilika, na tunapaswa kuifanya mapitio ya mara kwa mara.

### **Ushirikiano katika eneo la kazi: mamlaka, vikosi vyta kuokoa maisha, mfumo wa kijamii**

Sababu ya msingi katika usalama (na kwa ujumla, katika vipengele vyote vyta kazi za kibinadamu) ni ushirikiano wa kutosha (kwa kiwango kikubwa au kidogo) katika eneo la kazi, kuanzisha na kudumisha mawasiliano na mahusiano ya kutosha na mamlaka mbalimbali, vikosi vyta usalama, na mamlaka fanisi, kwa kadri ya miundo ya kijamii iliyopo, iwe katika ngazi ya jamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, makanisa, nk.

### **Ushirikiano wa usalama baina ya mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi nyinginezo**

Ushirikiano halisi wa usalama baina ya mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi nyingine mara nyingi huwa na maendeleo duni, kutokana na ukosefu wa taarifa, kuaminiana au maslahi, tofauti katika madaraka na majukumu, nk

Nafasi za ushirikiano ambazo mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi nyingine wanaweza kuunda, hufanya uwezekano wa angalau hatua mbili za ushirikiano wa vitendo katika suala la usalama:

- a) Kupeana taarifa juu ya mabadiliko katika mazingira ya kazi na katika matukio ya usalama.
- b) Uundaji wa mikakati ya pamoja kwa ajili ya matatizo ya usalama yanayofanuliwa kama vipaumbele.

Kwa kiwango cha chini, angalau hatua (a) inahitajika, ingawa kwa dhahiri matokeo bora hutokea kwa (a)

na (b), lakini ni vigumu kutekeleza na kudumisha hatua hii ya ushirikiano kwa sababu zilizotajwa kabla, na kwa nyingine, ambazo ni zaidi ya kikomo cha urefu wa makala hii kueleza. Hata hivyo, kupeana taarifa na mikakati ya pamoja ni chombo madhubuti kwa kuboresha usalama wa watetezi wa haki za binadamu.

### **Kukabiliana na mikakati: usimamizi wa hatari wa kundi**

Makundi yaliyo katika tishio hutumia mikakati mbalimbali ya kukabiliana ili kupunguza hatari iliyotambulika. Mikakati hii itakuwa tofauti sana kutegemeana na mazingira (vijijini, mijini), aina ya tishio, rasilimali za kijamii, kiuchumi na kisheria zilizopo, n.k Mingi ya mikakati hii inaweza kutekelezwa mara moja na kutimiza malengo ya muda mfupi, hivyo kuwa mbinu zaidi kuliko mikakati iliyoundwa kwa makini. Mingi ya mikakati hii hushughulikia mitizamo binafsi, na wakati mwengine mikakati ya kukabiliana inaweza kusababisha kiwango fulani cha madhara kwa kikundi, hasa iwapo mikakati hiyo haibadiliki.

Mikakati ya kukabiliana inahusiana kwa karibu na aina na ukali wa tishio na uwezo na udhaifu wa kikundi.

Tunaposhughulikia ulinzi, inabidi tuzingatie mikakati ya kukabiliana, kuimarisha ile inayofaa, tukijaribu kudhibiti ile yenye madhara na kuiheshimu iliyobaki (hasa ile inayohusiana na dhana za kitamaduni au imani za kidini).

Kati ya mikakati ya kukabiliana nayo tunaweza kuorodhesha:

- Kuimarisha vikwazo vya ulinzi, vikifichwa vile muhimu.
- Kuepuka tabia ambazo zinaweza kutiliwa shaka na mtendaji mmoja au mwengine anayetumia silaha (hasa ikiwa mamlaka ya kijeshi ya mahali ambapo kundi linaishi ina mgogoro).
- Kutumia sehemu mbalimbali za kujificha nyakati za hatari kubwa (sehemu zenye ugumu kufikika, kama milima au misitu), kuishi katika nyumba tofauti, n.k Wakati mwengine familia nzima hujificha, wakati mwengine watetezi tu hufanya hivyo. Kujificha kunaweza kufanyika wakati wa usiku, au kwa kipindi cha wiki kadhaa.
- Mazungumzo na nchi au serikali au watendaji wanaotumia silaha kisheria.

- Kutoa mashitaka kwa vyombo vya sheria au kwa maoni ya wananchi.
- Kushirikiana (na makundi mengine yaliyo katika hali kama hiyo), kutoa malalamiko ya pamoja, kufanya maandamano, n.k.
- Kuanzisha (au kuendeleza) "maeneo salama".
- Kutafuta ulinzi wa kutumia silaha au wa kisiasa kwa mmoja wa watendaji wa kutumia silaha.
- Kufanya uhamisho wa lazima (kuhamishia makazi mengine au kutoa hifadhi), familia kwa familia au uhamiaji mkubwa. Uhamisho unaweza kuwa uliopangwa au ukimbiasi wa haraka.

Wakati wa kuchambua mikakati ya kukabiliana, tunapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Unyeti: Ikiwa mikakati ya kukabiliana ina uwezo wa kushughulikia haraka mahitaji ya usalama wa kikundi.
- Urekebekaji: iwapo mikakati ya kukabiliana huwezesha mabadiliko ya haraka kwa ajili ya kukabiliana na hali mpya, mara hatari ya mashambulizi inapokwisha (kwa mfano, mtetezi anaweza kuwa na chaguzi kadhaa, kujificha au kuishi kwa muda katika nyumba za watu wengine). Mikakati hii inaweza kuonekana dhaifu au isiyo madhubuti, lakini mara nyingi hudumu kwa muda mrefu.
- Uendelevu: uwezo wa kudumu kwa muda, licha ya vitisho au mashambulizi yasiyoua.
- Ufanisi: uwezo wa kutosha kulinda.
- Ubatilikaji.

### **Kuwalinda wengine**

Kwa madhumuni ya kitabu hiki, ulinzi tutauelewa kama, shughuli ambazo zinaweza kufanywa ili kuchangia usalama wa watu wengine. Ulinzi wa usalama wa pande mbili unakuwa pande mbili za sarafu moja, ili waweze kushirikiana uchambuzi na mikakati. Hata hivyo kwa mtizamo wa kusudio, wanatofautiana katika baadhi ya mbinu na taratibu fulani.

Watetezi, katika kudhibiti usalama wao wenyewe, hufanya shughuli za ulinzi kwa ajili ya wengine: watetezi wengine, wahanga, sekta za kijamii, n.k Kwa njia hiyo hiyo, vyombo vingine (kwa mfano mashirika ya kimataifa yasiyokuwa ya kiserikali) hufanya shughuli za ulinzi kwa ajili ya watetezi.

Mikakati ya ulinzi ni migumu, kwa sababu lazima izingatie mambo ambayo yanaathiri usalama wa wengine (kufuatia, kwa mfano, mfumo wa vitisho-udhaifu-uwezo), pia jinsi wanavyofanya wengine katika kujilinda wenyewe (mikakati yao ya kukabiliana). Ili kukabiliana na utata huu, tumeunda Mfumo wa Uendeshaji kwa Ulinzi wa Ugani, unaotumika kwa watetezi wa haki za binadamu<sup>15</sup>. Mfumo huu lazima uwe wa ufanuzi zaidi kuliko orodha rahisi ya kuzingatia: Ni lazima utafakari mwingiliano na ushirikiano na migongano ya vyombo vya aina zote vinavyofanya kazi katika ulinzi, ili kutathmini matokeo ya aina mbalimbali au shughuli za ulinzi kwa njia ya mpangilio zaidi ambao ndio uliopo sasa.

Mfumo wa Uendeshaji kwa Ulinzi wa Ugani ni chombo kikubwa na rahisi kutumika, kuchanganywa na kudhibitiwa katika hali tofauti za shughuli za ulinzi zinazofanywa na serikali, mashirika ya nchini na mashirika yasiyo ya kiserikali, watu walioathirika na mashirika ya kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyohusishwa. Mfumo huu unaweza kutumika na mtu binafsi kwa chombo chochote kati ya hivyo, wakati ikifanya au kufikiria kufanya shughuli za ulinzi, au kwa makundi ya vyombo hivyo, pamoja na mtazamo wa sekta nzima.

Mfumo wa Uendeshaji kwa Ulinzi wa Ugani una hatua sita:

1. Uchambuzi wa mazingira na matukio;
2. Uchambuzi wa hatari (vitisho, udhaifu, uwezo);
3. Mikakati ya kukabiliana ya kundi athirika;
4. Hatua zilizochukuliwa na taasisi nyngine;
5. Hatua za kuchukua: Mikakati na Mipango;
6. Tathmini ya athari.

Hizi hatua 6 zinaweza kuchukuliwa pamoja na watetezi ambao ulinzi wa usalama wao unapitiwa upya, ili kupata mfumo wa pamoja wa ulinzi, ambao ndio lengo la mwisho la mchakato mzima.

### **Hatua zaidi katika usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu**

Hapa tutaorodhesha mapendekezo kadhaa ya malengo ya kutimiza kwa ajili ya usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu:

- Mafunzo katika usimamizi na mipango ya usalama (kukiwa na watetezi wa haki za binadamu wa aina mbalimbali, inabidi mafunzo haya yarekebishwe kulingana na mazingira na uwezo wa aina mbalimbali).
- Kuingiza suala la usalama katika mipango ya kawaida ya kazi.
- Kutoa nyenzo muhimu kwa ajili ya usimamizi wa usalama wa watetezi: rasilimali watu, fedha, njia za kiufundi, n.k

Ili kufikia malengo haya, tunaweza kuchukua angalau hatua<sup>16</sup> zifuatazo:

Mfumo wa Uendeshaji kwa Ulinzi wa Ugani (au chombo kingine chenye lengo linalofanana) unaweza kutumika kuititia mahitaji ya usalama na ulinzi wa watetezi walio katika vitisho katika mazingira teule.

- Semina au warsha za mafunzo katika usalama na ulinzi: Mafunzo yanaweza kuwa pamoja na uchambuzi wa pamoja (kwa kutumia Mfumo wa Uendeshaji kwa Ulinzi wa Ugani) uliotajwa katika kipengele kilichotangulia, ili hatua zote mbili zichukuliwe kwa mpigo.
- Semina au warsha za kufuatilia na kusaidia mipango ya maendeleo na usalama iliyoundwa baada ya mafunzo (warsha hizo lazima zifanyike katika kipindi cha miezi 6-12 baada ya mafunzo ya awali).
- Kutoa vitabu vya mwongozo wa usalama na ulinzi na nyaraka za kumbukumbu.
- Utafiti zaidi ili kuboresha usalama na ulinzi wa watetezi.

Kitengo cha Utafiti na Mafunzo ya Ofisi ya Ulaya ya PBI kwa sasa kinazifanya kazi mada hizi, na lengo letu ni kupanua kazi hii kwa njia ya ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi nyngine, ambazo zina lengo la pamoja la kushughulikia vizuri mahitaji ya usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu.

15 Kazi hii bado inaendelea na imefikiriwa pia itumiwe na IDP, wafadhili, vyama vya wafanyakazi, nk.

16 Kitengo cha Utafiti na Mafunzo cha Ofisi ya Ulaya ya PBI tayari kinazifanya kazi , pamoja na NGO nyngine kama vile vyama vya kijamii vya kimataifa.

## Bibliografía

ADAMS, J.: *Risk*. Uchapishaji Chuo Kikuu cha London. London, 1995.

AXWORTHY, Lloyd: *Human Security: Safety for people in a changing world*. Idara ya Mambo ya Nje na Biashara ya Kimataifa. Ottawa, Kanada. 1999.

BERISTAIN, Carlos: *Reconstruir el tejido social*. Tahariri Icaria. Barcelona, 1999.

CROUCH, EAC, na WILSON, R.: *Risk/Benefit Analysis*. Ballinger. Cambridge (Mass), 1982.

DWORKEN, Jonathan T.: *Threat Assessment*. Taasisi ya Utafiti wa Umma. Virginia (USA), 1999.

EGUREN, Enrique: “*Beyond security planning: towards a model of security management*”. Jarida la Misaada ya Kibinadamu. Septiembre 2000. Bradford, R.U.

LÓPEZ CEREZO, J., y Luján, J.: *Ciencia y del política riesgo*. Tahariri ya Alianza. Madrid, 2000.

MAHONY, Liam y EGUREN, Enrique: *Unarmed Bodyguards: International Accompaniment for the Protection of Human Rights*. Uchapishaji Kumarian. Connecticut, 1997.

PAUL, Diane: “*Protection in practice: Field-level strategies for protecting civilians from deliberate harm*”. Makala ya 30 ya Mtandao wa RRN. Taasisi ya Maendeleo nje ya nchi, London, 1999.

VAN BRABANT, Koenraad: *Operational Security Management in Violent Environments*. Mapitio ya 8 ya Matendo Mema. ODI. London, 2000.

VAN BRABANT, Koenraad: “*Mainstreaming the Organizational Management of Safety and Security*”. Ripoti ya 9 ya HPG. ODI, London, Marzo 2001.

# Sura ya 3

## Kiwewe na Mikakati ya Kukikabili kwa Watetezi wa Haki za Binadamu

Ukiwa Mtetezi wa Haki za Binadamu, unakabiliana na hatari nyingi katika kazi yako. Wengi wenu mmenyanyaswa, mmeteswa au kutiwa kiwewe - ama moja kwa moja, au kama matokeo ya kushuhudia na kuweka kumbukumbu za hadithi za wengine. Kukabiliana na madhara baada ya matukio yaliyokupata kunaweza kuwa kugumu sana, hasa katika mazingira ya kuhamishwa nchini na kutengwa, ambayo yenyewe hutia kiwewe. Kupata huduma nzuri za afya na ushauri wa kitaalamu wa muda mfupi au muda mrefu kuhusu kiwewe (kulingana na mahitaji yako binafsi) ni muhimu, pamoja na msaada wa kijamii. Katika matukio mengine, inaweza kuwa vigumu kupata tiba sahihi – ama kwa kutokuwa na huduma hapo, au kwa sababu ya hofu ya jumla kwa watu, hakuna matibabu kwa mtu mwenye kiwewe. Hivyo ni muhimu kuunda mtandao wa msaada wa kijamii ambapo unaweza kupata uelewa na utambuzi. Msaada wa kijamii unaweza kuwa mdogo au mkubwa, kulingana na hali ya kipekee ya mtu binafsi. Inaweza kuwa pamoja na watetezi wenza wa haki za binadamu, familia, marafiki, viongozi wa dini, walimu, vyombo vya habari, taasisi, vikundi vya kijamii, na zaidi. Jamii si muhimu kutohaka na msaada binafsi inayotoa tu, bali pia kwa sababu ya mamlaka yake ya kutetea mwingiliano - kushinikiza mamlaka (si serikali pekee, bali pia mamlaka za kidini) kutambua kwamba kitu fulani kimetokea, kuelewa sababu za kutokea kwake na kutoa ufumbuzi na fidia kwa kile kilichotokea.<sup>17</sup>

Ni muhimu mtu kuyapa uzito yaliyomtokeia ili kuyashughulikia na kuyazoea. Uelewa wa jinsi kiwewe kinavyoweza kukuathiri pia ni muhimu; kwani hukusaidia kubuni mikakati inayostahili kukabiliana na maisha yako ya kila siku ili uweze kuendelea kufanya kazi kama binadamu thabiti. Ni muhimu kwa watetezi wa haki za binadamu kutambua kwamba hali wanayokumbana nayo si jambo la kipekee, bali ni matokeo ya mikakati ya mawazo makini ya ukandamizaji, yenye malengo yaliyofafanuliwa wazi wazi. Uelewa huu, uliowekwa katika makundi na kuhusisha tiba sahihi, uzingativu wa huduma binafsi, uhusiano wa kindugu na hisia za msaada toka kwa jamii, yanaweza kukusaidia kukabiliana na kiwewe ulichopata.

Tunatumaini kuwa sehemu hii itakusaidia katika kuendeleza mtindo wa msingi wa msaada ambao wewe, kama Mtetezi wa Haki za Binadamu, unaweza kujenga katika kazi yako, na unaweza kutumika kwa

mahitaji yako na mazingira yaliyopo. Hii inatokana na mtindo wa huduma ilioanzishwa na Kituo cha Kanada kwa ajili ya Wahanga wa Mateso jijini Toronto, Kanada na kazi ya Taasisi ya Cordelia huko Hungary.

### Mateso na Vurugu zilizoandalialiwa

Mateso na vurugu za kupangwa si kitu ambacho “hutoke”. Ni vitendo visivyo na mantiki wala mpangilio, vya uendawazimu vya watu wendawazimu. Ni mikakati madhubuti ilioandalialiwa kwa makini ya udhibiti wa jamii. Mbinu za mateso na vurugu za kupangwa zina historia na hufunzwa. Nchi mbalimbali zina utendaji na utaalamu wao wanaopendelea. Wahalifu binafsi watafanya kwa makusudi uvunjaji sheria kwa watu binafsi. Mtu anaweza kupata mateso na kufanyiwa vurugu za kupangwa kama mtu binafsi, hata hivyo, hadhira kuu ni jamii nzima. Lengo zima ni kumdhuru mtu kimwili, kisaikolojia na kiroho ili kumwogofya, kumvunja moyo na kuidhibiti jamii yake yote. Si jambo la bahati mbaya kwamba viongozi wa jamii mara nyingi huwa walengwa wa kwanza; hali kadhalika si jambo la kustaajabisha kwamba watetezi wa haki za binadamu ndio wateule mahsus. Anapochukuliwa kiongozi imara toka katika jamii, akashikiliwa kwa muda bila ya mawasiliano yoyote na bila mtu yeoyote kujua kinachotokeea na ikiwa hakuna mtu unayeweza kumfuata amwombe msaada, kisha akiwa yu hai na akarudishwa katika jamii akiwa amedhurika, ametiwa hofu na kiwewe, hupeleka ujumbe mzito kwa wanajamii waliobaki ili wasipambane, kuzungumzia, au kudai haki na usawa. Kinaweza kuwa chombo chenye ufanisi mkubwa cha ukandamizaji. Ukweli kwamba watu huendelea kupambana na kuongelea na kushutumu unyanyasaji ni uthibitisho wa ujasiri na azma yao. Lakini mtu hawesi kukana kwamba mara nyingi hupata madhara makubwa.

### Sehemu ya I

#### Mateso, Vurugu Zilizoandalialiwa na Afya

#### Uzoefu wa Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1977 Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso kimebaini athari za mateso na mapambano juu ya afya za watu binafsi, ikiwa ni pamoja na watu wazima na watoto. Kuna athari nyingi za muda mfupi na za muda mrefu

17 Makalailiyoandikwana Maria Teresa Dremetsikasna Michele Millard

za mateso na vurugu za kupangwa:

### **Kimwili**

- maumivu, ya muda mfupi na ya kudumu
- kuvunjika mifupa na maumivu ya viungo
- majeraha
- kuharibika meno na ufizi
- matatizo ya mapafu
- ugumba na utasa
- kukosa nguvu za kiume
- matatizo ya kuchafukwa tumbo
- kudhoofika uwezo wa kusikia
- uharibifu wa viungo vya ndani
- kina mama kupata magonjwa yasiyokuwa ya kawaida
- uharibifu wa misuli
- madhara kwa uti wa mgongo
- kovu katika tishu
- shinikizo kali la damu
- maambukizi ya kibofu cha mkojo na matatizo ya njia ya mkojo
- kukatwa viungo vya mwili
- kupata kiharusi na/au mwili kufa ganzi
- kupoteza uwezo wa kufanya ngono
- maumivu ya kichwa

### **Kisaikolojia**

- majonzi
- majuto, ikiwa ni pamoja na majuto ya mnusurikaji
- ugonjwa wa wasiwasi
- woga uliokithiri
- matatizo ya usingizi, ikiwa ni pamoja na kukosa usingizi na ndoto za kutisha
- kudhoofika kwa uwezo wa kuweka kumbukumbu, kupoteza kumbukumbu
- kujenga hisia za chuki
- matatizo ya uzingativu
- kutojiamini kushika madaraka
- wepesi wa kupandwa na hasira
- kuzukwa na hofu kubwa mara kwa mara
- hisia za kujiua, majoribio ya kujiua
- wasiwasi
- mawazo ya matukio yaliyopita na yanayojiingiza
- matarajio ya kufupishiwa maisha
- kupungukiwa na uwezo wa kuwa na hisia nzito za aina mbalimbali

- kupungukiwa na matarajio ya maisha na uwezekano wake
- matatizo ya ziada kwa watoto, ndugu na marafiki
- kupungua kujamini
- upweke na ubinafsi
- ulegevu
- hofu ya kila kitu
- huzuni na majonzi

Wakati madhara ya mwili hatimaye yanaweza kupona (ingawa wakati mwingine haiwi hivyo), madhara ya kisaikolojia na kiroho yanaweza kuwa tatizo kubwa zaidi kuyashughulikia. Fedheha, udhalilishaji, hofu na kutengwa ni mambo muhimu ya aina hii ya kiwewe, na inaweza kuwa vigumu sana kwa mtu kupata msaada. Hata hivyo, katika kukabiliiana na vita mateso na mapambano na ukiukwaji wa haki za binadamu, haitoshi kulenga mtu mmoja pekee. Watu huishi katika miundo ya kifamilia, kijumuia, kijamii, kisiasa na kiuchumi na kila moja ina athari kwa nyingine. Ubora wa maisha hupimwa kwa mambo mengi na afya ni jambo muhimu. Afya yenyewe ni wazo tata - tunazungumzia afya ya kimwili, kiakili au ya kiroho? Yanahusianaje haya? Je, moja ni muhimu kuliko jingine? Mtu aliyepata kiwewe kwa vyovoyote atahitaji aina fulani ya msaada wa kitabibu na wa kisaikolojia. Lakini yatosha kwenda tu kwa daktari na kufungwa bendeji? Inakuwaje unaporudi nyumbani? Unazungumzaje na majirani na marafiki ambao wanaweza kuwa na hofu na woga wao wenyewe? Inakuwaje ikiwa utarudi katika jamii ukiwa na woga tokana na ghasia na unyanyasaji unaoendelea ambayo yana miiko mikubwa juu ya kuzungumzia juu ya mambo fulani? Je, unaweza kuwa na afya katika mazingira magumu?

Vinavyochangia afya kijamii ni hali ya kiuchumi na ya kijamii ambazo watu huishi nazo, ambazo huchangia katika afya zao. Kumekuwa na mijadala hivi karibuni baina ya mamlaka mbalimbali ugani juu ya kuhusisha rasmi vurugu kama kichangia afya cha kijamii ambavyo kwa sasa hujumuisha:

- kutokuwepo kwa usawa wa kipato
- kuhusishwa na kutohusishwa kijamii
- dhamana ya ajira na kazi
- mazingira ya kufanya kazi
- mchango wa uchumi wa kijamii
- huduma ya utotonu
- elimu
- dhamana ya chakula
- makazi

Ni wazi kuwa kuzungumzia mazingira ya kijamii

na kimwili peke yake haitoshi kwa kushughulikia athari za kiwewe na maelezo ya vurugu inabidi yachukuliwe kama suala tofauti ili kukuza ufahamu wa upana wa madhara yake na njia inayofaa kushughulikia suala hili.

Katika juhudhi za kushughulikia mahitaji ya wanusurikaji wa vurugu wakati wa mapambano na mateso yaliyofanywa dhidi ya watu binafsi, familia na jamii, Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso hutumia dhana ya kiwewe na madhara ya kisaikolojia kama ilivyofafanuliwa na Ignacio Martin-Baro. Martin-Baro alikuwa Kasisi wa Wajesuti wa Kihispania na mwanaasaikolojia aliyefanya kazi El Salvador katika miaka ya 1980. Kazi yake imekuwa ikichapishwa na Chuo Kikuu cha Harvard. Alipofuatwa na wenzake wa Harvard walioata kutafsiri kazi yake, alijibu: "Katika dunia yako, ni kuchapisha au kuangamia. Katika yangu, ni kuchapisha na kuangamia." Na hakika, aliuawa mwaka 1989 na kikosi cha mauaji huko El Salvador katika mauaji ya watu wengi na mtunza nyumba wake, binti yake na makasisi na wasomi wengine kadhaa wakifanya kazi ugani.

Nadharia yake ilielezea jinsi "tabia za kiwewe" zinavyojitezea. Dhana hii inatoa pia utaratibu ambao Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso hutekelezea mtindo wake wa utoaji huduma kwa wanusurikaji wa mateso. Ni mtindo wa jumla ambao huchanganya huduma ili kukidhi mahitaji ya wanusurikaji wa mateso. Inahusisha huduma "katika ofisi ya shirika" na mtandao mkubwa (mpana) wa watu binafsi na mashirika ambayo hutoa huduma kwa wateja wa Kituo cha Kanada kwa Waathirika wa Mateso au huwaunganisha na mitandao mingine ambapo mahitaji yao yanaweza kutimizwa.

Kwa mujibu wa Martin-Baro, kuna vipengele vitatu vyta kiwewe cha kisaikolojia:

1. Wakati mtu hubaki kuwa mhanga mkuu wa vurugu za kupangwa, aina ya kiwewe hutegemea vyanzo vyake kijamii.

Mateso na vurugu za kupangwa kimsingi ni matatizo ya kijamii, na si matendo ya tahadhari ya watu binafsi. Hutokea kama njia ya udhibiti wa kijamii na kwa kuwa idhini imetolewa kwa ngazi nyingi. Mhalifu amepewa idhini na msimamizi wake wa karibu, msimamizi na kamanda wake, na kuendelea hivyo hadi madaraka ya juu zaidi. Jamii inaweza pia kushiriki katika hili kwa njia ya ukimya wao na kukana kutokea kwa matendo haya.

2. Kwa kuwa kiwewe hujengwa kijamii, mhanga binafsi hali kadhalika na sababu za kijamii

zinazochocha zinahitaji tiba na ufumbuzi.

Haitoshi kumfunga mtu bendeji. Ikiwa atapelekwa tena katika mazingira hayo hayo ambayo yanababisha kiwewe kutokea, basi atatiwa kiwewe tena. Iwapo mateso na vurugu za kupangwa ni tatizo la kijamii, basi ufumbuzi wake lazima pia uwe wa kijamii.

3. Kiwewe kitakuwa sugu iwapo mambo yaliyosababisha kutokea kwake hayajashughulikiwa hata kidogo.

Kiwewe cha kisaikolojia ni pamoja na kuelewa kuwa vurugu za kupangwa hujenga mazingira ya "tabia za kiwewe" kushamiri, wakati kukiwa na:

- Mgawanyiko wa kijamii na hakuna usawa;
- Kashfa za taasisi na **maduru ya ukimya** vinagubika ukweli wa kijamii;
- Vurugu za kupangwa na vita vinaleta madhara kwa watu binafsi na familia zao na mitandao binafsi, pia jamii ambazo wao ni wahusika.

Unyimi ndio mfumo mkuu wa ulinzi unaotumiwa na mtu binafsi, familia na jamii nzima. Inafanya kazi kwa njia ifuatayo, kujenga kile Martin-Baro alichokiita maduru ya ukimya:

Katika ngazi ya mtu binafsi mnusurikaji:

- Hudhibiti matukio - hataki kukumbuka.
- Anataka kuwalinda wengine kutokana na tukio hilo lenye uchungu - hataki wengine wapatikane na ubaya wa tukio hili.
- Hategemei kuelewa au kuaminika - wakati mwingine huwa vigumu kuelewa jinsi watu wanavyoweza kufanyiana ukatili, na mara nyingi, hadithi za mateso zinaweza kuwa za ajabu na zisizosadikika. Hii mara nyingi hufanywa makusudi kabisa kwa upande wa wahalifu - kufanya jambo la kutisha mno kiasi kwamba kuliungelea kutachochaea kutoamini. Pia, katika tamaduni nyingine, kuna miiko mikali dhidi ya kuzungumzia uzoefu fulani, hasa yanayohusu ujinsia na ukatili wa kijinsia. Ni kawaida kwa wahanga kulaumiwa kwa kile kilichowatokea na wakati mwingine kufukuzwa nchini au kipelekwa katika mauaji ya heshima.
- Hataki kumpa mtesaji nguvu kwa kuruhusu matokeo ya kiwewe - ni vigumu kukubali kuwa kupata kiwewe kungeweza kusababisha madhara ambayo hayatibiki. Pia ni mfumo wa kujihami unaofanya watu wafuate mtindo wa maisha ya kawaida, lakini kwa kweli kwa kufanya kazi kwa mateso.

Katika ngazi ya familia wanachama wa karibu:

- Hutaka kumlinda mpPENDWA wao - si kumkumbushia mawazo ya uchungu na kuhimiza maendeleo ya maisha ya kawaida.
- Hawazungumzii tukio la kiwewe - inaweza pia kuleta hisia za majuto kwa upande wa familia, kwamba hawakuweza kuzuia hili kutokea.
- Hujitenga na ndugu wengine, marafiki, huduma ya msaada, n.k. - kupoteza imani kwa wengine ni jambo la kawaida. Pia, kiwewe hicho kinaweza kubaki kama imani ndani ya familia na kuva vigumu zaidi kuwfikia wengine (ambao wao wenye we wanaweza kukosa raha kabisa na kuwa na hofu kubwa).
- Hutaka kusonga mbele na kusahau tukio la kiwewe - umuhimu wa kuishi huwakilisha kila kitu.

Katika ngazi ya jamii na taasisi ya watu:

- Huamua kupuuuzia - tena ni vigumu kufikiria kuwa mtu anaishi katika jamii ambayo mambo haya hutokeea.
- Hujisikia kutishiwa na kujaa hofu ya kuingiliana na watu - watu hujishughulisha na maisha na kulinda familia zao wenye we.
- Hujisikia dhaifu kusaidia au kubadilisha hali - matatizo yanaweza kuonekana makubwa mno, pia yasiyowezekana kushughulikia, hofu ni kubwa mno.
- Huwalaumu wahanga - mara nyingi uhamasishaji wa mnusurikaji hulaumiwa. Mnusurikaji anaweza kulaumiwa kwa kushindwa kudumisha dhamana na usalama wa familia.
- Hawataki kuhusika na "masuala ya nje" - mara nyingi ufinyu wa mawazo husababisha matatizo makubwa, hasa iwapo haikutokea moja kwa moja kwa kundi fulani.

### Makundi ya Msaada

Baada ya kuelewa jinsi kiwewe kinavyotokea katika jamii sasa tunaweza kuangalia jinsi ya kukabiliana nacho. Mfumo ule ule ambao Martin-Baro aliutumia kuelezea tabia mbalimbali za kiwewe (Makundi ya ukimya) huweza kutumika kama msingi wa mtazamo madhubuti. Sasa unaitwa Makundi ya Msaada (awali uliitwa Makundi ya Mshikamano).

Kuunda makundi ya msaada katika ngazi tatu tofauti - mtu mmoja mmoja, familia na jamii/taasisi – ukanaji hubadilika kuwa msaada kama ifuatavyo:

Katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, mnusurikaji:

- Hueleweka na kupata msaada - marafiki na familia husikiliza na kuukubali au kuhalalisha uzoefu huo.
- Hujifunza kukabiliana na stadi za "kukinga" athari za kiwewe - kwa mfano, kuepuka sehemu zinazokumbushia kiwewe, kutumia na kuendeleza mtindo wa maisha bora, kudumisha mahusiano na watu wengine.
- Hujenga "umuhimu" kwa uzoefu - "Mimi niliumia kwa sababu nilipigania haki za binadamu za watu wengine. Haya ndio malipo ninayogharamia kwa hiari yangu ", au kuimarisha hali ya kiroho ya mtu (kwa mfano, kazi mojawapo ya dini ni kuelezea mateso).
- Hutambulika vizuri na familia na jamii.

Katika ngazi ya familia:

- Hujenga uelewa - uzoefu wa kiwewe mara nyingi hubadilisha watu. Wanaweza kuwa wakimya, kujitenga zaidi, kupigwa na butwaa kirahisi, hupata usingizi kwa shida na huwa na hasira za haraka zaidi, hukasirika au kuhuzuniwa sana. Familia huelewa chanzo cha tabia hii.
- Hupata stadi za msaada za kukabiliana - kusikiliza, kumpa mtu nafasi na faragha. Kutoa msaada wa uamuzi wa haraka ambao mnusurikaji ataupata.
- Hutambua athari za kiwewe kwa familia - ni vigumu kutambua kwamba mtu anayerudi anaweza asiwe tena kama alivyokuwa kabla. Kutokana na kutoweka, mtoto amempoteza mzazi, mke kampoteza mume, mzazi kampoteza mtoto. Mtu aliyetoweka anaporudi, mambo yanaweza kuwa tofauti sana - mtoto anaweza kujenga hasira kwa "kutelekezwa" na mzazi na majukumu ya kijinsia katika familia yanaweza kubadilika kwa kuwa imebidi mke achukue majukumu ambayo si ya kijadi sana wakati mumewe akiwa hayupo. Muundo wa familia unaweza kuharibika kutokana na hili.
- Hujenga mahusiano na jamii - kutoa huduma zilizopo, ushauri na urekebishaji. Kumwunganisha na mashirika mengine ili kujenga mshikamano na jamii.


Katika ngazi ya jamii na taasisi, jamii:

- Hutoa fursa za haki na utambuzi - kwa michakato ya ukweli na maridhiano, mahakama na tiba.

- Huduma za elimu, afya na jamii zipo na hupatikana - haitoshi kuwa na kliniki ambayo imebobeza katika urekebishaji wa wanusurikaji wa mateso. Kliniki lazima pia ifikike kisiasa, kijiografia na kifedha.
- Hujenga mazingira ya kuanzisha suluhisho la kijamii.
- Huanzisha mazoea ya kumbukumbu ili kuwatambua wahanga na wale waliokufa.

### Aina Anuai za Huduma

Tukipanua makundi ya mshikamano katika makundi mengine zaidi ya msaada, aina mbalimbali za huduma huundwa na mambo mengine mengi ambayo ni muhimu kuzingatiwa huibuka. Mambo haya mapya ni pamoja na:




© Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso, Toronto - Kanada 2005

Kutafsiri aina anuai za huduma katika upeo wa utoaji huduma unganifu na mtindo sahihi wa maendeleo ya jamii, upanuzi zaidi wa makundi unahitajika. Hili ni muhimu katika kuhakikisha uhamaji kutoka kwenye **kundi la uwezeshaji binafsi** ambapo mitazamo binafsi ya uwezo inaendelezwa kuwa kundi la **maendeleo ya kundi dogo**. Misaada yao ya kijamii huleta mabadiliko binafsi ya tabia na kulifanya kundi kuwa **kundi la shirika la kijamii** ambalo huendeleza au huanzisha hatua za ndani kuhusu masuala ya kijamii yaliyofafanuliwa, huendeleza mazungumzo ya kijamii/kitaalam, huibua migogoro kwa ngazi inayotambua. Hii kwa kawaida huimarisha uhusiano na makundi mengine ya jamii, hivyo kuunda kundi linalofuata la **umoja na utetezi**, kushawishi kwa ajili ya sera madhubuti zaidi za afya ya jamii, katika kufikia makubaliano ya kimkakati na yanayofaa kwa ushirikiano na ufumbuzi wa migogoro. Mara nyingi kundi la tano la **utekelezaji wa kisiasa** huhitajika ili kukamilisha mnyororo wa makundi ambayo tena huishia katika hali ya **uwezeshaji binafsi**. Hatua

hizi za kisiasa huunga mkono harakati kubwa zaidi za kijamii, na kujenga mtazamo endelevu wa baadaye, unaopendelewa na demokrasia shirikishi iliyoimarishwa.

Mkakati uliofatiwa na Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso kuhakikisha kuwa michakato ya hapa chini inafanyika ni pamoja na huduma zilizoundwa mahsus kama vile ushauri nasaha wa makazi, Kiingereza kama lugha ya pili (iliyobuniwa kwa ajili ya wanusurikaji waliopata kiwewe), wanajamii waliofanya urafiki na viungo na huduma za kitaalamu kwa ajili ya tiba na/au hati halali za utibabu. Makundi ya misaada ya pamoja (msaada wa wenzi) inayoendelea pia huwaandaa wanusurikaji kujihusisha na mfumo mkubwa zaidi kama ulioelezwa hapo juu. Wakati huduma za Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso zimeundwa kwa ajili ya wanusurikaji wa mateso ambao kwa kawaida huja Kanada kama wakimbizi (hivyo hupata ushauri wa makazi na mafunzo ya lugha), jinsi jamii na uanzishaji wa kisheria wa utibabu yanavyohusishwa katika mchakato wa urekebishaji yana umuhimu maalum kwa watetezi wa haki za binadamu. Mingi ya miundo iliyoonyeshwa hapo juu, inaweza kutumika kwa mafanikio kukidhi mahitaji ya watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi mahali hapo. Msaada wa wenzi unaoendelea umethibitisha kuwa muhimu kwa mchakato wa uponyaji hali kadhalika kama viungo vya kuimarisha uhusiano na jamii kwa ujumla. Hata hali inapoonekana kukatisha tamaa kabisa, haiwezekani kupata marafiki mionganoni mwa watu wa kawaida hali kadhalika wale walio katika nafasi za uwezo au mamlaka ambao wanakuuhurumia. Kuzingatia mahusiano haya na kuweza kutambua wakati wa kutokea ni chombo muhimu katika mchakato wa uponyaji. Elimu kwa umma na ushirikiano wa kimataifa ni njia muhimu ambazo zimefanya Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso kijihusisha na jamii na kuhakikisha kuwepo kwa mahusiano na masuala makubwa zaidi ambayo yanahitaji utekelezaji wa kisiasa. Kujihusisha si tu katika jamii unayoishi, bali kubwa zaidi, la kimataifa pia litaboresha athari na aina mbalimbali za mapambano kwa ajili ya haki za binadamu. Kile ambacho hakiwezi kukamilika pekee na kwa kutengwa kitafanikiwa katika mtandao mzima wa msaada. Huu ni ukweli kwa uponyaji na kwa ajili ya kazi yenye kazi ya haki za binadamu.



© Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Toronto - Kanada 2005

### Unapowasaidia watu waliopata kiwewe kumbuka:

- Uzoefu wa mateso ni jambo la mtu binafsi kama watu wenyele walivyo.
- Unapowasaidia wengine kuzoea hali ya kiwewe, fahamu kuwa huu ni mchakato wa njia mbili – Mtetezi wa Haki za Binadamu humtathmini mnusurikaji na mnusurikaji humtathmini Mtetezi wa Haki za Binadamu.
- Mnusurikaji huyadhibiti maeleo- huheshimu kwamba watu huamua kueleza wazi historia zao kwa muda wanaopenda wao wenyele.
- Kufahamu mukhtadha wa hali unayotathmini - mazingira yako mwenyewe na yale ya mnusurikaji. Ikiwa umepata kiwewe wewe mwenyewe, fahamu kuwa masuala yako yanayohusiana na kiwewe yanaweza kujulisha mahusiano yako na watu wanaajaribu kuwasaidia.
- Kuepuka dhana.
- Kuzuia kujirudia kwa kiwewe
- Kutambua mipaka yako mwenyewe na kufahamu mchakato wa kupata uzoefu wa kiwewe kutokana na mtu mwagine
- Kuweka uwiano katika matatizo na mahitaji ya mnusurikaji na yako mwenyewe.
- Kuchanganya uwezo wa kutambua na maarifa na ujuzi.
- Kukumbuka kuwa wewe ni sehemu ya mtandao wa msaada na huduma katika huduma za aina

mbalimbali. Hauko peke yako au bila nyenzo.


Kwa kuongezea juu ya uzoefu wa moja kwa moja wa kiwewe, watetezi wa haki za binadamu mara nyingi hukutana na tatizo la kiwewe kwa watu wanaowasaidia. Kiwewe cha kiwango kidogo au kutokana na mtu mwagine ni matokeo ya kawaida. Vielelezo hivi viwili hapa chini vinaweza kutumika kama mwongozo wa msingi katika kutambua dalili za kupata kiwewe kuititia kwa mtu mwagine, na kile kinachohitajika ili kukabiliana na madhara<sup>18</sup> yake.

### Kiwewe Kupitia Mtu Mwingine

#### Dalili zilizojitokeza sana

- Kumhurumia sana mnusurikaji
- Humlinda kwa kumpa mahitaji bila kumpa uhuru wa kuchagua
- Matarajio yasyiovezekana
- Kushindwa kuacha kufikiria kiwewe
- Hujiamini kuwa mtu pekee wa kuweza kusaidia
- Kushindwa kusaidia

- Kupoteza uwezo wa kutambua hisia za mtu mwagine
- Kuiweka karibu na mnusurikaji
- Matarajio yenye shaka
- Hataki kufikiria juu ya kiwewe
- Huamini hakuna




© Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso, Toronto -Canada 2005

Kujiepusha na kupata kiwewe kutokana na mtu mwagine na uchovu wa mwili huhitaji uwiano wa:

- Maarifa binafsi
- Mipaka na majukumu yaliyoelezwa waziwazi
- Mfumo wa msaada thabiti binafsi na wa taasisi
- Watu wenye mfadhaiko kutambuliwa na kukubalika.

<sup>18</sup> Sehemu ya II ya makala hii itajadili zaidi juu ya kupata kiwewe kuititia kwa mtu mwagine



### **Kutumia Kanuni za Utendaji za Kituo cha Kanada kwa Wahanga wa Mateso**

- Kuwezeshwa tena – wanusurikaji ni mawakala wa uponaji wao wenyewe.
  - Kufahamu vipimo vya kisiasa, kidini na kitamaduni – uzoefu wa kiwewe ni wazo la kinjozi mno. Hakuna watu wawili watakaopata uzoefu wa kiwewe kwa njia inayofanana. Uponyaji pia unaweza kuwa na utata na kuelezwa na mitazamo mbalimbali, imani na uwezo binafsi wa kukabiliana.
  - Urahisi wa kubadilika kuendana na hali
  - Mbinu ya ujumla - mahitaji ya mnusurikaji ni mengi. Fahamu kwamba si tu suala la matibabu, bali la kisaikolojia na kiroho pia. Ubora wa maisha pia huathiri mchakato wa uponyaji. Unapokidhi mahitaji ya mnusurikaji, ni muhimu kutoa huduma mbalimbali, kitaalamu na pia kijamii. Unaposhughulikia uzoefu wako binafsi wa kiwewe, uwe makini na kuchukua fursa ya huduma na mitandao.
  - Imani, usiri, na heshima ni muhimu sana kwako na watu unaofanya nao/kuwafanya kazi.
  - Mamlaka hubaki kwa mnusurikaji – huhitaji kuwa dhaifu au kudharauliwa kwa sababu ya kiwewe. Wala kwa watu unaowapa msaada hawapaswi kuwa hivyo.
  - Kujali mahojiano na maswali ya tathmini katika kazi yenu kama Watetezi wa Haki za Binadamu kuna umuhimu mkubwa, si tu kwa sababu ya uaminifu, lakini pia kwa sababu ya kurudisha kiwewe (kwako na pia kwa mtu unayemsaidia).
  - Usikilizaji makini - umakini wa kile mtu anachokueleza. Elewa wazi kadri iwezekanavyo.
  - Ukimya wa kibunifu - wakati mwengine ni bora tu kuwa na mtu. Ukimya si lazima umaanishe kutojua kitu.
  - Kufahamu sababu za kiwewe kujirudia.
- Kwa kuhitimisha, sambamba na mfumo wa Martin-Baro, kuna miongozo inayotambulika, inayojulikana sana ambayo mashirika mengi yameigundua:
- Mateso ni suala pana la kijamii, si tu suala la matibabu

- Mateso ndio tatizo, si wanusurikaji wake
- Wanusurikaji wawe mawakala wa uponaji wao wenyewe
- Wanaojitolea (wanajamii) ni vichocheo vya mabadiliko
- Maadili ya msingi ya kiulimwengu (haki za binadamu) ni nguzo imara
- Ushirikiano katika kazi ni muhimu

### **Sehemu ya II**

#### **Kiwewe kupitia mtu mwengine na unyong'onyevu wa mwili**

#### **Uzoefu wa Taasisi ya Cordelia (ilichukuliwa kwa ruhusa ya Dk. Lilla Hardi, Taasisi ya Cordelia, Hungary)**

Watetezi wa Haki za Binadamu mara nyingi hutumikia nafasi mbili kwa wakati mmoja. Wao hufanya kazi na wahanga wenyewe wa ukiukaji wa haki za binadamu - wanaweza kuwa wahanga na wakati huo huo wasaidizi. Hivyo, zaidi ya kiwewe cha moja kwa moja, Watetezi wa Haki za Binadamu hukabiliwa na uzoefu wa kiwewe cha wateja wao. Pamoja na watu wengine wanaofanya kazi katika kazi za mfadhaiko na hatari, Watetezi wa Haki za Binadamu wako katika hatari fulani ya kiwewe kupitia kwa mtu mwengine au cha kiwango kidogo, uchovu wa kujali na unyong'onyevu wa mwili. "Kiwewe husambaa," anaandika Judith Herman, na sababu za kusambaa ni uhusiano wa binadamu. Kiwewe huenezwa kwa njia nyingi kwa mahusiano baina ya watu - ni tata, ni binafsi, hubadilika, na inahusu vizazi mbalimbali.

#### **Kiwewe kupitia mtu mwengine**

Je, kiwewe kupitia mtu mwengine ina maana gani? Ni sawa na Matatizo Baada ya Kiwewe, lakini cha kiwango cha chini zaidi. Inaweza kuwa hivi:

- Huruma – kuwa sehemu ya udhaifu na ukataji tamaa wa mteja
- Upokeaji jukumu la msaidizi kwa uzito mkubwa sana – ulinzi wa mteja wa kupita kiasi - tabia tegemezi ya mteja na kuhoji uwezo wa msaidizi
- Mtazamo wa majuto kwa maisha ya mtu mwennyewe
- Kuangamiza mipaka ya kitaalam
- Msaidizi hujisikia dhaifu

- Hupoteza udhibiti wa hali hiyo, hukwama

Kukabiliwa na ukatili, unyama na ushushaji hadhi wa mahusiano ya binadamu kunaweza kuharibu imani ya mtu katika ubinadamu na kuongeza uchungu kwa Watetezi wa Haki za Binadamu. Kukabiliana na uzoefu wa kiwewe kunaweza kuamsha uzoefu wa kiwewe kwa Mtetezi wa Haki za Binadamu mwenyewe – nani huamua jukumu la msaidizi? Unapofanya kazi katika vikundi ambavyo hupata kiwewe kitokanacho na watu wengine, inawezekana kujenga mtazamo usiobadilishika (“kila mtu ametoka kutaka kunikamata” au “ni wakala wa serikali”), kuunda upya uhai wa mshambulizi/mhanga wa uhalifu na kumsingizia mwanatimu dhaifu. Timu na hata mashirika yamevunjika kwa sababu hii, hasa kama mahali hapana sera au mahusiano ya kushughulikia masuala kwa njia ya kudhibiti athari mbaya.

### Unyong'onyevu wa mwili

Kwa mujibu wa mwanasaikolojia wa New York Herbert J. Freudenberger, Daktari wa Falsafa, ambaye aliunda istilahi hii. Unyong'onyevu wa mwili ni hali ya uchovu au kuchanganyikiwa unaoletwa na kujihusisha kwa dhati katika jambo, mtindo wa maisha, au uhusiano ambaao umeshindwa kufanikisha matunda yaliyotarajiwa. Unyong'onyevu wa mwili ni tatizo lilioundwa kwa nia njema, kwa sababu hutokeaa wakati watu wanapojaribu kufikia malengo yasiyowezekana na kuishia kudhoofisha nguvu zao na kupoteza mawasiliano kwa wao wenyewe na wengine.

Sababu za unyong'onyevu wa mwili:

- Mzigo mkubwa/uliokithiri wa hisia
- Sifa maalum binafsi mahsus (Utu, huruma, uelewa) dhidi ya kuchanganyikiwa
- Mtazamo unaozingatia mteja - “mshtuko wa ukweli”
- Migogoro ya majukumu: wanawake na unyong'onyevu wa mwili - hisia za wasiwasi na hatia dhidi ya “mwanamke mwenye uwezo uliokithiri” au “mama wa nyumbani mwenye uwezo uliokithiri”

Jambo la mzaha kuhusu unyong'onyevu wa mwili ni kwamba inachotokea kwa mtu huyo huyo ambaye awali alikuwa na shauku na kujaa nguvu na mawazo mapya aliposhirikishwa kwanza katika kazi au hali mpya. Mtu wa aina hii kwa ujumla huwa na matarajio makubwa sana ya kile kinachoweza kufanikisha. Wakati muda unapokwenda na

malengo yote kutofanikiwa, shauku hufa na aina ya unyong'onyevu hujijenga. Badala ya kupunguza malengo au kukubali ukweli, huzuia kuchanganyikiwa na mtu binafsi hujaribu zaidi.

Mambo matatu huhusishwa na unyong'onyevu wa mwili:

- *Mgogoro wa majukumu*: mtu ambaye ana majukumu yanayokinanza ataanza kujisikia kuingizwa katika pande nyingi na atajaribu kufanya kila kitu vizuri kwa usawa bila kuweka vipaumbele. Matokeo yatakuwa hisia za uchovu au uchovu unaohusishwa na unyong'onyevu wa mwili
- *Utata wa majukumu*: Mtu binafsi hajui kinachotarajiwa toka kwake. Anajua kuwa anatarajiwa kuwa mfanyakazi mzuri lakini hana uhakika hasa wa jinsi ya kutekeleza hayo kwa sababu hana mtindo au miongozo ya majukumu ya kufuata. Matokeo yake ni kwamba hahisi kuwa amekamilisha chochote cha manufaa hata kidogo.
- *Kuzidiwa na majukumu*: Mtu binafsi hawesi kukataa na huendelea kuchukua majukumu zaidi ya uwezo wake wa kuyashughulikia hadi hatimaye hupata unyong'onyevu wa mwili.

### Dalili

Mwanzo huwa pole pole. Dalili za awali ni pamoja na uchovu kihisia na kimwili; hali ya kutengwa, wasiwasi, kukosa uvumilivu, kutokuwa na shauku na hisia za kutovutiwa kiasi kwamba mtu huanza kuchukia kazi inayohusika na watu ambaao ni sehemu ya kazi hiyo. Katika hali mbaya, mtu ambaye hapo kwanza alijali sana kuhusu programu au kikundi atajihami kufikia kikomo cha kutojali tena hata kidogo.

- Uchovu wa kihisia, kiakili, kimwili
- Hisia za kukosa msaada na kukata tama
- Hisia za kutojua chochote
- Dalili za kimwili: maumivu ya kichwa, udhaifu, kujinyoosha mno, maumivu ya shingo na mabega, maumivu ya tumbo, kuongezeka uzito, kupungua kwa kinga hadi kupata maambukizi, matatizo ya kukosa usingizi
- Dalili za kihisia: huzuni kubwa, kuhisi kukosa msaada, kukata tamaa (“roho yangu ilikufa”).
- Dalili za kiakili: mtazamo hasi, kutoshawishika na umbali katika mahusiano ya binadamu, wasiwasi

badala ya kutambua hisia za wengine.

Kama ilivyo kwa uzoefu wa kiwewe, watu huwa na kawaida ya kuunda mifumo ya ulinzi ili kukabiliana. Baadhi ni madhubuti kuliko wengine. Ulinzi dhaifu ni pamoja na ukataaji na kutoaminiana, kuijweka katika hali ya mtu mwengine: "Serikali ndio adui", kumtambua mhanga au mshambulizi, kugawanyika: wasaidizi/maadui; "ama unakuwa pamoja nasi au dhidi yetu", na kutolipa umuhimu: "Ni mateso kidogo tu ... " Ulinzi imara zaidi ni pamoja na ucheshi na kuelekeza nguvu katika shughuli zinazokubalika kijamii (kujihusisha katika shughuli za uzalishaji au ubunifu).

### **Kuzuia Unyong'onyevu na Uponaji**

- **USIKANE.** Hisi athari katika mwili wako. Kwa hiari, anza kukubali mfadhaiko na shinikizo ambayo yamejionyesha wazi kimwili, kiakili, au kihisia.
- **EPUKA KUTENGWA.** Usifanye kila kitu peke yako! Endeleta au jenga upya uhusiano wa karibu na marafiki na wapendwa wako. Ukaribu si kuwa huleta utambuzi mpya tu, bali pia ni kero kwa fadhaa na majonzi.
- **BADILISHA MAZINGIRA YAKO.** Kama kazi yako, uhusiano wako, hali, au mtu anakushawishi, jaribu kubadilisha mazingira yako, au ikibidi, ondoka.
- **PUNGUZA UZITO WA MAWAZO KATIKA MAISHA YAKO.** Baini yale maeneo au masuala ambayo yanakujia kwa nguvu zaidi mawazoni na ujitalidi kuondoa shinikizo hilo.
- **USIJALI SANA.** Ikiwa mara kwa mara huchukua matatizo na majukumu ya watu wengine, jifunze kujinasua kwa upole. Jaribu kufanikisha mambo yako mwenyewe.
- **JIFUNZE KUSEMA "HAPANA".** Utasaidia kupunguza uzito wa mawazo kwa kuzungumzia mawazo yako kwa uhuru. Hii ina maana ya kukataa maombi au madai ya ziada kwa wakati wako au katika hisia zako.
- **ANZA KUJITO NA KUJIBANDUA.** Jifunze kujituma, si katika kazi tu, bali hata nyumbani na kwa marafiki. Katika hali hii, kutofungamana ina maana ya kujiokoa mwenyewe.
- **TATHMINI UPYA MAADILI YAKO.** Jaribu kuchagua maadili ya maana kutoka yale ya muda na yanayodumu kwa muda mfupi tu, ya muhimu kutoka yasiyo muhimu. Utahifadhi nguvu na muda, na kuanza kujisikia kuzingatia zaidi.
- **JIFUNZE KUTAFUTA NGUVU ZA KUTOSHA.** Jaribu kufikiria maisha kwa wastani. Una nguvu za kutosha. Kuwa na hakika ya kile kinachohitajika katika maisha yako, kisha anza kuweka uwiano wa kazi na upendo, raha na. kuupumzisha mwili wako.
- **TUNZA MWILI WAKO.** Usiruke milo, kujinyima milo muhimu, kupuuzia haja ya kulala, au kuvunja miadi ya daktari. Jitunze kwa lishe.
- **PUNGUZA HOFU NA WASIWASI.** Jaribu kupunguza sana hofu ya kishirikina - haibadilishi kitu chochote. Utapata udhibiti mzuri zaidi katika hali yako iwapo utatumia muda kidogo wa kuhofia na muda zaidi wa kushughulikia mahitaji yako halisi.
- **ENDELEA KUWA MCHESHI.** Anza kujijengea maisha ya furaha. Watu wachache sana huteseka kwa unyong'onyevu wa mwili wakati wakiwa na furaha.

Mateso na kiwewe ni uzoefu wa kubadilisha maisha. Uwezo wa mtu kukabiliana itategemea mambo mengi: mwenendo wa mtu binafsi na uwezo wa kukabiliana, upatikanaji wa mifumo ya msaada wa taasisi na jumuiya na mazingira yanayozunguka yote yana mchango mkubwa sana katika mchakato wa uponyaji. Ni ukweli wa kusikitisha kwamba si kila mmoja ataweza kupona. Wakati mwengine madhara yaliyofanywa ni makubwa mno. Si mazingira yote yanayofaa kwa uponyaji. Ni vigumu sana kuzoea kiwewe kama mtu bado anaishi katika jamii ambamo ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu unaendelea kufanyika. Hata hivyo, utafiti unaonyesha kuwa watu wengi wanaweza kupona vizuri kabisa kama watapata msaada wa lazima, hata katika hali tete na ya hatari. Ni muhimu pia kutambua kwamba uponyaji unaweza kuwa mchakato wa maisha yote. Kutakuwa na nyakati nzuri na kisha nyakati ambazo kumbukumbu zinakuwa karibu kujitokeza. Hata hivyo, kama utatambua kuwa huko peke yako, na kwamba kuna jamii inayojali ambayo iko tayari katika muundo wowote unaona unafaa zaidi – iwe kuitia kwa familia, marafiki, viongozi wa kiroho, wafanyakazi wenza, majirani, Watetezi wengine wa Haki za Binadamu au hata jumuiya ya kimataifa - kisha kazi ya uponyaji na kuzoea kiwewe inaweza kuanza.

# Sura ya 4

## Kampeni za Utetezi wa Haki za Binadamu

Mikakati ya kuendesha kampeni, kushawishi, na kazi ya utetezi vinaweza kutumika kama zana na watetezi wa haki za binadamu katika kazi yao ya kulinda haki za watu wengine. Malengo ya kufanya kampeni ni kuleta mabadiliko chanya, kuwafanya watu watekeleze dhamira zao au kutimiza wajibu na majukumu yao. Pia zinaweza kutumika katika kukuza uelewa wa masuala fulani kwa mapana. Makala hii inataka kutoa maelezo ya jumla ya msingi juu ya namna ya kubuni mikakati ya kampeni inayofaa kwa masuala mbalimbali na asili<sup>19</sup> tofauti za mashirika.

Kufanya kampeni juu ya haki za binadamu ni njia muhimu ya kutafuta ukiukwaji wa haki za binadamu na kuwafidia wale ambao haki zao zimekiukwa. Watu binafsi na jamii wanaweza kuteta haki zao wenye (angalia ukuaji wa hivi karibuni wa uhamashajji wa raia) au wengine wanaweza kufanya kampeni kwa niaba yao, hasa pale ambapo makundi hayana ufahamu wa haki zao wenye au ushawishi wa kudai mabadiliko. Kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi<sup>20</sup> wa Haki za Binadamu, "Kila mmoja ana haki, mtu mmoja mmoja na kwa kushirikiana na wengine, kukuza na kujitahidi kwa ajili ya ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu na uhuru wa msingi katika ngazi za mkoa, taifa na ya kimataifa". Kwa kweli, kila mtu ana haki ya kufanya kampeni kwa ajili ya haki za wengine pia na zao wenye.

### Mipango ya kampeni

Ili kampeni iwe ya mafanikio, lazima malengo yawkwe kutegemea na mabadiliko unayotaka kuleta. Malengo haya ni lazima yawe maalum, yanayopimika, yanayotekelzeza, yenye uhalisia na wakati maalum. Ili kujua malengo yako ni maalum au yanapimika namna gani, lazima kwanza ujiulize kile wewe mwenye we unachotumaini na kutarajia kuwa kitakuwa tofauti baada ya kampeni.

- 19 Makala halisi ya Carol Magambo na kufanyiwa marekebisho na Rachel Nicholson Kiambatanishi cha vyombo vya habari vya Kijamii (Sura ya 4.5) na Neil Blazevic  
20 Jina kamili la Azimio ni: Azimio kuhusu Haki na Majukumu ya Watubinafsi, Makundi na Vyombo Vya Kijamii Kuendelezana Kulinda Kiulimwengu Haki za Binadamu Zinazotambuliwa na Uhuru wa Msingi. Inaweza kupatikana kuititia Ofisi ya Ubalozi wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu: <http://www.ohchr.org/english/law/freedom.htm>

Pili, inabidi ufanyike utafiti ili kupata taarifa kwa ajili ya mkakati wa kampeni yako. Kuelewa kikamilifu masuala yaliyo hatarini ndiko kutakakosaidia uundaji wa mkakati madhubuti. Hii itakusaidia kufanua tatizo unalojaribu kutatua na kufahamu, kwa mfano, nani hukiuka na kwa nini haya hutokea. Unapofanya utafiti ni lazima pia uweze kujibu maswali kama vile ni ujumbe **gani** tunaojaribu kutoa na ni mabadiliko **gani** tunayotaka kuyapata? **Kwa nini** tunataka mabadiliko haya? Tunamlenga **nani** – ni wadau na wabeba jukumu gani walio na ushawishi juu ya suala hili? Tulifanye **namna gani** jambo hili na tutumie njia **ipi**? Je, ni kwa njia ya intaneti, simu, vyombo vya habari, miyadara, mijadala, maandamano, maonyesho au maandalizi ya dua? Juhudi zetu tuzilenge **wapi**? Je, ni katika ngazi ya mahali husika, kitaifa, kikanda au kimataifa? Na mwisho kampeni hiyo itafanya **lini**? Mtu anapofanya utafiti juu ya masuala ya kampeni, inabidi aunde njia bora ya kufikia malengo na kutumia mchanganyiko wa mbinu mbalimbali za kampeni ambazo tutaziangalia baadaye. Majadiliano ya timu ya kampeni juu ya mbinu za kutumia yatathibitika kuwa ya manufaa kwani itabidi faida na hasara zake zipimwe.

Huu ni mfano wa kampeni maalum, inayokwenda hatua kwa hatua kuititia utafiti na mchakato wa mpango:

Wewe ni shirika la kijamii la kiraia nchini Uganda ambaye unataka kuona Muswada wa Sheria ya Mahusiano ya Nchini unapitishwa. Inabidi ujiulize, kwa nini tunahitaji Muswada huu upitishwe?

*Kutoa usawa kwa wanawake na wanaume katika mambo yanayohusiana na ndoa, talaka na mali ya familia.*

Kwa nini mpaka sasa haijapitishwa?

*Kutokana na upinzani toka idara fulani za jamii.*

Watu gani wana ushawishi katika mukhtadha huu?

*Wabunge, Mawaziri na wafanyakazi wa Wizara ya Jinsia.*

Sawa, kwa hiyo tutawashawishije watekeleze?

*Je, hilo linaweza kufanya kwa kutia sahihi maombi, maandamano au mikutano ya hadhara, au utetezi binafsi kwa njia ya barua na mikutano itafaa zaidi?*

Nani mwengine anafanya kazi suala hili – tunaweza kuunda mitandao na mashirika mengine ya vyama

vya kiraia? Wakati gani ni mzuri zaidi kutekeleza hili? Majibu ya maswali haya hutoa misingi ya mkakati wa kampeni yako.

Kufanya kampeni mara nyingi sana inaweza kuelenza kama mazungumzo na jamii, kuwashawishi watu kuwa na shauku isiyo ya kawaida katika kuunga mkono kitendo ambacho hakitawanufaisha moja kwa moja. Kampeni zina lengo la kuhamasisha na kuchochea idadi kubwa ya watu na kama ikitumika vizuri ni chombo kizuri kwa kuleta mabadiliko. Katika kuanza kampeni yoyote inabidi kujenga mwamko, yaani kuanzisha na kufanya ijulikane kuwa tatizo hilo lipo. Pili, kuna haja ya kufanya umma na wale wote wanaohusika kuwa na mwelekeo mmoja na kukubali tatizo ni nini, nani anayeteseka, nani atupiwe lawama na ufumbuzi gani unawezekana. Kisha litolewe ombi au wito kwa umma kwa ujumla, mashirika ya vyama vya kiraia vinavyohusika na wote wale wanaohusika kujiunga na hili huhitaji chombo cha kawaida kinachopatikana au utaratibu kabla ya kitendo hatimaye kuchukuliwa. Katika suala la kampeni dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu, kwanza mtetezi wa haki za binadamu anahitaji kuwawezesha au kuhakikisha kwamba kundi lengwa (watu binafsi au umma kwa jumla) wanajua haki zao, wanakubali kwamba haki zao zimekiukwa na inabidi kufanywa kitu juu ya hilo na la muhimu zaidi **inawezekana**.

Wakati wa kuanza kampeni za kukomesha ukiukaji wa haki za binadamu, mtetezi wa haki za binadamu lazima aijue hadhira na aweze ‘kuwaelewa’. Ili kufanikisha hili, ni muhimu kufanya “uchambuzi wa wadau”. Kuna wale ambao tayari ‘wameshabadilika’ yaani watu ambao wanajua tayari juu ya tatizo hilo na wanataka kuona mabadiliko. Inafaa kufanya uchunguzi ambapo ushirikiano na makundi mengine yanayohusika na mada yako na mitandao mingine unawenza kuundwa. Kisha lipo kundi la wale ambao ni vigumu sana kuwfakishia taarifa unayotaka kuwapa kwa sababu wao hudhani kuwa wanajua kila kitu juu ya madhumuni ya suala hili la haki za binadamu. Wabunge wanawenza kuangukia katika kundi hili. Muda na nguvu zitumike kwa kuelimisha makundi yote haya juu ya ukweli na faida za kampeni hii.

### **Mpango/nyenzo za mawasiliano ya kampeni**

Kuna nyenzo mbalimbali za kufanya kampeni. Ni muhimu kujifunza jinsi ya kutumia zana sahihi kwa ajili ya kazi inayofanyika kwa kutumia taarifa na rasilimali zinazopatikana. Moja ya nyenzo hizo

ni *kuandika barua*: barua hutumwa kwa hadhira maalum kuhusiana na ukiukwaji na kufafanua wazi tatizo hilo na nini kifanyike ili kufikia mabadiliko. Ni rahisi kuziandika, binafsi na hutumia fursa ya urasimu wa serikali (mara inapopokelewa au kutumwa humfikia mwandikiwa moja kwa moja bila kuambiwa njoo kesho) hata hivyo, wana mipaka kama vile gharama kubwa za posta au viwango vya chini vya kujua kusoma na kuandika katika baadhi ya jamii ambazo zinaweza kuwaacha waunga mkono maarufu.

*Kushawishi* huhusisha kutoa maoni na taarifa kwa wafanya maamuzi ili kuwashawishi kwa hatua unayotaka ichukuliwe. Hii mara nyingi ina maana ya kuwasiliana na maafisa ambao kufanya sheria na sera, na kuzungumzia matakwa na maoni, kukabiliana na hoja za wapinzani, na kudhihirisha msaada mkubwa kwa suala hilo.

*Maombi* ni ujumbe rasmi wa maandishi uliotolewa kwa mamlaka kuomba kauli rasmi au hatua, pamoja na orodha ya watiaji saini kwa ombi hilo. Kwa kawaida huwa rahisi na wenyewe gharama nafuu kupanga, huonyesha kiwango cha tatizo la umma na ni njia rahisi ya kufanya watu watoe msaada wao.

*Vyombo* vya *habari* mara nyingi ni muhimu kwa ajili ya kufanya kampeni kwa mafanikio. Moja ya njia za kwanza kufanya vyombo vya habari vijue habari zako ni kuwatumia barua pepe au taarifa waaandishi wa habari kuwaeleza juu ya tukio au utekelezaji, kusema ni nini kitafanyika na wapi. Toa kichwa cha habari cha kuvutia kwa taarifa yako, kionekane na kuunda matukio yanayofaa kuwa habari, wape watu mafunzo ya jinsi ya kuzungumza na vyombo vya habari na uwe na msemaji wa kampeni wa vyombo vya habari ili kuepuka watu mbalimbali kutoa maoni tofauti ambayo yanawenza kukwamisha kampeni. Njia nyingine ya kutumia vyombo vya habari ni kwa njia ya ziara za mazungumzo. Haya kwa mfano ni pamoja na mnusurikaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu au mtetezi wa haki za binadamu kutoa maelezo ya uzoefu na changamoto zake. Kwa kawaida ziara za mazungumzo hulenga hadhira maalum kama vile wanasheria, wabunge au wanavyuo. Kwa kawaida hii huvutia vyombo vya habari, ambayo inamaanisha kuwa ujumbe utaenea kwa hadhira kubwa zaidi. Unapotumia nyenzo hii kwa ajili ya kampeni, inabidi kuzingatia mambo mengi kama vile aina ya hadhira inayolengwa, jinsi ya kupanga maneno ya ujumbe na jinsi vituo mbalimbali vya vyombo vya habari vinavyofanya kazi. Kwa mfano, kuna vituo vya redio ambavyo huwalenga vijana hivyo huifikia hadhira ya vijana. Kutumia vituo hivi ingemaanisha kundi lengwa lako inabidi liwe vijana. Inabidi pia kufanya utafiti njia za kutumia vyombo vya habari

vinavyotosheleza hadhira uliyolenga na kupata maelezo ya mawasiliano ya waandishi wa habari stahiki.

*Matukio ya umma* kama vile maandamano, mikutano ya hadhara na miyahdara ni nyenzo bora sana hasa katika kuhamasisha umma na kuvutia vyombo vya habari, hata hivyo utangazaji mwingu unahitaji kufanyika ili kutoa habari kwa umma na kufanikisha ushiriki wake.

*Msaada wa mtu mashuhuri* ni nyenzo nyingine ya kimkakati wa kufanya kampeni ambapo mtu binafsi maarufu hutumika kusaidia kushawishi maoni ya umma kwa kuwajengea uaminifu ili kuwapa imani na picha ya suala hilo.

Kufanya kampeni katika mtandao kwa kutumia *intaneti* imekuwa mashuhuri katika miaka ya hivi karibuni kama njia ya kupeana habari na ujumbe wa kampeni na hadhira kubwa. Tovuti za maombi kuititia mtandao wa intaneti kama vile Avaz zimekuwa zikitumika kwa athari kubwa kuhamasisha msaada mkubwa kwa kampeni maalum na kuwawezesha waunga mkono kuchukua hatua haraka.

Hata hivyo makala hii haitakamilika bila kuzungumzia vyombo vya habari vya kijamii, moja ya vyombo vya kufanya kampeni kinachoendelea, kipy na cha haraka zaidi kinachopatikana. Angalia kiambatanishi cha vyombo vya habari vya kijamii (Sura ya 4.5) mwishoni mwa sura hii kwa majadiliano ya kina zaidi.

Kwa kuwa vyombo vya habari vya kijamii havikuathiriwa na vikwazo vingi vya vyombo vya habari vya kijadi, vinaweza kufikia hadhira isiyofungwa na eneo la karibu. Vyombo vya habari vya kijamii pia hutoa fursa ya kutoa taarifa ambazo vyombo vya habari vya jadi kwa kawaida huenda havikushughulikia, hasa ikiwa havionekani kufaa kuwa habari katika vituo vya vyombo vya habari. Hutoa nafasi ya kutoa hadithi nzima na fursa kwa mtumiaji kutoa maoni au hata kushiriki katika mazungumzo na watu wengine kwa kutuma maoni. Maelezo ya papo kwa papo ya jinsi vyombo vya habari vya kijamii vinavyoenea, bila kudhibitiwa na muda uliopangwa kuchapisha na nafasi za kutangaza habari, huifanya kuwa moja ya nyenzo bora kwa majadiliano ya mabadiliko ya haraka ya hali. Mfano wa hivi karibuni ambapo chombo hiki kilitumika kwa ufanisi ilikuwa wakati wa kuinua hali ya Afrika ya Kaskazini na Mashariki ya Kati hivi karibuni. Vituo vya video, tovuti za mitandao ya ‘tweets’, na ‘Facebook’ zilifanywa kuufahamisha ulimwengu kinachoendelea katika nchi hizi.

Wakati wa kutumia intaneti au aina fulani za vyombo vya habari vya kijamii, lazima kuzingatia<sup>21</sup> usalama wa mtandao wa intaneti. Vyombo hivi pia vina mipaka, hasa katika suala la upatikanaji. Wafanya kampeni wanahitaji ujuzi na vifaa vya kuunda tovuti na si watu wote hupata huduma ya intaneti. Mafanikio ya tovuti ni vigumu pia kuyafanya tathmini.

Kiutendaji inashauriwa kutumia nyenzo mbalimbali kufanya kampeni za kutolea ujumbe wako: kwa mfano, wakati baadhi wataridhika kutia sahihi maombi, wengine wanaweza kutaka kueleza msimamo wao kwa kushiriki katika maandamano. Hii huhamasisha ushiriki wa watu mbalimbali. Kauli mbiu ya kampeni pia inaweza kuwa wazo zuri kwa sababu kama utaendelea kutumia kauli mbiu hiyo kwa muda, hujulikana na kampeni yako itahusishwa na kauli mbiu hiyo.

Unapotumia nyenzo yoyote ya kampeni kati ya hizo hapo juu, kuutoa ujumbe huo kwa njia sahihi ni muhimu kwa mafanikio. Inabidi uwasilishe ujumbe wako kwa namna ambayo watu wanaweza kuelewa wazi kampeni yako inahusu nini na unataka kufanikiwa nini. Ujumbe unaotarajia kutoa lazima uwe maalum: kwa mfano ‘omesha utoaji kafara wa watoto’ badala ya ujumbe wa ujumla kama ‘haki sasa’, ambayo haielezi unataka haki kwa ajili ya nani au kwa nini. Ujumbe wako na jinsi unavyotolewa lazima vihusiane wazi na madhumuni ya kampeni na hadhira lengwa. Kwa mfano, taarifa ya kina inaweza kuwa njia bora ya kuishawishi serikali kuunga mkono suala fulani lakini inaweza isifae kwa umma kuchukua hatua. Badala yake umma unaweza kushughulikia zaidi upande wa ubinadamu wa suala hilo. Taarifa unayota lazima pia iaminike na iwe ya kutegemewa. Aidha, muda wa mawasiliano yako ni muhimu pia katika kuhusiana na kiasi gani suala lako litakavyopata uzingativu. Kwa mfano kutoa kauli katika vyombo vya habari wakati uuzaaji wa ardhi muhimu unapokuwa katika vichwa vya habari inaweza isiwe wakati sahihi kwa sababu kampeni yako itazidiwa. Wakati wa kufanya kampeni, watetezi wa haki za binadamu lazima daima wakumbuke kuwa mawasiliano ni mchakato wa njia mbili, yaani inahitaji ushiriki hai wa pande zote mbili. Uwe na shauku ya kupokea maoni ya kuthibitisha kwamba ujumbe umepokelewa kama ilivyokusudiwa. Hili ni jambo la lazima kwa mawasiliano yenye ufanisi.

Wakati wa kubuni mkakati wa kampeni, lazima utoe ufumbuzi unaotekelzeza na wenye uhalisia au mapendekezo kwa tatizo unalotaka kushughulikia.

21 Kwa rejea ya kamili kuhusu usalama wa wa mfumo wa tarakimuangalia ‘Usalamakatika Kisanduku’ ya ‘FrontLine’ na ‘Tactical Tech’ katika <http://security.ngoinabox.org/>

Kwa kawaida haya ni mapendekezo ya kile unachofikiri kifanyike ili kufikia mabadiliko na yanaweza kupelekwa kwa wadau mbalimbali. Ni kuanzia hapo, kwamba mamlaka zinaweza kupata mawazo ya jinsi ya kushughulikia hali hiyo na mwelekeo wa kufuata.

Katika maandalizi ya kamjeni lazima daima mtu awe na mpango wa mgogoro au mpango mbadala kwa ajili ya dharura. Kuchangia mawazo kufanyike kuhusu hatari zinazoweza kutokea na jinsi ya kushughulikia hali ya mgogoro. Kwa mfano, mnapofanya maandamano, polisi hutishia kuwakamata kama hamtasimama. Hapa ndipo unapokuja mpango Mbadala kwa sababu kama timu, mngepaswa kutarajia dharura zinazoweza kutokea. Kwa hali hii, je, mtamaliza kamjeni nzima kwa namna hiyo, kuwaita waunga mkono wenye ushawishi kupinga kizuizi au kuitisha mkutano wa waandishi wa habari kutumia kizuizi hicho kwa kuitangaza zaidi kamjeni yako?

Kuingia katika ushirikiano na mashirika mengine ya Watetezi wa haki za binadamu pia hueneza ujumbe wa kamjeni kwa watu wengi zaidi na kuimarisha ufanisi wa kamjeni. Ni vizuri kubaini makundi ambayo yatakuunga mkono, ambayo tayari yanakuunga mkono, na wale unaotumaini wanaweza kukuunga mkono. Kamjeni kubwa ni bora zaidi. Kwa mfano kama una kiongozi wa dini kwa upande wako una nafasi kubwa zaidi kwamba utakuwa umelenga kundi fulani la watu ambaa wanawaamini viongozi wao au watu ambaa wasingelifikiria suala hili kama ‘lisingewafikia’ kutoka kanisani kwa njia ya mahubiri. Pia, wakiukaji wanaweza wasijali sana kama ni kundi la wahamasishaji wa haki za binadamu ‘wakipiga kelele’ lakini itakuwa ni habari tofauti kama kundi la viongozi wa dini na/au wa jadi watajiunga nao. Hii ndio sababu ni muhimu kuhusisha watu wengine ambaa wanaelewa wazo lako na wako tayari kujunga nawe.

### Fungu la rasilimali

Kuendesha kamjeni mara nyingi kunahitaji fedha. Kwa hiyo timu ya kamjeni inahitaji kutathmini fedha na rasilimali watu ya kutosha kufanya kamjeni. Je, una rasilimali gani? Kuna nafasi ya kupata msaada zaidi kutoka mahali pengine? Nani anaweza kusaidia kufanya kazi hiyo kutosha na ukweli kwamba watu wengi huenda wakafanya kamjeni katika muda wao wa mapumziko? Maswali haya na mengine mengi yanapaswa kuulizwa wakati wa kipindi cha mipango ya kamjeni kwani huamua njia na ukubwa wa kamjeni kwa kuwa kamjeni huchukua muda na rasilimali nyingi kuiandaa na kuitekeleza. Pia, ushirikiano unaweza kusaidia kwani

mashirika mengine ya watetezi wa haki za binadamu wanaweza kujiunga kusaidia aidha kifedha au kutoa rasilimali watu na vifaa.

### Tathmini ya matokeo

Wakati kamjeni ikiendelea na baada ya hapo ni muhimu kufanya tathmini ya matokeo yake. Ni muhimu kulinganisha matokeo na malengo yaliyoandaliwa kabla ya kamjeni. Unahitaji kujiuliza: Ni kina nani ambaa tumewafikia? Je, tumewafikia watu sahihi? Je, tumewafanya wachukue hatua? Tulipata matatizo gani? Je, kitu gani tulisahau kuzingatia? Je, kamjeni hiyo imeleta mabadiliko? Hayo ndio mabadiliko tuliyoyataka? Nini kifanyike baada ya hapo? Kutokana na hili, timu ya kamjeni itakuwa imepata picha ya wazi ya kile kilichofanikiwa na mafundisho gani yaliyopatikana yanaweza kutumika kwa ajili ya kamjeni ijayo. Uaminifu na mbinu muhimu kwa kazi ya mtu mwenywewe ni muhimu kwa kupata matokeo ya uhakika.

Kwa muhtasari, kufanya kamjeni ni jambo lenye manufaa kama litaleta mabadiliko ya kweli ya muda mrefu. Wakati mwingine ni vigumu kupima matokeo ya kamjeni lakini hili lisikuzuie. Inatoa fursa kubwa ya kufanikisha mabadiliko yasiyoweza kubadilika kwani huongeza nguvu ya kuungwa mkono na umma na kugeuza msimamo huo kuwa vitendo. Kamjeni zikitumika vizuri, zinaweza kuwa na matokeo mazuri sana katika kupambana na ukiukaji wa haki za binadamu duniani kote na kuwaleta wahalifu kujibu madai.<sup>22</sup>

22 Kwa maelezo zaidi kuhusu kamjeni soma ‘Amnesty Campaigning Manual’ katika <https://www.amnesty.org/en/library/info/ACT10/002/1997> (Arabic: <https://www.amnesty.org/en/library/asset/ACT10/002/1997/en/5d58f141-e8a4-4a23-bc17-224a7e12c756/act100021997ara.pdf>)

# Sura ya 4.5

## Vyombo vya Habari vya Kijamii kwa ajili ya Haki za Binadamu

### Vyombo vya Habari vya Kijamii kwa ajili ya Kampeni

Watetezi wa haki za binadamu lazima wafahamu matumizi ya teknolojia ya vyombo vya habari vya kijamii na kupanga jinsi vitakavyoweza kutumika ili kufikia malengo ya kuendeshea kampeni. Wakati huo huo teknolojia mpya lazima zichunguzwe kwa kina manufaa yake, ili kufanya watetezi wa haki za binadamu kufanya maamuzi sahihi zaidi ya kugawa muda na rasilimali wakati wa utekelezaji wa kampeni za haki za binadamu.

Kampeni nyingi ni za umma kwa jinsi zinavyoendeshwa, hata hivyo iwapo, kwa sababu yoyote ile, kampeni yako inahusika na taarifa binafsi au imelenga tu jamii binafsi, unapaswa kufikiria upya utumiaji wa vyombo vya habari vya kijamii. Vyombo vingi vya habari vya kijamii viko katika miliki ya umma, na baadhi ya mbinu za kupata mawasiliano yako zinaweza kukwepwa kwa urahisi. Tovuti mbalimbali za vyombo vya habari vya kijamii hutumia njia tofauti kufanya mawasiliano binafsi na zinapaswa kueleweka kama zilivyo.

Zaidi ya masuala ya faragha na usalama kuna suala la ufanisi. Ujumbe wa kampeni uliopangwa vizuri ukasambazwa kuititia vyombo vya habari vya kijamii hauwezi kuchukua nafasi ya barua rasmi, mapendekezo ya utaratibu wa haki za binadamu, au mkutano na mdau mbeba jukumu. Baadhi ya malengo ya kampeni hufanikishwa kwa njia za utetezi za kijadi.

### Vyombo vya habari vya kijamii ni vipi?

Vyombo vya habari vya kijamii vilianza kwa njia ya tovuti ambayo watu wangeweza kuwasiliana na marafiki na familia na kufanya nao mawasiliano binafsi. Mitando hii ya kijamii ilipozidi kuwa maarufu nayo pia ikawa mitando kwa ajili ya usambazaji wa mada. Mada fulani ikiwa maarufu hupitishwa katika mtando wa kijamii wote toka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwengine, ikiongeza kwa haraka hadhira ya mada hiyo. Inapotokea hivi, maudhui hiyo husemekana ‘imepata virusi’.

Hii huzua tofauti kati ya vyombo vya habari vya kijadi na vile vya kijamii. Ni masuala ya maamuzi ya tahariri na hadhira. Kwa upande wa vyombo vya habari vya kijadi, vituo vya vyombo vya habari vilivyoanzishwa hufanya maamuzi ya *nini cha kusema*, kwa *mtazamo wa nani, na jinsi ya kuukuza*, yote kwa njia ya udhibiti wa tahariri. Si

kwamba tu vituo vya vyombo vya habari vinaweza kuamua kutoa au kuacha kutoa taarifa ya tukio, wao huchagua ujumbe mzima kwa ujumla na hisia ambazo msomaji ataachwa nazo, na pia kuamua kama ni ‘habari ya ukurasa wa mbele’ au hadithi ya kufukiwa katikati ya gazeti.

Kinyume chake, kwa upande wa vyombo vya habari vya kijamii, maudhui huanzia kutoka vyanzo mbalimbali na kusambazwa kulingana na maamuzi yaliyotolewa na hadhira yake. Kama msomaji katika mtando wa kijamii anafurahia mada fulani anaweza ‘kushirkiana’ au ‘kuyapenda’ maudhui hayo na kutuma kwa anwani zilizo katika mtando wao wenyewe wa kijamii. Kama hawakuvutiwa na maudhui hayo wanaweza kupuuza tu.

Kwa njia hii, katika mitando ya kijamii mikubwa na isiyo na mpangilio, vyombo vya habari husika vinaweza kufikia ‘jamii zinazovutiwa’ kwani watu binafsi husambaza mada tu ambazo huwavutia kwa watu wengine waliovutiwa kama wao. Unaposhirikisha vyombo vya habari vya kijamii kwa madhumuni ya kazi ya haki za binadamu, unapaswa kugundua jamii hizo zinazovutiwa zinazofaa kwa eneo lako mwenyewe la kazi na kujitahidi kuwa mwanachama wa jamii hizo anayejulikana.

### Kutumia Vyombo vya Habari vya Kijamii

Nyenzo za vyombo vya habari vya kijamii daima hubadili, na mitando mbalimbali ikipata na kupunguza umaarufu baada ya muda. MySpace, mmoja wa waanzilishi wakubwa wa vyombo vya habari vya kijamii, alipoteza umaarufu kwa kasi katika mwaka 2005 wakati kampuni iliponunuliwa kwa Dola 580,000,000, na mwaka 2011 ilipouuzwa tena, lakini kwa Dola 35,000,000 tu. Wakati wa kutangaza, tovuti maarufu zaidi za mtando wa kijamii ni pamoja na ‘Facebook’, ‘Twitter’, ‘Youtube’, ‘LinkedIn’, ‘Reddit’, ‘Digg’, na ‘Google +’.

Kumbuka kwamba mitando mbalimbali ni muhimu kwa madhumuni tofauti. ‘Twitter’ imebobe katika ujumbe mfupi sana, kwa kawaida ukijumuisha vyanzo na maneno muhimu. ‘Youtube’ imebobe katika video za mtando wa intaneti wakati tovuti kama ‘Flickr’ au ‘Picassa’ hutoa huduma ya picha. ‘LinkedIn’ ni mtando wa kijamii kwa ajili ya wataalamu wakati ‘Facebook’ unaunganisha aina nyingi za vyombo vya habari kwa ajili ya mawasiliano binafsi na ya kitaalam.

Licha ya tofauti hizi kati ya programu, inabidi baadhi ya mikakati ya pamoja izingatiwe wakati wa kutunga na kutekeleza mkakati wako wa vyombo vyahabari vyakijamii:

**Jitambulisse** - katika ‘uingizaji taarifa’ wa tovuti za duniani kote, ni muhimu kuwakilisha shirika lako na kampeni yako kwa uwazi ili uweze kueleweka haraka na kwa urahisi na mtazamaji. Kuchagua jina ambalo linaleze kazi yako na kuepuka vifupisho virefu. Ambatisha nembo ya shirika au kampeni yako katika akaunti na mawasiliano yako ya mtandao wa intaneti.

**Uwe chanzo cha kuaminika** - tumia programu yako ya vyombo vyahabari vyakijamii kueneza ujumbe wako wa kampeni, maudhui yako ya awali, na pia kueneza tena maudhui husika kutoka vyanzo vingine. Kwa mfululizo wa kupashana maudhui husika juu ya mada ya kampeni yako, unaweza kuwa chanzo cha kuaminika katika jamii ya watu wanaovutiwa na mada hiyo hiyo. Kwa njia hii kampeni yako na chapa ya shirika lako huimarishwa na kuwa mamlaka inayotambulika katika eneo lako la kazi.

**Mtandao na maingiliano** - kushiriki katika vyombo vyahabari vyakijamii katika njia thabiti kutakupa mawasiliano bora zaidi na mashirika na watu binafsi wenyewe mawazo ya kufanana. Unaweza ukajikuta kwamba unaweza kuingiliana na mashirika makubwa au watu wenyewe umaarufu mkubwa na watoa maamuzi kama wanatumia zana hiyo hiyo ya vyombo vyahabari vyakijamii kama wewe. Utakapofanikiwa, fanya mazungumzo ‘ya faragha’ na uzungumzie taarifa muhimu au kujadili ushirikiano kupitia ujumbe binafsi, barua pepe, au kupiga simu. Vyombo vyahabari vyakijamii ni majadiliano ambayo hurudishiwa kile ulichoweka: kadri unavyojihusisha na kushirikiana na wengine ndivyo kadri wengine watakavyochukua hatua na kuwasiliana nawe.

**Kuwa mbunifu** - vyombo vyahabari vyakijamii ni kitu jipya na eneo la ubunifu mkubwa. Uwe mbunifu katika njia ya kutumia vyombo vyahabari vyakijamii kwa ajili ya kazi yako ya haki za binadamu. Fanya kampeni nyingi za siku za kukuza ufahamu wa maudhui mbalimbali yaliyotayarishwa kwa kila siku. Alika hadhira yako kuonyesha hisia zao kwa hadithi binafsi katika ‘video blogs’. Toa tuzo kwa ajili ya maoni ya kazi za sanaa, hadithi, au mashairi. Changia mawazo na shirika lako na pia kuangalia wanachofanya mashirika mengine katika mikakati yao ya vyombo vyahabari vyakijamii.

**Nenda nje ya mtandao** - tambua kuwa si walengwa na wadau wako wote watakaoweza kukufuata katika vyombo vyahabari vyakijamii. Angalia kutumia usambazaji wa ujumbe kupitia programu kama ‘FrontlineSMS’ kueneza ujumbe wako kwa walengwa na wadau kwa njia ya ujumbe wa maandishi. Hamasisha watu kueneza ujumbe wako kwa njia ya mdomo au kuwa mabalozi wa ngazi ya jamii kwa ajili ya kampeni yako. Weka shughuli zako za vyombo vyahabari vyakijamii na maudhui katika mikakati yako ya kijadi ya shirika, na kinyume chake.

# Sura ya 5

## Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu – Haja ya Utekelezaji wa Kimkakati

Jukumu muhimu linalotekeliza na wanawake watetezi wa haki za binadamu limekuwa likizidi kutambuliwa katika miaka ya hivi karibuni. Hata hivyo, changamoto na mahitaji yao maalum hayajaelewaka kabisa na kushughulikiwa kutoka nje au ndani ya harakati za haki za binadamu. Makala hii ina lengo la kutoa maelezo ya jumla ya hali na changamoto za Watetezi wa Haki za Binadamui pamoja na njia zinazofaa kwa ulinzi bora na msaada katika kanda ya Mashariki na Pembe ya Afrika.<sup>23</sup>

### Changamoto

Ufanuzi wa watetezi wanawake wa haki za binadamu hauhusishi wanawake ambaao ni watetezi wa haki za binadamu tu lakini pia hujumuisha wanaume ambaao hutetea haki za wanawake. Kama ilivyoelezwa wakati wa kampeni ya Watetezi wa Haki za Binadamui iliyoinduliwa mwaka 2004,<sup>24</sup> ‘Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu’ ni wanawake wenye juhudini katika ulinzi wa haki za binadamu ambaao ni walengwa kwa *jinsi zao* pamoja na wale wote walio na juhudini katika ulinzi wa haki za wanawake ambaao ni walengwa kwa *kile wanachofanya*.<sup>25</sup> Wanawake watetezi wa haki za binadamu mara nyingi hukabiliwa na changamoto kadhaa kutokana na kuwa watetezi wa haki za binadamu na kuwa wanawake na/au kutetea haki za wanawake. Haya huja katika sura ya ubaguzi unaoendelea kukubalika kisheria, sheria za kimila na kidini. Ukweli kwamba wanawake watetezi wa haki za binadamu wanaendelea kufanya kazi katika jamii iliyoawaliwa kwa kiwango kikubwa na wanaume inayowapangia wanawake sifa kama vile unyenyekevu, kulea na utii, inafanya kuwa vigumu zaidi kwa mtu kutetea haki zake mwenyewe na zile za wengine. Hatua kama hizo kwa haraka huchukuliwa kama tishio kwa utaratibu ulioenea (mfumo dume) na kukataliwa kama mila potofu na utamaduni unaokwenda kinyume na utamaduni. Ukweli kwamba bado ni wanaume hasa wanaounda mitazamo na maadili ya jamii na jamii, hurahisisha utumiaji wa madaraka haya yasiyo na msimamo

kuonyesha jitihada hizi kama hasi na zenyenye madhara kwa jamii, ili kudumisha hali kama ilivyo. Ni muhimu pia kuwafikiria wale wanaume ambaao hujihusisha katika harakati za haki za wanawake na ambaao pia ni walengwa kwa kupinga ‘kanuni za kijinsia’. Haki zinazotetewa na wanawake (na baadhi ya wanaume) kama vile usawa katika ndoa, haki ya ardhi na umiliki wa mali, haki ya huduma ya afya na elimu nk, mara nyingi hazichukuliwi kuhusika au kuwa halali. Kwa hiyo uchukuaji hatua kwa ajili ya wanawake watetezi wa haki za binadamu mara nyingi hukataliwa na kunyimwa idhini, na kusababisha adhabu na vurugu kwa familia, jumuia na jamii nzima kwa ujumla.

### Mifano kutoka kanda ndogo

Kenya:

Mifano inayounga mkono hoja hii ni minge, kama ile ya mtetezi wa haki za binadamu ambaye alitetea dhidi ya Ukeketaji wa Wanawake katika eneo la Wasomali la Kenya. Baada ya binti yake kutahiriwa kwa nguvu na ndugu, alianza kampeni katika eneo la nyumbani kwao dhidi ya matendo haya ya kitamaduni yaliyoenea. Anakumbuka,

*“Nilipokuja na wazo la kuendesha kampeni dhidi ya ukeketaji kwa mara ya kwanza, lilikabiliwa na upinzani mkubwa na uadui wa wazi kutoka kwa jamii yangu. Nilishitakiwa kwa kuanzisha maadili ya Magharibi kuchukua nafasi ya utamaduni wa Kisomali. Baadhi ya viongozi wa dini pia walipinga kampeni yangu, kwa kuwa waliamini tohara ilikuwa ibada ya kidini. Hata hivyo, hii bado ni dhana potofu. Nikawa gumzo la mji, sokoni, maofisi pamoja na misikitini. Nikapewa jina la kudhalilishwa “Kintir”, maana yake “kisimi”. Hii haikunizua kupambana kwa ajili ya haki za wanawake, lakini ilimwathiri binti yangu kijamii na kitaaluma hadi ikabidi ahame kutoka Kenya ya Kaskazini kwenda kusomea Kenya ya Magharibi”.*

Wanawake ambaao hufanya kampeni dhidi ya ukeketaji bado wanakabiliwa na changamoto kubwa katika kazi zao za kila siku. Hata hivyo matokeo ya maendeleo mazuri huko Kenya ni kuperishwa kwa sheria ya hivi karibuni dhidi ya ukeketaji.<sup>26</sup>

23 Makala halisiya Nora Rehmer, na kufanyiwa marekebisho na Lynsey Allan na Carina Raj Maria Jacobs

24 Taarifa na rejea kuhusu kampeni hii na masuala yanayohusiana yanaweza kupatikana katika <http://www.defending-women-defendingrights.org>.

25 International Consultation on Women Human Rights Defenders.ResourceBook.(uk..6)<http://www.defendingwomen-defendingrights.org/pdf/WRHD-Resource-English-press.pdf>

26 Makala ya Habari za Shirika la BBC “FGM: Kenya acts against unkindest cut” tarehe 8 Septemba, 2011. <http://www.guardian.co.uk/society/sarah-boseley-global-health/2011/sep/08/>

Sheria hii mpya inaharamisha kufanya ukeketaji na kupeleka mtu nje ya nchi kufanyiwa ukeketaji. Wajumbe wa Chama cha Wabunge Wanawake wa Kenya walisema ilikuwa siku ya kihistoria:

*“Nimepigania kwa miaka 18 hadi kufanikisha sheria hii. Leo ni siku ya uhuru kwa wanawake. Wanaume walipata uhuru wao mwaka 1963 - lakini leo wanawake wamefanikiwa kupata uhuru wao kutoka kwenye mikono ya kikatili ya jamii”<sup>27</sup> alisema Sophia Abdi Noor.*

Pamoja na kwamba sheria hiyo ni hatua ya kipekee ya kusonga mbele, huchukua zaidi ya sheria pekee kutokomeza kweli vitendo hivyo ambavyo vimejikita mizizi yake katika utamaduni, na Watetezi wa Haki za Binadamui wanaendelea kushiriki katika kampeni<sup>28</sup> hii.

#### *Uganda:*

Chini Uganda, mashirika ya wanawake; Akina Mama wa Afrika, ‘Action Aid International Uganda’, ‘Isis-WICCE’ na ‘Women’s Network Uganda’ walijaribu kufanya igizo lililoitwa “Mazungumzo ya Uke”, ambalo lilihadithia tukio kubwa la ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake ikiwa ni pamoja na ukeketaji, kujamiihana kwa maharimu, na unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo mchezo ambaulikuwa wa mafanikio uliofanyika nchini Kenya, ulipigwa marufuku na Baraza la Habari kwa madai ya kutukuza kile walichoita ngono kinyume cha kawaida, yaani kupiga punyeto, usagaji na ushoga. Utekelezaji wa Baraza ulifikia kuweka kizuizi cha uhuru wa kujieleza na uthibitisho wa nguvu ya mfumo dume ambaao bado umetawala katika vyombo vingi vya kutoa maamuzi. Katika mchakato wa mjadala mkali wa umma, waandaaji walijengewa uadui na kashfa na viongozi wa serikali na watu wengine maarufu katika jamii. Katika tukio la hivi karibuni zaidi, Waziri wa Maadili na Uadilifu “alishauri” hoteli kuu nchini Uganda isitoe ukumbi kwa ajili ya warsha juu ya haki za wafanyabiashara

---

women-africa

- 27 Kama hapo juu. Kwa mujibu wa makala ya habari hizi wakati wa kilele cha Umoja wa Afrika mwezii Juni ambaoulipendekeza kupigwa marufukukwa ukeketaji, Benin, Ivory Coast, Djibouti, Egypt, Eritrea, Ethiopia, Ghana, Guinea, Niger, Nigeria, Kenya, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Senegal, Chad, Tanzania, Togo na Uganda walikuwa na sheria ya kupinga hili tayari. Kuna nchi tisa (zikiwemo zile ambazo ni kinyume cha sheria)ambako hutendeka sana: Djibouti, Egypt, Eritrea, Ethiopia, Guinea, Mali, Sierra Leone, Somalia na Sudan 85% ya wanawake hufanyiwa ukeketaji
- 28 Makala ya Habari za Shirika la IRIN “Kenya: Legislation failing to curb FGM/C” tarehe 2 Juni, 2011. <http://www.irinnews.org/report.aspx?reportid=92869>

ya ngono ambayo ilisababisha waandaaji kulazimika kuhamisha warsha hiyo.

#### *Ethiopia:*

Mwaka 2001, Serikali ya Ethiopia ilisimamisha kwa muda Chama cha Wanasheria Wanawake wa Ethiopia na kuzuia akaunti zake kwa kile ilichoita “kujishughulisha na shughuli tofauti na zile walizoidhinishwa na sheria”<sup>29</sup> Hii ilitokea baada ya chama hiki kuilaamu Wizara ya Haki kwa kushindwa kufuatilia madai ya mhalifu ipasavyo juu ya ukatili majumbani unaoendelea. Chama cha Wanasheria Wanawake wa Ethiopia, moja ya mashirika yasiyo ya kiserikali lililo bora nchini Ethiopia linalofanya kazi ya usawa na haki za kijamii, liliacha mamia ya kesi za ukatili majumbani bila kushughulikiwa wakati wa kipindi cha kusimamishwa. Kitendo hiki cha Serikali kilionyesha ukiukwaji wa wazi wa uhuru wa kujieleza na haki ya kusambaza habari. Hata hivyo, Chama cha Wanasheria Wanawake wa Ethiopia, baadaye kiliweza kufanikiwa kurudishiwa utekelezaji wake kwa maamuzi ya mahakama baada ya Waziri wa Sheria kuhamishiwa wizara tofauti. Mbinu kama hizi huendelea kutumika na serikali ya Mashariki na Pembe ya Afrika. Katika kukabiliana na hali hii, Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa juu ya hali ya watetezi wa haki za binadamu, Margaret Sekaggya, aliandikia suala hili ndani ya taarfa iliyotolewa Desemba 2010 katika maandalizi ya kikao cha 13 cha Baraza la Haki za Binadamu. Mwandishi huyu anaagiza kuwa hakuna nchi inayoruhusiwa kuchukua hatua ya “vitisho, kueleza habari za mtu, kunyang’anya mali, kusimamisha shughuli na kutoshirikisha katika michakato ya kitaifa ya ushauri” kwa misingi ya ubaguzi.

#### **Changamoto za kijinsia**

Changamoto ya dhahiri ambayo huwakabili wanawake watetezi wa haki za binadamu katika kazi zao ni kwamba mara nyingi ujinsia wa mtetezi ni muhimu katika kampeni dhidi ya kazi zao. Mara nyingi wanawake watetezi wa haki za binadamu ni walengwa kwa njia ambayo inalenga katika kuwaum.iza wao kama wanawake<sup>30</sup>, kama vile

- 29 Shirikala ‘Human Rights Watch’ (2001) Ethiopia: Serikali Yavamia Wanasheria Wanawake, tarehe 17 Oktoba, 2001. <http://www.hrw.org/press/2001/10/ethiopia-1017-ltr.htm>
- 30 A/HRC/16/44, Taarifa ya Margaret Sekaggya ya Mwandishi Maalum kuhusu Hali ya Watetezi wa Haki za Binadamu kwa Baraza la Haki za Binadamu, tarehe 20 Desemba, 2010. Inapatikana katika aya ya 87 ukurasa wa 17. Taarifa hii inzungumzia tarifa iliyopelekwa mwa kwa 2005 tokajamhuriya Afrika ya Kati kuhusu jaribio la kumbaka binti wa mwanamke mtetezi, na tishio la kumbaka mwanaharakati wa watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi nchini Kenya.

ukatili wa kijinsia na ubakaji. Watetezi wachache wa haki wanaotetea haki za mashoga na wasagaji wamekabiliwa na mashambulizi na vitisho vya ubakaji “unaotibika” unaoambatana na kazi zao. ‘ushawishi wa kingono’ mara nyingi hutumika “kuwatisha, kuwadhalilisha, kuwafedhehesha, kuwakandamiza au kuwakatisha tamaa wanawake kushughulikia masuala ya ujinsia, ngono au haki nyingine za binadamu.”<sup>31</sup> Hii inaweza kuchukua miundo mbalimbali, mingo ikiwa na lengo la kuafikiana uaminifu na heshima iliyoletwa na watetezi. Nembo kama vile *msagaji, mgeni* na *mpinga utamaduni* hutumika ili kutozithamini na kuziharamisha haki wanazopigania, pamoja na haki yao ya kusema. Miiko inayoendelea ya haki za ujinsia na za kingono hufanya kazi kama kuunga mkono wale wanaojaribu kuwanyamazisha wanawake watetezi wa haki za binadamu.

### **Uhuru wa kutoadhibiwa wahalifu**

Vitendo vya kukiuka haki za Watetezi wa Haki za Binadamu huwalenga mwanamke binafsi wa haki za binadamu pamoja na mashirika ya kutetea haki za wanawake. Wahalifu wa ubaguzi na ukiukwaji wa dhahiri wa haki za watetezi hutofautiana baina ya watendaji wa Serikali<sup>32</sup> na wale wasio wa Serikali wakiwemo wanajamii na familia za watetezi. Kuwawayibisha wakiukaji, huwa kazi ngumu katika mazingira ambayo kwa kawaida ni ya uadui kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu au haki wanazotetea. Ingawa serikali nyingi za kanda ndogo huchangia katika viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, makubaliano yao ni holela na huongozwa na ajenda za kisiasa. Msaada wa “masuala ya wanawake” na baadhi ya serikali mara nyingi hubainika kutopewa uzito na kuwa wa kubahatisha usioshughulikia ipasavyo chanzo halisi cha kuendelea kwa ubaguzi na kukosekana kwa usawa. Hali ya kudharauliwa kwa wanawake inayoendelea katika jamii hudhoofisha uwezo wao wa kuapeleka wakiukaji wa haki zao kwenye vyombo vya kisheria. Hii ni ukweli zaidi kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu waliokwenda kinyume na zile zinazodaiwa kuwa ni kanuni za kawaida kwa kuzungumzia haki na fursa. Mamlaka zinaweza kutumia madaraka yao kwa njia

31 Kama ilivyotajwa awali n. 6 ukurasa wa 8

32 Kama ilivyotajwa awali n.12 katika aya ya 107, ukurasa 20. “TMwandishi Maalum anahofia wingi wa ukiukaji ambaou unaonekana kufanywa na maafisa au wawakilishi Serikali, wakiwemo maafisa wa polisi, jeshi, maafisa wa Serikali na mahakama. Ukiukaji huu, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewareportedly include arrest, mistreatment, torture, criminalize ni pamoja na kukamata, kutendea vibaya, kutesa, kutiwa hatiani, kuwekakizuinikwamakosalakinipia kunya yapaapaa, vitisho, vitisho vya kifo na mauaji.”

mbalimbali kama vile kuzuia usajili wa shirika kwa misingi ya maeneo yao wanayoshughulikia, kesi za muda mrefu na unyanyasaji wa dhahiri toku kwa vyombo vya usalama. Ingawa mfumo wa kimataifa umejengwa juu ya uwajibikaji na wajibu wa mataifa kwa raia zao, hii mara nyingi ni vigumu kutekelezwa. Udhaifu wa jumuiya ya kimataifa katika kutumia shinikizo kwa wakiukaji wa kiserikali mara nyingi hubainika katika kukosa kwake ushawishi katika masuala yanayo julikana kama matatizo ya kitaifa ambayo huundwa kwa kuashiria uhuru wa taifa. Katika taarifa yake, SR Margaret Sekaggya hasa alikubali jukumu la Serikali na matukio ya kutisha yaliyotaja ni nchi gani ambayo wahalifu huonekana kuwalenga wanawake na haki za watetezi wa haki za kundi la wachache.

Aidha, watetezi pia hukabiliwa na ukiukwaji kutoka kwa watendaji wasiokuwa wa kiserikali. Istilahi hii hujumuisha watendaji wa aina mbalimbali kama vile familia na jamii, mashirika binafsi, wafanyakazi wa vyombo vya habari, makundi yenye silaha, mashirika ya waumini wenye imani kali za kidini na taasisi za fedha za kimataifa. Kwa bahati mbaya, mfumo wa sheria wa kimataifa wa sasa bado una masharti duni juu ya uwajibikaji wa watendaji hawa na utekelezaji halisi. Wajibu wa mataifa kulinda raia wake na hivyo wa haki za binadamu mara nyingi hautekelezwi. Hivyo, wahalifu mara nyingi hukosa bila kuadhibiwa. Vikosi vyenye msimamo mkali kisiasa na/au kidini mara nyingi hukiuka haki za raia na kuanzisha utawala wa sheria amba kwa makusudi huweka mipaka ya uhuru wa msingi wa jamii. Wanawake mara nyingi hulengwa kwa misingi ya jinsi zao na nafasi yao kijamii. Hasa katika hali za mgogoro wa kutumia silaha na kujitenga, watendaji wasio wa kiserikali ni mionganoni mwa wahalifu wakuu wa ukiukaji wa haki. Wanawake mara nyingi hushambuliwa na kudhalilishwa, kwa mara nyingine, kwa msingi wa jukumu lao kama watanza maisha na alama ya heshima ya jamii. Wanawake watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi katika hali ya migogoro ya kutumia silaha hukabiliana na ongezeko la changamoto ya kuwa mtetezi na kuwa mwanamke na hivyo ni rahisi wao kudhurika na mashambulizi maalum ya kijinsia. Watetezi huwa wateule wa mashambulizi ili kuonyesha hatari ya kuzungumzia waziwazi na hivyo kuzuia wanajamii wengine wasifuate nyayo zao. Hata hivyo, kama ni ndugu wa karibu au jamii inayokiuka haki za mwanamke mtetezi wa haki za binadamu, uwajibikaji na urekebishaji huwa mgumu zaidi kwa kuhusisha wanaotawaliwa kihisia na kijamii. Madhara ya utetezi wa haki zao za binadamu kwa familia na watoto na mtazamo hasi wa wanandoa, vinaweza kudhoofisha utayari wa wanawake

kuzungumza wazi. Hofu ya kukataliwa na kutengwa na jamii inaweza kushawishi mtetezi asiseme kweli juu ya suala nyeti. Kwa kawaida kuna fursa ndogo ya kimbilio salama zaidi ya nyumbani kwao mtetezi anapokuwa katika tishio. Matendo ya ukatili wa kimwili na kingono ndani ya familia unaosababishwa na kazi ya mwanamke kama mtetezi mara nyingi yatashughulikiwa kama "suala la ndani" na mamlaka ambapo mhalifu atapata adhabu ndogo au kutoadhibiwa kabisa. Ni hizi hali zinazoendelea ndizo zinazopelekea uwajibikaji ulioboreshwu wa watendaji wasiokuwa wa kiserikali na utambuzi wa haki za wanawake watetezi wa haki za binadamu kutetea haki za wengine bado kuwa changamoto kubwa.

### Hatua ndogo za kuleta mabadiliko

Ni njia gani nyingine inayoweza kufanikisha ulinzi bora zaidi kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu? Kwa hakika hakuna jibu rahisi kwa swali hili. Hata hivyo, tokana na ufanuzi wa hapo juu, inakuwa wazi kwamba njia hiyo iwe ya wafuasi wengi, wakishughulikia vyanzo halisi vya ubaguzi unaoendelea ambao husababisha hatari mahususi kwa watetezi wa haki za binadamu. Hii itabidi ikusudie kubadilisha itikadi ya wahalifu na kuunda miundo na taasisi katika jamii ambayo inaweza kutoa ulinzi sawa kwa raia wote bila kujali jinsi. Hili halifanyiki kwa muda mfupi, na makala hii hawesi kudai kutoa ufumbuzi kwa hali ya kutokuwa na usawa inayoendelea katika jamii yetu. Hata hivyo, hujaribu kutoa mawazo ya utekelezaji kwa madhumuni ya kushughulikia madhara maalum yanayoweza kuwapata watetezi wa haki za binadamu katika mtazamo<sup>33</sup> wa muda mrefu. Kampeni ya kimataifa juu ya watetezi wa haki za binadamu iliyotajwa hapo juu ni mfano mzuri wa kujaribu kujenga mabadiliko ya pamoja. Imetokana na jitihada za mitandao kati ya vikundi vya haki za wanawake na mashirika ya haki za binadamu, na hivyo kuleta pamoja utaalamu na hamasa toka misingi mbalimbali. Lengo la kampeni lililotangazwa ni kuunga mkono haki za binadamu duniani kote katika juhudhi zao za kuendeleza haki za wengine. Hata hivyo, kampeni inakusudia kulenga wale watetezi walio hatarini kutohana na jinsi zao na/au utambulisho wa kijinsia. Ili kufanikisha hili, mkazo utawekwa juu ya "kuendeleza mikakati chaniganuzi na ya kisiasa ya pamoja kwa kuimarisha ulinzi wa wanawake watetezi wa haki za binadamu katika muktadha mpana zaidi wa kuthibitisha dhamira

33 Sehemu nyingine za kitabu hutoa ushauri wa jinsi ya kushughulikia matatizo ya usalama ya watu binafsi. Angalia sura "Watetezi wa Haki za Binadamu katika vitisho: Mtazamo wa Ugani kwa Kazi zao" na "Vyombo vya Kimataifa na Kikanda kwa Ulinzi wa Wateteai wa Haki za Binadamu".

zilizotambuliwa kimataifa kwa kanuni za demokrasia na haki za binadamu na uhuru ulimwenguni."Hii ina maana inabidi juhudhi za kitaifa na kimataifa ziendelezwe bega kwa bega kuyapa uzito maeleo ya kitaifa na wakati huo huo kutumia nguvu za harakati za kimataifa katika kuanzisha na kutia msukumo wa mabadiliko. Kiufanisi hii ina maana kwamba watetezi wa haki za binadamu wanahitaji kuijandaa. Katika ngazi ya kitaifa changamoto hii ni kuunganisha pamoja watetezi wa haki za binadamu na kutambua vikwazo wanavyokabiliwa navyo kwa msingi wa kazi yao na jinsi zao. Hii inabidi ifanywe kwa kuzingatia mfumo wa sasa wa kijamii, kisheria, kisiasa na kiutamaduni uliopo ambamo watetezi wa haki za binadamu hufanya kazi na ambao wakati huo huo huathiri ubaguzi wao na uwezekano wao wa kuathirika. Ni kwa uchambuzi wa wazi wa vyanzo halisi vya ubaguzi na ukosefu wa usalama tu ndio unaoweza kuendeleza vyombo muhimu vya mabadiliko. Mikutano ya mashauriano ya kitaifa kama ile iliyofanyika nchini Togo au Nepal<sup>34</sup> inaweza kuwa chaguo moja la kuwaunganisha watetezi wa haki za binadamu kwa ajili ya mipango ya uchambuzi na mkakati. Hata hivyo huwa muhimu kuhusisha harakati kubwa za kitaifa za haki za binadamu katika hatua yoyote ama kama lengo la kampeni au mbia wa mabadiliko. Kujenga kukubalika na kuungwa mkono kwa ujumla kati ya harakati kubwa za watetezi wa haki za binadamu juu ya uhalali wa madai ya watetezi wa haki za binadamu kuwa washirika sawa katika kutetea haki za binadamu liwe moja ya malengo.

Njia zilizochaguliwa kushughulikia suala la vyanzo vya madhara maalum ya watetezi wa haki za binadamu hutegemea sana mazingira ya kitaifa. Hata hivyo, kampeni zilizolenga kushughulikia masuala hayo sambamba na changamoto za jumla za watetezi wa haki za binadamu zinaweza kutoa msaada mkubwa zaidi na matokeo endelevu zaidi. Vyombo na vitendo vilivyoainishwa inabidi vihusiane na kufaa kutumika katika hali ya sasa ya kushughulikia watendaji muhimu – hivyo mashauriano na chama cha kiraia kikubwa na kushirikiana mafunzo yaliyopatikana katika kampeni na utetezi yanaweza kuwa ya manufaa sana katika kuandaa kampeni thabiti yenyeh lengo. Ushiriki wa rasilimali watu na uzoefu katika hatua kama hizo lazima upatikane. Kujenga hali ambapo masuala mahususi ya watetezi wa haki za binadamu yanashughulikiwa na kupata ulinzi kama ilivyoainishwa na serikali katika nyaraka za kimataifa kama vile Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya

34 Masimulizi yake na matukio yanayofanana nayo yanaweza kupatikanakupitia <http://www.defendingwomen-defendin-grights.org/actions.php>

watetezi wa haki za binadamu, watendaji wasiokuwa wa kiserikali na chama cha kiraia inapaswa kuwa lengo la msingi. katika hatua yoyote ya kuchukua.

Kuelezea umuhimu wa kuchukua hatua za pamoja kwa niaba ya ulinzi bora wa watetezi wa haki za binadamu, inahitaji kueleweka kiasi cha ukubwa wa eneo la kujihusisha nalo linaloweza na ambalo ni lazima lifanyiwe kazi. Kutetea mageuzi ya sheria na sera ni eneo moja tu linalohitaji kushughulikiwa kwa juhudhi. Ushawishi kwa ajili ya kupitishwa kwa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu kama chombo cha kitaifa chenye masharti ya kisheria, na kuanzisha mikakati ya kuhakikisha uzingatiaji wake vitasaidia wazo la watetezi wa haki za binadamu kwa ujumla pamoja na watetezi wa haki za binadamu hasa. Wakati huo huo itaweza kuwajibisha watendaji wasio wa kiserikali kwa ukiukaji wa haki za watetezi wa haki za binadamu.

Hata hivyo, marekebisho ya sheria hayawezi kuwa suluhisho pekee. Mabadiliko hayo yanahitaji kwenda sambamba na kulenga mawazo na miundo ambayo husaidia kuendeleza hali iliyopo sasa ya kutokuwa na usawa na fikra za hali ya kuwa mwanamme na ya kuwa mwanamke. Matatizo yanayowakumba watetezi wa haki za binadamu tena na tena toka ndani ya jamii na familia zao kwa misingi ya kazi yao yanahitaji kuchukua hatua za ziada zinazolenga imani zinazoidhinishwa na mila na utamaduni. Kwa hiyo, kwa kufanya kampeni na uhamashajili kwa jamii ni muhimu.

Mbali na kazi ya kushawishi iliyoelizwa hapo juu, watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi mahali hapo wana hatari maalum kabisa zinazowakibili katika kazi zao na uwezo wao wa kutoa mchango kwa usalama wao wenyewe bado haujatumika kikamilifu. Sehemu nydingine za kitabu hiki zinajaribu kuwaunga mkono watetezi wa haki za binadamu kwa kuwapa taarifa juu ya usimamizi wa usalama wao wenyewe na tathmini ya hatari. Sehemu ya rejea katika kitabu hiki pia inatoa vitabu maelezo zaidi ambayo kwa pamoja yatawawezesha watetezi wa haki za binadamu kupata mafundisho kwa ajili ya mahitaji yao maalum ya usalama.

Mashirika kadhaa kwa sasa yanatoa msaada kwa ajili ya ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu. Kati yao shirika la ‘Front Line’ na ‘Urgent Action Fund for Women’ ambayo maelezo yao ya mawasiliano na maelezo mafupi ya fani yao ya kazi yanawenza kupatikana katika kiambatanisho cha kitabu hiki.

## Utambuzi

Uundaji wa programu mbalimbali ili kutambua na kuheshimu kazi ya kishujaa ya watetezi wa haki za binadamu inaweza kutumika kwa manufaa ya kampeni kwa ajili ya kuonekana na kutambuliwa kwa watetezi wa haki za binadamu na changamoto zao maalum. Tuzo<sup>35</sup> za haki za binadamu zilizotolewa kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu zinaweza kutumika kama motisha muhimu katika kazi yao, ambayo haishughulikii wazo lao binafsi tu bali pia hutoa fursa ya kuimarisha kuonekana kwa mafanikio na changamoto za watetezi wa haki za binadamu.

Mfano wa programu kama hiyo ni ‘International Women of Courage Award’(Tuzo ya Kimataifa ya Wanawake Jasiri) iliyotolewa na Mke wa Rais wa Marekani Michelle Obama na Katibu wa Nchi Hillary Clinton mwaka 2010.<sup>36</sup> Tuzo hiyo ilitolewa kwa Mwanasheria wa Kenya, Ann Njogu, Mwenyezekiti wa CRAW, kituo cha sheria kinachotoa msaada wa kisheria na warsha kuhusu haki za wanawake kwa wanawake maskini kutoka maeneo ya vijijini. Miiongoni mwa programu nydingine za haki za binadamu, Ann pia alisaidia kampeni kwa ajili ya katiba mpya na kufanya kazi katika miradi inayohusu ujinsia, urithi wa mjane na mahari. Kama sehemu ya kazi yake, Ann amekabiliwa na matukio mabaya katika kuendeleza haki za wanawake; amekuwa akitishiwa, kukamatwa na kushambuliwa. Licha ya yote haya, Ann bado anaamua kuendelea na kazi yake, akionyesha juhudhi kubwa kwa haki za binadamu.

Kwa ujumla,, ni muhimu kwa watetezi wa haki za binadamu wenyewe kutambua na kukabiliana kwa bidii na changamoto. Hii inaweza kufanya vizuri zaidi kwa kushirikiana na kuunda mikakati inayostahili kukabiliana na ukosefu wa usawa wa msingi katika jamii, jambo ambalo kwa bahati mbaya bado pia linaonekana katika harakati za haki za binadamu. Kupata watetezi wenza kuijunga katika harakati za haki za binadamu, itanufaisha jambo hili, kwa kutumia uwezo wao na kupanua wigo wa ushawishi. Watendaji wa Serikali na wasio wa Serikali kutambua changamoto mahsusizi za watetezi wa haki za binadamu linapaswa liwe jambo la kuzingatia zaidi la utetezi wa haki za binadamu

35 Kwa mfano ‘Ginetta Sagan Fund Award’, ‘Front Line Award’, ‘Martin Ennals Award for Human Rights Defenders’, ‘REEBOK Human Rights Award’ au ‘Robert F. Kennedy Human Rights Award’.

36 ‘Human Rights Watch,’ “Defending Women in Kenya”(Kutetea Wanawakenchini Kenya) tarehe 19 Aprili, 2010. <http://www.hrw.org/en/news/2010/04/19/defending-women-kenya> (ilipatikana tarehe 1/12/11)

kwa mashirika ya kimataifa na watendaji wengine muhimu katika mikutano kama vile Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Mkakati unaoendelezwa kwa pande zote ndio utakaokuwa na matokeo endelevu katika mtazamo wa muda mrefu.

# Sura ya 6

## Kutetea Kundi la Wachache katika Tabia ya Mwenendo wa Kufanya Mapenzi

Suala la wafanya ngono kinyume cha kawaida bado ni nyeti sana katika Afrika. Wanaharakati katika masuala ya watu wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili na wenye jinsi tata hukabiliana na vitisho vikubwa toka kwa serikali mbalimbali pamoja na jamii kwa ujumla kutokana na mambo wanayoendeleza. Hivi sasa, wanaharakati hawa bado wanakosa msaada kutoka katika harakati yenye kubwa ya haki za binadamu, jambo ambalo linavunja moyo mno. Hivyo harakati za wafanyao mapenzi ya jinsi hiyo, hukabiliwa na changamoto nyingi za nje. Hata hivyo, kuna changamoto za miundo ya ndani na za kitiakadi ambazo pia hudhoofisha uwezo wake wa kuendesha masuala yake kwa njia ya kimkakati na kudhibitiwa. Makala hii inajaribu kutoa maelezo ya jumla juu ya masuala ya wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kwa kutoa ufanuzi na kueleza changamoto za wanaharakati wanaofanya kazi katika eneo hili, pamoja na kuunganisha kazi yao kwa juhudini kubwa zaidi za watetezi wa haki za binadamu na haki<sup>37</sup> zao.

### Istilahi

Kifupisho wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kwa pamoja kinamaanisha watu wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili na wa jinsi tata, kifupisho kinachojumuisha tabia mbalimbali za mwenendo wa kufanya mapenzi, yaani na jinsi yako, tofauti au zote na utambulisho wa kijinsia (SOGI). Wafanyao mapenzi kinyume cha desturi huchukuliwa neno lenye maana pana zaidi kuliko "shoga" au "msenge". Lina maana ya uvutiwaji tofauti wa kufanya mapenzi wa watu ambao ni tofauti na kile kinachochukuliwa kama desturi ya kufanya ngono na mtu wa jinsia tofauti, yaani mvuto wa ngono na mtu wa jinsia tofauti. Neno *msagaji* linahusu wanawake ambao huvutiwa kihisia za mapenzi na ngono na wanawake tu wakati *mashoga* inahusu wanaume ambao huvutiwa na wanaume tu. Wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili wanaweza kuvutiwa kihisia za mapenzi na ngono na mwanamume au mwanamke.

Kifupisho wafanyao mapenzi kinyume cha desturi pia ni pamoja na utambulisho wa aina mbalimbali wa kijinsia katika neno 'wenye jinsi mbili'. *Wenye jinsi mbili* inahusu mtu ambaye utambulisho wake kijinsia hauendani na kundi la kiume/kike, kwa

kawaida watu huwekewa wakati wa kuzaliwa. Kwa kweli, maana, matarajio, na wajibu unaoambatana na makundi ya *jinsia* ya "kiume" na "kike" ni hujengwa na jamii. Kwa kulinganisha, neno la kibaiolojia jinsi humaanisha hali ya kisaikolojia ya kuwa na via vyatia vya kiume au kike. Wakati au kabla ya kuzaliwa, watoto hutajwa kama mwanaume au mwanamke kulingana na jinsi familia, wakunga, na/au madaktari wanavyoona sehemu zao za siri. Watu wenye jinsi mbili kisaikolojia, kimwili, kihisia, kingono na/au kiroho ama hujisikia kuwa wa jinsia tofauti kuliko ile walijopewa wakati wa kuzaliwa au hawawezi kupatanisha utambulisho wao wenye na kundi<sup>38</sup> mojawapo la jinsia. *Watu wa jinsi tata* "ambao jinsi zao haziko wazi kwa misingi ya viungo vyatia vya ngono au muundo wa kromosomo (chembe hai inayoonyesha jinsi). Kuna hali nyingi tofauti na maoni yahusuyo na ambayo yamo katika makundi ya istilahi hii. Ni hali ya kibaiolojia."<sup>39</sup>

### Changamoto ya watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi

Watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi hukabiliana na hatari na changamoto mbalimbali katika Afrika. Pamoja na ukweli kwamba mingi ya mitazamo hasi na sheria zinazowabagua watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi ililetwa na wakoloni, unyanyapaa wa kijamii mara nyingi uliohalalishwa na dini na/au utamaduni siku hizi huonyesha matendo ya ushoga na vyama kama "wasio Waafrika" na "kinyume na utaratibu wa kawaida". Ingawa watu wenye jinsi mbili, na mahusiano ya wasagaji na mashoga kuwepo katika aina mbalimbali zinazokubalika katika maeneo mengi kote Mashariki na Pembe ya Afrika kabla ya uvamizi wa nguvu za kigeni, mitazamo hasi na sheria zinazoharamisha zilizoanzishwa kwa njia ya ukoloni ya madhara ya kudumu. Kanuni hizi hutumika sana na kutetewa vikali katika jamii na wananchi wengi, na vyombo vyatia vya habari na/au watu maarufu wakiwalemaza watu kutotumia haki yao ya usawa na kutobaguliwa.

38 Ufanuzi wa baadhi ya istilahi hizi bado zinapingwa kwambahazitoshelezikumaanishaukwelliwanaojaribukueleza. Maana yenye ya watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi pia linawezekitofautiana na istilahi ya hapojuu. Hata hivyo, makala hii haiwezi kujadili kikamilifu masuala haya.

39 Kama ilivyofafanuliwa na 'Swedish Federation for Lesbian, Gay, Bisexual and Transgender Rights'. Inayopatikana katika <http://www.rfsl.se/?p=3307>

37 Makala halisi ya Nora Rehmer, na kufanyiwa marekebisho Lynsey Allan na Carina Raj Maria Jacobs

Changamoto zinazowakibili watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kwa misingi ya tabia zao za mwenendo wa kufanya na utambulisho wa kijinsia mionganoni mwa wengine ni pamoja na:

- Ubaguzi katika kupata ajira, huduma za afya, taarifa na usalama;
- Mateso, kukamatwa kiholela na kudunisha matibabu kama ukiukaji wa haki ya uhuru wa mtu na matibabu ya kibinadamu;
- Mashambulizi yaliyoidhinishwa na Serikali yanayofanywa na wanafamilia, ndugu, "marafiki", waajiri, na wenza gerezani. Wasagaji na wanaume wafanyao mapenzi na watu wa jinsi zote mbili wanakabiliwa na viwango vya juu vya ubakaji na wanaume wa jinsia tofauti. Mashoga mara nyingi hubakwa gerezani na watu wa jinsia tofauti;
- Kunyimwa haki ya haki na tiba;
- Kudai kwa kutumia vitisho vya kufichua tabia ya mtu ya mwenendo wa kufanya mapenzi kwa malipo ya fedha, mali na/au fadhila ya mapenzi, ambayo huongeza, uwezekano wa kupata madhara kihisia, kiuchumi na kimwili
- Kashfa na unyanyaswaji

Katika nchi kadhaa za Mashariki na Pembe ya Afrika, sheria ambazo zinaharamisha mahusiano ya jinsia moja zipo na zinatekelezwa. Watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi hukabiliwa na unyanyaswaji na kifungo ambacho mara nyingi huenda sambamba na udhalilishaji, mateso na kashfa. Mara nyingi kutoadhibiwa huwa ni sheria ya ubaguzi inayotumika kama uhalalishaji wa kuwanymima watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi ulinzi sawa kisheria. Utumiaji vibaya wa madaraka kwa mamlaka kama vile polisi dhidi ya mashoga huidhinishwa kwa kurejea vifungu vya kisheria vinavyokataza matendo ya kibasha pamoja na maoni ya mikutano ya wananchi juu ya matendo yanayodaiwa kuwa ni usherati kama hayo.

Watu hawa hukabiliana pia na ukatili na ukiukaji wa holela wa haki zao kama vile mateso, kubakwa, kifungo, unyanyasaji na kashfa kutokana tu na desturi zao za kufanya mapenzi/utambulisho. Mahitaji ya misingi yanayozingatiwa sana katika Tamko la Ulimwengu kuhusu Haki za Binadamu na katiba za nchi hunyimwa wale wanaodaiwa kuwa mashoga au wenze jinsi mbili. Ukatili dhidi ya wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenze jinsi mbili mara

nyingi hautolewi taarifa, hauwekwi katika nyaraka na hatimaye huishia kutoadhibiwa. [...] Ukimya huu wa fedheha ni ukonaji mkubwa wa kanuni ya haki za binadamu kiulimwengu. [...] Ukitoa watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi, watu binafsi toka ulinzi huu hukiuka wazi sheria ya haki za binadamu pamoja na viwango vya kawaida ya ubinadamu vinavyotufanua sisi wote ", anasema Kamishna wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Louise Arbour.<sup>40</sup>

Matokeo yake, maisha ya mafichoni ni changamoto ambayo wafanya mapenzi kinyume cha desturi wengi inabidi wakabiliane nayo ili kuepuka unyanyasaji na kifungo. Hii moja kwa moja hudhoofisha uwezo wao wa kuendelea na masomo, ajira ya uhakika na upatikanaji wa huduma ya afya. Hii huwafanya wawe katika hatari zaidi kihisia, kijamii na kiuchumi. Tafiti nyingi zimeondoa mashoga kutoka programu za VVU / UKIMWI, ikiwa ni pamoja na uhamasishaji, ushauri nasaha, elimu ya ngono salama, na matibabu. Matokeo yake, kundi hili limebakia katika uwezekano mkubwa wa kuwa hatarini.<sup>41</sup>

Mwaka 2006 gazeti la vichekesho la Uganda, *The Red pepper* lilichapisha orodha ya majina, maeneo ya kazi, na maeneo ya makazi yaliyodaiwa kuwa ya mashoga, kuchocha hofu ndani ya jamii ya wafanya mapenzi kinyume cha desturi na kukiuka wazi haki zao kama watu binafsi kwa faragha. Hivyo uchapishaji huo ukachocha mjadala wa ubishani mkubwa na chuki kubwa kwa mashoga, ulioendeshwa katika magazeti na alijiunga kwa wito wa wanasiwa wenze vyeo vya juu na viongozi wa dini kwa ajili ya mashtaka ya mashoga.<sup>42</sup> Mwaka 2010, gazeti la Uganda la *Rolling Stone* pia lilichapisha orodha ya watu "kuwatangaza" kwa umma na kuhitajika kunyongwa. Watu binafsi kadhaa ambao picha zao zilichapishwa matokeo<sup>43</sup>

40 Utoaji mada wa Ofisi ya Balozi wa Umoja wa Mataifa kwa Haki za Binadamu, Bi.Louise Arbour katika Mkutano wa Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu za watu Wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenze jinsi mbili; Montreal, tarehe 26 Julai, 2006.

41 Kwa mfano: Tume ya Kimataifa ya Haki za Binadamu za Mashoga na Wasagaji (2007) Haifahamiki kabisa. Jinsi Programu ya VVU/UKIMWI inavyowavunja moyo Watu Wanaofanya Mapenzi na watu wa jinsi zao barani Afrika. <http://www.iglhrc.org/files/iglhrc/otm/Off%20The%20Map.pdf>

42 'Human Rights Watch' (2006) "Uganda: 'Press Homophobia' Inaongeza Hofu ya Kuchukuliwa Hatua kali za Kinidhamu. Serikali inaongeza nguvu Kampeni Dhidi ya Jamii ya Mashoga na Wasagaji", September 8, 2006 <http://www.hrw.org/news/2006/09/07/uganda-press-homophobia-raises-fears-crackdown>

43 Makala ya Habariza Shirika la BBC "Mashambulizi yaripotiwa katika gazeti la Uganda 'liliojulikana' kama shoga", tarehe

yake walinyanyaswa. Wanaharakati walichukua gazeti hilo mahakamani na walilipwa fidia kwa kashfa. Ilipofika mwaka 2011, utamaduni wa ‘kuwatangaza’ watu binafsi juu ya tabia za mienendo yao ya kufanya mapenzi ulikuwa umefikia kilele chake kwa kifo cha kutisha. Mwanaharakati maarufu wa Kiganda wa wafanya mapenzi kinyume cha desturi, Kato Daudi, ambaye alikuwa mmoja wa watu walijotajwa katika makala iliyochapishwa na gazeti la *Rolling Stone* aliuawa kikatili Januari 2011.<sup>44</sup>

Kashfa na ushawishi wa watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi inaweza kuchangia zaidi ukosefu wa usalama wao pamoja na kudharauliwa au hata kutengwa na familia zao na jamii kwa ujumla. Hii bado huongeza uwezekano wao wa kuhatarishwa kifedha na kisaikolojia kwa kuondolewa katika ajira na msaada wa kijamii kutoka kwa familia na jamii.

Ukimya wa watetezi wengi wa haki za binadamu kuhusu masuala haya umethibitisha changamoto katika kuendeleza dhana ya kiulimwengu ya haki za binadamu.

Aina hizi za ubaguzi uliofanywa na mamlaka, watunga sheria, watetezi, umma na watu binafsi ni kiashiria dhahiri cha ukosefu wa utambuzi uliopo kwamba haki za wafanya mapenzi kinyume cha desturi ni haki za binadamu.

### **Ulinzi wa Kisheria**

Mwaka 1994 Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa ilitoa uamuzi katika kesi ya *Toonen v. Australia* kwamba sheria ya Serikali ya Australia ya Tasmania inayokataza ufanyaji ngono katи ya wanaume watu wazima walioridhiana kwa siri ilikuwa ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu.

Ilisema kuwa masharti katika kifungu cha 2 (1) cha Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za raia na za Kisiasa 1966 juu ya kutobagua kwa msingi wa “ngono” yajumuushe hisia mbalimbali za mtu binafsi za ufanyaji mapenzi.<sup>45</sup>

22 Oktoba 2010 <http://www.bbc.co.uk/news/world-africa-11608241>

44 Makala ya Habari za Shirika la BBC “Mwanaharakati wa haki za mashoga wa Uganda, David Kato auawa”, tarehe 27 Januari, 2011, <http://www.bbc.co.uk/news/world-africa-12295718>

45 Kwa kurejea kesi ya Toonen dhidi ya Australia, Mawasiliano Na. 488/1992, UN Doc CCPR/C/50/D/488/1992, tarehe 4 Aprili, 1994.

### **Kifungu cha 2 (1) cha Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za raia na Kisiasa:**

*Kila mwakilishi wa Nchi katika Mkataba sasa anaahidi kuheshimu na kuhakikisha kwa watu wote ndani ya mipaka yake, na chini ya mamlaka yake, haki zinazotambuliwa katika Mkataba wa sasa bila ubaguzi wa aina yoyote, kama vile utaifa, rangi, jinsia, dini,,mtazamo wa kisiasa au maoni mengine, asili ya kitaifa au kijamii, mali au hali nyingine.*

Kwa kweli hii ina maana kwamba mtu yeyote asibaguliwe kwa misingi ya tabia yake ya mwenendo wa kufanya mapenzi. Tangu wakati huo, Kamati ya Haki za Binadamu imekuwa ikionyesha wasiwasi mara kwa mara juu ya sheria za kupiga marufuku matendo ya ushoga kuwa ni kueleweka kama kukiuka masharti ya Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za raia na za Kisiasa.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 26 cha Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za raia na za Kisiasa kinatoa ulinzi sawa wa sheria kwa mtu yeyote bila ubaguzi, ambapo huyataka mamlaka kuwalinda watu binafsi wafanyao mapenzi kinyume cha desturi na kwa madhara yoyote, na kuondoa sheria ya kibaguzi inayoruhusu utendewaji tofauti kwa misingi ya mwelekeo wa mtu kimapenzi.

### **Kifungu cha 26 cha Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za raia na Kisiasa:**

*Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanastahili haki sawa ya kulindwa bila ubaguzi wa sheria. Kwa hali hii, Sheria ipige marufuku aina yoyote ya ubaguzi na kuwashakikishia watu wote ulinzi sawa na unaofaa dhidi ya ubaguzi kwa misingi yoyote, kama vile utaifa, rangi, jinsia, lugha, dini, mtazamo wa kisiasa au maoni mengine, asili ya kitaifa au kijamii, mali, uzawa au hadhi nyingine.*

### **Masharti ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu 1986 yanaahidi:**

*Kila mtu atakuwa na haki ya kufaidi haki na uhuru unaotambuliwa na uliokubaliwa katika Mkataba wa sasa bila ubaguzi wa aina yoyote kama vile utaifa, kabila, rangi, jinsia, lugha, dini, mtazamo wa kisiasa au maoni mengine, kitaifa na asili ya kijami, mali, uzawa au hadhi<sup>46</sup> nyingine yoyote.*

46 Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu 1986

Kwa kuzingatia Kifungu cha 60<sup>47</sup> cha Mkataba kinachohamasishwa na masharti ya sheria ya kimataifa ya haki za binadamu, na taratibu zilizopitishwa katika Umoja wa Mataifa, hii ina maana kuwa maamuzi yake yanapaswa kuongozwa na falsafa ya sheria iliyoamuliwa katika vyombo sawa vya haki za binadamu.

Mnamo mwaka 2006, Kanuni<sup>48</sup> za Yogyakarta zilianzishwa, kama mwongozo fafanuza wa matumizi ya sheria ya kimataifa ya haki za binadamu kwa utambulisho wa tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi na wa kijinsia. Inahusu sheria iliyopo ya kimataifa ya haki za binadamu, na inatumika kwa utambulisho wa tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi na wa kijinsia. Kwa mfano, Kanuni ya 6 juu ya haki ya faragha inasomeka:

*Kila mtu, bila kujali tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi na utambulisho wa kijinsia, anastahili kupata faragha bila kuingiliwa kiholela au kinyume cha sheria, ikiwa ni pamoja na kuhusiana na familia zao, nyumbani, au kwa maandishi pamoja na ulinzi kutokana na mashambulizi yasiyo halali kwa heshima na sifa zao. Haki ya faragha kwa kawaida ni pamoja na uamuzi wa kufichua au kutofichua taarifa zinazohusiana na tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi au utambulisho wa kijinsia, pamoja na maamuzi na chaguzi kuhusu mwili wa mtu na maafikiano ya kingono na mahusiano na wengine.<sup>49</sup>*

Tarehe 15 Juni, 2011, Baraza la Haki za Binadamu wakati wa kikao chake cha kumi na saba lilipitisha Azimio<sup>50</sup> juu ya tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi na utambulisho wa kijinsia. Nguvu ya azimio hili ni msisitizo wake wa maazimio ya awali

47 "Tume ichoochee hamasa toka sheria ya kimataifa juu ya Haki za Binadamu na Haki za Watu, hasa kutoka masharti ya vyombo mbalimbali vya Haki za Binadamu na Haki za Watu, Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Shirika la Umoja wa Afrika, Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu, vyombo vingine vilivypitishwa na Umoja wa Mataifa na nchi za Afrika katika suala la Haki za Binadamu na Haki za Watu hali kadhalika masharti mbalimbali yaliyopitishwa katika Mashirika Maalum ya Umoja wa Mataifa ambayo ni wajumbe wa Mkataba wa sasa."

48 Zinapatikana katika <http://www.yogyakartaprinciples.org/>

49 Kanuni ya 6: [http://www.yogyakartaprinciples.org/principles\\_en.htm](http://www.yogyakartaprinciples.org/principles_en.htm)

50 Azimio kuhusu Haki za Binadamu, tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzina Utambulishowa Kijinsia. A/HRC/17/L.p/Rev.1. Mkuu wa Baraza la Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa of the Human Rights Council, kikao cha kumi na saba. Tarehe 15 Jun, 2011. (<http://daccess-dds-ny.un.org/doc/UNDOC/LTD/G11/141/94/PDF/G1114194.pdf?OpenElement>

juu ya kukuza na kulinda haki za binadamu bila ubaguzi, pamoja na kuamua kuitisha mjadala<sup>51</sup> wa jopo juu ya suala hili wakati wa kikao cha 10 cha Baraza la Haki za Binadamu.

### **Uhamasishaji wafanyao mapenzi kinyume cha desturi**

Katika Afrika, kuna mashirika machache ya wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kutokana na mazingira ya ujumla kisheria, kisiasa na kijamii na kiutamaduni yaliyotawala katika nchi nyingi. Kwa kuwa ushoga ni marufuku kisheria katika mataifa mengi ya Mashariki na Pembe ya Afrika, kutetea haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kunaharamishwa moja kwa moja au kwa kificho kwa njia ya sheria na/au mchakato wa usajili kwa mashirika yasiyo ya kiserikali. Hii inazuia kazi ya wanaharakati kwani cheti cha usajili kinahitajika kwa mahitaji mengi ya utawala wa shirika. Miongoni mwake ni ukodishaji wa nafasi ya ofisi, uanzishwaji wa msingi imara na salama wa uendeshaji, ufunguzi wa akaunti ya benki ya kupokea fedha za wafadhili au ununuzi wa vifaa. Sifa zinazohitajika kuendesha shirika hazipo mara zote, na bado upatikanaji wa mafunzo ni mdogo sana kwa ubaguzi mkubwa wa hisia zao za jinsi ya kufanya kimapenzi na/au utambulisho wa jinsia ambaa uliupa utetezi wao umuhimu tangu mwanzo.

Mgawanyiko na migogoro ya ndani miongoni mwa wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi katika kuyapa kipaumbele masuala na mbinu za kutumia kwa ajili ya kuendeleza haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi hudhoofisha ufanisi<sup>52</sup> wao. Kwa hiyo ni muhimu kwa wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kuungwa mkono katika kutatua migogoro na kupanga mikakati ili waweze kukusanya juhudhi na nguvu katika kushughulikia changamoto za sasa zinazowakabili wafanyao mapenzi kinyume cha desturi. Changamoto zaidi zinaundwa kutoka ndani ya harakati hii kwa njia ya kutoaminiana, usaliti, na matumizi mabaya ya mamlaka yanayosababishwa na kudharauliwa kulikokithiri kijamii na kiuchumi, ukosefu wa fursa zinazowasukuma wengi kuweka

51 Kama hapo juu aya ya 2 "Aamua kuitisha majadiliano ya jopo wakati wa kikao cha 19 cha Baraza la Haki za Binadamu, kilichopewa maelezo yaliyomo katika utafiti ulioagizwa na Baloo na kuwa na mazungumzo yenye manufaa, yanayok-wenda na wakati na ya uwazi kuhusu suala la sheria za kibaguzi na uitendo vya kikatili dhidi ya watu binafsi kutokana na tabia zao za mienendo ya kufanya mapenzi na utambulisho wao wa kijinsia."

52 Mfuko wa 'Urgent Action Fund' kwa ajili ya Wanawake' (2005) Watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi wajiaandaa katika Afrika Mashariki: Jaribio la kweli kwa Watetezi wa Haki za Binadamu. <http://www.urgentactionfund.org/documents/UAF-LGBTI%20REPORT%20FINAL.pdf>

maisha yao binafsi mbele ya mapambano makubwa pamoja na athari mbaya za usimamizi wa mfadhibili. Mfadhibili mara nyingi huja katika namna ya utafiti usiotosheleza ambapo fedha hutolewa, tathmini isiyojitosheleza ya kumbukumbu za ufuatilaji wa uwezo wa usimamizi wa watu binafsi, pamoja na matarajio yasiyo na uhalisia katika suala la matokeo na nyaraka kuhusu uwezo wa mashirika. Masuala haya yanaweza kushughulikiwa kwa njia ya mazungumzo makali na wadau wote wanaohusika, ili kuimarisha uwezo wa harakati za kukabiliana na changamoto zake kubwa za nje.

Ukosefu wa msaada kutoka kwa mashirika ya kawaida ya haki za binadamu unaweza kuelezewa na mfumo wa kisheria wa kikatili na maoni ya umma yaliyopo juu ya uharamu wa ushoga. Watetezi wa haki za binadamu wengi wa kawaida huhofiauzuiliwaji na serikali wakati wa kutetea haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi. Aidha, mara nyingi haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi hayachukuliwi kuwa halali na stahiki, mara nyingi bila ya kujua. Huu ni ukiukaji wa wazi wa haki za binadamu wa kila mahali, kwamba watetezi wa haki za binadamu inabidi wakabiliane kama wanataka kutambuliwa hivyo (tazama Utangulizi wa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watetezi wa haki za binadamu). Kwa sababu hiyo, jukumu moja kuu la wanaharakati ni kuhamasisha watetezi wenzao wa haki za binadamu katika suala lao. Kimsingi, hii ni lazima ifanyike kwa kutumia njia ya haki za msingi, ambayo inasisisitiza maadili ya msingi wa usawa na kutobagua iliyopo katika viwango vya msingi vya kimataifa kama vile Azimio la Haki za Binadamu na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu. Kupata msaada kutoka harakati za haki za binadamu ni muhimu katika kuimarisha sauti ya wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi na kuonyesha uaminifu zaidi kwa suala lake katika kuzungumza na watunga sheria na wananchi wengi.

Ili kufanikisha mabadiliko, wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi inabidi washughulikie vikwazo vilivyotajwa hapo juu kwa njia ya kimkakati. Hivi karibuni wamepata msaada mkubwa toka harakati za haki za binadamu katika utetezi wao na kampeni za kurekebisha sheria na matendo ya kibaguzi; hata hivyo bado kuna mengi ya kufanya.

Licha ya kujenga ushirikiano imara na vyama vya kiraia, wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi wanapaswa kutumia njia rasmi zilizopo na vyombo vya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa au Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa

Mabaraza<sup>53</sup> ya Mikataba na Taratibu<sup>54</sup> Maalum, una uwezo wa “kufuutilia utekelezaji wa Serikali na sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na kutoa mapendekezo ipasavyo. Uchambuzi na hitimisho la Taratibu Maalum na Mabaraza ya Mikataba kwa upande wake inaweza ikaleta mabadiliko katika sheria ya nchi na utendaji kadri mataifa yanavyojitahidi kuleta sheria na sera zao na kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. [...] Uwasilishaji wa kesi za watu binafsi na maelezo ambayo huonyesha miundo ya ukiukaji wa haki muhimu kwa wafanyao mapenzi kinyume cha desturi unaweza pia kusababisha Taratibu Maalum na Mabaraza ya Mikataba kulipa uzito eneo hili la ulinzi wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na njia ya maendeleo ya falsafa ya sheria.”<sup>55</sup> Kuwa na uwezo wa kuchukua hatua na kuishinikiza Serikali, Taratibu Maalum na Mabaraza ya Mikataba inahitaji taarifa za kuaminika na malengo adilifu yatakayozingatiwa na mapendekezo yao. Hii inaweza kutolewa na mashirika ya kimataifa, kikanda au ya kitaifa kwa kufuata taratibu thabit. Shirika la ‘Amnesty International’ limetengeneza waraka wenye kichwa, “Haki za Binadamu za Wasagaji, Mabasha, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili: waraka wa kwanza kufanya kazi na Mabaraza ya Ufuatilaji wa Mikataba ya Umoja wa Mataifa na Taratibu Maalum za Tume ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki<sup>56</sup> za Binadamu”

- 53 Vyombo vya mikataba ni kamati za wataalamu zilizoanzishwa ili kufuutilia uzingatiasi wa wawakilishi wa nchi kwa masharti ya mikataba kama vile Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Haki za Kisiasa, Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni), Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Mateso na Ukatili mwagine, Matendo ya Kinyama au Kudhalilisha au Adhabu, Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Ufutaji wa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake, Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Ufutaji wa Aina zote za Ubaguzi wa Asili ya Kijamii, Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto na Mkataba kuhusu Ul-inzi wa Haki za Wafanyakazi Wahamiaji Wote na Wanafamilia.
- 54 Taratibu Maalum ni wataalamu muhimu na wa nchi waliteulewa na Tume ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu (sasa Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu) wakiangalia ukiukaji maalum au ukiukaji unoatokea katika nchimbali. Wanaweza kuitwa “Mwandishi Maalum”, “mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu”, “imtaalamu wa kujitegemea”, au kuundwa kama “kikundi cha kazi”.
- 55 Shirika la ‘Amnesty International’ (2005) Haki za Binadamu za Wasagaji, Mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili: Haki za Binadamu za Wasagaji, Mabasha, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili: waraka wa kwanza kufanya kazi na Mabaraza ya Ufuatilaji wa Mikataba ya Umoja wa Mataifa na Taratibu Maalum za Tume ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu. Al Index: IOR 40/004/2005, p. 1. <http://web.amnesty.org/library/Index/ENGIOR400042005?open&of=ENG-347>
- 56 Kama hapo juu

ukielezea uwezekano na taratibu za wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi katika kutumia njia hizi katika utetezi wa kazi zao.

Tume ya Afrika ya Binadamu na Haki za Watu ina taratibu sawa za kutosha. Kifungu cha 55 kinaruhusu utoaji wa malalamiko juu ya ukiukwaji wa masharti kama yalivyoainishwa katika Mkataba wa Afrika na mwakilishi wa nchi (inajulikana kama Mawasiliano) kwa Tume hiyo na mtu binafsi au shirika ili mradi lalamiko hilo likubaliane na Mkataba wa Afrika na ufumbuzi wa kitaifa umetumika pale ilipowezekana (Kifungu cha 56 (5)).<sup>57</sup> Tume kisha huamua juu ya kukubalika kwa lalamiko hilo. Likikubalika, litapelekwa kwa serikali husika, ambayo inaombwa kujibu maelezo juu ya kesi hiyo na hatua zilizochukuliwa kwa utatuzi wake. Kwa kushauriana, Baraza la Umoja wa Afrika linaweza kuiomba Tume kuchapisha matokeo yake na kutoa mapendekezo. Ikiwa inaonekana kutokea ukiukaji mkubwa, inaweza kuamuriwa ufanyike uchunguzi zaidi. Waandishi Maalum mbalimbali wame wahimiza watu binafsi, wanaharakati, na mashirika kutoa taarifa za matukio ya ukiukaji ili yafanyiwe uchunguzi zaidi na ushiriki wa Serikali mbalimbali juu ya marekebisho. Kutumia Mchunguzi pamoja na Tume ya Afrika kuandaa taarifa zinazoshughulikia au kutaka kusahihiha taarifa zilizotolewa na nchi wanachama, ni utaratibu mwingine ambao unaweza kutumika kupata ufumbuzi kwa ukiukwaji na kutetea heshima ya haki katika ngazi ya kikanda.<sup>58</sup> Taarifa ya Serikali hivi karibuni ilishughulikiwa na Tume ya Haki za Binadamu za Wasagaji na Mashoga ya Kimataifa na Wafanyao Mapenzi Kinyume cha Desturi wa Uganda (SMUG) katika "Taarifa ya Haki za Watu Wasagaji, Mashoga, wanaovutiwa kimpenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenye jinsi mbili katika Jamhuri ya Uganda, chini ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu".<sup>59</sup>

Taarifa kivuli hii iliwasilishwa kwa Tume ya Afrika wakati wa Kikao cha 40, mwezi Novemba 2006 katika kushughulikia taarifa itolewayo kwa vipindi maalum iliyoandaliwa na Serikali ya Uganda kama ilivyowasilishwa na Kikao cha 39. Taarifa vivuli kama hizo hutoa fursa ya kurekebisha makosa yenye ukweli kuhusiana na ukiukwaji wa haki unaofanywa na serikali dhidi ya watu wafanyao mapenzi kinyume

57 Angalia 'Amnesty International' (2006) A Guide to the African Charter on Human and Peoples' Rights. AllIndex:IOR63/005/2006.http://web.amnesty.org/library/Index/ENGIOR630052006?open&of=ENG-373

58 Kupata hadhi ya Uangalizi , inabidi shirika liwe limesajiliwa kisheria.Taarifa juu ya taratibu za kutuma maombi zinapati-kana

59 <http://www.iglhrc.org/files/iglhrc/reports/Uganda%20Shadow%20Report%20.pdf>

na desturi na kuziba mapengo yahusuyo masuala yao yanayoonekana katika taarifa za vipindi maalum zitolewazo na Serikali mbalimbali. Mapendekezo juu ya jinsi Serikali husika, itakavyotatua tatizo hilo, ni sehemu ya mkakati wa ushawishi ambao kisha huhusisha wanachama wengine wa Tume ya Afrika katika kumwajibisha mwakilishi huyo wa serikali.

Shirika lisilo la kiserikali ambalo liliomba hadhi ya mtazamaji kwa Tume ya Afrika ni Muungano wa Wasagaji wa Kiafrika. Maombi ya hadhi<sup>60</sup> ya mtazamaji yalifutwa mwaka 2008, miaka miwili baadaye, tarehe 25 Oktoba, 2010, maombi yao yalikataliwa. Tume ya Afrika ilishindwa kutoa sababu za kukataliwa kwa maombi hayo baada ya kuahirishwa mara mbili kabla.

### Mkutano wa Kijamii wa Dunia

Mbali na kutumia taasisi mbalimbali kupata mabadiliko, wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi wanahitaji kuwa na vikao ambavyo wanaweza kuwasilisha suala lao. Mfano mmoja kama hiyo ni Mkutano wa Kijamii wa Dunia uliofanyika Kenya mwezi Januari, 2007, ambapo mashirika ya wafanyao mapenzi kinyume cha desturi toka duniani kote na hasa Afrika yalitumia fursa hii kuzungumzia wazi matatizo yao na kuelimisha watu wengi kuhusu haki zao na mahitaji yao. Walifanya hivyo kwa kuendesha warsha, wakipanga vipindi kadhaa vyta mazungumzo, na kutoa taarifa kwa njia ya kuonyesha umma. Mwitikio toka kwa wanaharakati wenzao ulikuwa mzuri sana na uliweka msingi wa utetezi zaidi, hasa katika nchi ulipofanyika, Kenya. Maendeleo yaliyofanywa katika mikutano hiyo inapaswa itumike kimkakati na ifuatiliwe na wanaharakati.

### Tuze ya Martin Ennals kwa Watetezi wa Haki za Binadamu mwaka 2011

Katika umri wa miaka 21, Kasha Jacqueline Nabagesera alijihuisha na kufanya kazi ya haki za mashoga nchini Uganda. Kuanzia hapo amekuwa msemaji shupavu kwa haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi. Kasha alikuwa mmoja wa watu wa kwanza kuzungumzia wazi kuhusu utambulisho wake wa kijinsia. Mwaka 2007 baada ya kuzungumza kuhusu heshima na uvumuliu wa mashoga katika Mkutano wa Kijamii wa Dunia nchini Kenya, alinyanyaswa. Ni Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Uhuru na Kutembea Uganda. Jina

60 [http://www.defendingwomen-defendingrights.org/cal\\_application.php](http://www.defendingwomen-defendingrights.org/cal_application.php)

la Kasha lilitokea pia katika gazeti la *Rolling Stone* mapema mwaka jana. Mwaka 2011, Kasha alifanywa mpokeaji wa heshima wa Tuzo ya Martin Ennals kwa Watetezi wa Haki za Binadamu. Licha ya kukabiliana na unyanyaswaji wa umma, Kasha alidumisha uaminifu wa dhamira ya kutetea haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi.

Hata hivyo, wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi wanapaswa kutathmini kwa makini hali hii katika nchi zao. Changamoto ya kwanza ni kutafuta washirika waaminifu, wenye nia thabiti, kukubali juu ya kile cha kufanikisha katika mazingira ya eneo lililotolewa kitaifa, na kuona ni jinsi gani hilo linavyoweza kufanyika kwa ufanisi. Ni muhimu kutambua uwezekano wa waunga mkono wa jambo la mtu, ambayo mara nyingi ni mashirika ya nchini ya wanawake, mashirika ya haki za binadamu ya kimataifa, mashirika ya wahisani, wafanyakazi wa mashirika ya kimataifa, na balozi zilizochaguliwa. Kuunda umoja na mashirika hayo kungeweza kuwa na matokeo mabaya na vile vile mazuri. Kunufaika na nguvu zao za kijamii, kisiasa na kiuchumi kunaweza kusaidia katika kutangaza na kwa kiasi fulani kuhalalisha masuala ya wafanyao mapenzi kinyume cha desturi. Hata hivyo, kuhusiana na kuyashirikisha waziwazi mashirika ya kimataifa katika jitihada za ndani ya nchi, uhamasishaji binafsi, uhalali na kujituma kwa wanaharakati wa nchini inabidi kusizidiwe na msaada wa kimataifa, kwani hoja ya ushoga kuwa "ngeni" na 'isiyo ya Afrika "bado imetawala. Kwa hiyo wanaharakati lazima waingie ushirikiano wa kimkakati na waunga mkono wakizingatia athari zote zinazoweza kutokea na kutumia ushirikiano huo zaidi katika ngazi za kutunga sheria na sera.

Wafadhili na mashirika ya kimataifa kwa upande mwingine lazima kuhusisha mmoja wa wafanyao mapenzi kinyume cha desturi katika shughuli zao kila inapowezekana. Kwa mfano, kualika wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi katika warsha na mafunzo hakutaongeza uwezo wao wa kulinda haki za watu binafsi wafanyao mapenzi kinyume cha desturi tu bali pia kuwazungumzia wanaharakati wenzao maoni yao na kuwafanya wajue suala la kibinadamu ambalo mara nyingi huachwa katika mjadala kuhusu ushoga. Kwa kujumuisha watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi katika huduma ya afya ya uzazi, na programu za

VVU / UKIMWI, mashirika yanaweza kujaribu kupambana na kutelekezwa kulikolikumba kundi hili katika eneo hili na ambalo limeongeza uwezekano wao wa kuwa hatarini zaidi.

Kupata msaada kutoka vyama vya kiraia ni changamoto kubwa ambayo wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi hukabiliana nayo katika mazingira ya sasa kote Mashariki na Pembe ya Afrika. Kubaguliwa kwao kunakoendelea katika harakati za kitaifa za haki za binadamu huwanyima uhalali wao mbele ya umma na Serikali na huchochea uhalifu unaofanywa dhidi ya watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi. Kukutana na wanachama wa vyama vya kiraia kusikofungamana na upande wowote kwa ajili ya uhamasishaji inaweza kuwa mwanzo wa mtazamo chanya zaidi. Kuwashirikisha watunga sera na wabunge katika mikutano kama hiyo katika hatua ya baadaye inaweza kuleta ushawishi ili kuhalalisha ushoga. Kuendeleza hoja toka haki za binadamu na kwa mtazamo wa kisheria kwa namna ya kitaalamu, kwa msaada wa chama cha kiraia na ikiwezekana taasisi za kitaifa za haki za binadamu, kwa mfano Tume ya Haki za Binadamu, inaweza kuchangia kwa mitazamo mizuri na ya kibinadamu zaidi katika masuala ya hatarini na kuruhusu mazungumzo.

Mwaka 2009 Muungano wa vyama vya kiraia vya Haki za Binadamu na Sheria za Kikatiba uliundwa nchini Uganda katika kukabiliana na Muswada wa Sheria ya Kupambana na Ushoga iliyowasilishwa Bungeni na Mhe. David Bahati. Muungano huu unajumuisha wafanyao mapenzi kinyume cha desturi na mashirika mengi yanayodaiwa kutaka kuzuia kupitishwa kwa Muswada huu pamoja na kushughulikia hadi kupata utambuzi kamili na heshima kwa haki za kingono za wananchi wote wa Uganda. Hadi leo, Mswada huu haujapitishwa, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linaweza kupewa sifa shinikizo la kimataifa na kazi kubwa ya Muungano huu na washirika wake.

Kuwaelimisha wananchi wengi ni kujipanga vizuri kwa kuzingatia imani za kidini na kitamaduni zilizo na nguvu ambazo zimeshikiliwa sana. Kukuba masuala ya wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kwa mtazamo fulani ambao unaweza ukasikilizwa

zaidi ni muhimu ili kufanya njia ya kuingiza hilo akilini mwa watu. Shirika la ‘Amnesty International’ katika kitabu chake cha “Mwongozo<sup>61</sup> wa kuendesha Kampeni” linatoa sura juu ya jinsi ya kufanya kampeni kuhusu haki<sup>62</sup> za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi. Utafiti uliofanywa na mfuko wa ‘Urgent Action Fund’ kwa ajili ya Haki za Binadamu za Wanawake ulioitwa ‘LGBTI Organizing in East Africa: The True Test for Human Rights Defenders’(Maandalizi ya wafanyao mapenzi kinyume cha desturi katika Afrika Mashariki: Jaribio la kweli kwa Watetezi<sup>63</sup> wa Haki za Binadamu) hutoa mafundisho kutokana na uhamasishaji wa haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi Kusini mwa Afrika na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuendeleza wazo la haki zao katika mazingira ya Afrika ya Mashariki. Mwaka 2010 Ulinzi wa Kimataifa ilichapisha kitabu cha mwongozo kwa ajili ya wanaharakati wafanyao mapenzi kinyume cha desturi na kinachoitwa ‘Protection Manual for LGBTI Defenders ’ (Mwongozo wa Ulinzi kwa Watetezi<sup>64</sup> wa wafanyao mapenzi kinyume cha desturi) ambacho husaidia kubaini vitisho vya usalama ambavyo ni maalum kwa watetezi wafanyao mapenzi kinyume cha desturi, na kutoa hatua za vitendo vya jinsi ya kuboresha usalama binafsi. Pia mwaka 2010, ‘G-Kenya Trust’ ilichapisha ‘My way, your way, or the RIGHT way?’(Njia yangu, njia yako, au njia<sup>65</sup> SAHIHI?), kitabu kinachoelezea haki zilizokusanywa katika kanuni za Yogyakarta zinazofaa katika muktadha wa Kenya.

Kwa muhtasari, watu wafanyao mapenzi kinyume cha desturi hukabiliwa na ukiukaji wa haki zao za msingi katika Mashariki na Pembe ya Afrika kote. Kwa upande wa watetezi

wao, watetezi wa haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi, kuna changamoto nyingi katika kufikia makubaliano ya jumla ya haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kama haki za binadamu ingawa maendeleo yamepatikana katika miaka ya hivi karibuni. Wakati changamoto hizi zinashughulikiwa kwa ushirikiano na watetezi wa haki za binadamu za kawaida pamoja na za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi, ukiukaji wa haki za wafanyao mapenzi kinyume cha desturi kama vile sheria na matendo ya kibaguzi yanaweza kushughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

'Uafanuzi wa Azimio kuhusu watetezi wa haki za binadamu' ni waraka wa kurasa 100 zinazohamishika toka katika kompyuta, waraka ambaa huelezea haki zilizokubaliwa katika Azimio, kutokana zaidi na taarifa iliyopokelewa na taarifa iliyotolewa na Waandishi Maalum wawili kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu, Hina Jilani (2000-2008) na Margaret Sekagya (tangu 2008), katika kipindi cha miaka kumi na moja iliyopita.

Toka haki ya kulindwa na uhuru wa maoni na kujieleza hadi haki ya kuwasiliana na vyombo vya kimataifa na kupata fedha, uchambuzi wa 'ufafanuzi' wa kile ambacho haki hizi zinahusika nacho na kinachohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wake. Pia linashughulikia vikwazo vya kawaida na ukiukwaji unaowakibili watetezi, na hutoa mapendekezo ya kuwezesha utekelezaji wa Madola kwa kila haki.

[http://www.ohchr.org/  
Documents/Issues/Defenders/  
CommentarytoDeclarationondefendersJuly2011.pdf](http://www.ohchr.org/Documents/Issues/Defenders/CommentarytoDeclarationondefendersJuly2011.pdf)

## **MAKOSA YA BINADAMU, HAKI ZA BINADAMU: MWONGOZO WA CHOMBO CHA HAKI ZA BINADAMU CHA UMOJA WA MATAIFA *Tume ya Haki za Binadamu ya Ireland ya Kaskazini na Ulinzi wa Haki za British Irish (2011)***

Huu ni mwongozo ambaa utayasaidia mashirika yasiyo ya kiserikali, wanasheria, na watu binafsi kutumia njia zao kati ya mifumo mbalimbali ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa. Mifumo hii inaweza kuonekana migumu kwa wale wasioizoea lakini, kama mwongozo huu unavyoonyesha, kwa kweli zinapatikana na ni rahisi kutumia. Ingawa kimsingi ilikusudiwa wasomaji wa nchini Uingereza na Ireland, sehemu kubwa ya taarifa na utambuzi uliomo katika mwongozo huu utakuwa wa manufaa kwa watu katika nchi nyingi duniani.

Chanzo: [http://www.frontlinedefenders.org/  
manuals/human-wrongs-human-rights](http://www.frontlinedefenders.org/manuals/human-wrongs-human-rights)

## **Nyingine**

## **JITIHADA ZA NORWEI KUWAUNGA MKONO WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU: MWONGOZO WA HUDUMA ZA NJE (2010)**

Imeandaliwa miongozo kwa balozi zinazohusiana na msaada wa Norwei kwa ajili ya watetezi wa haki

za binadamu, ili kuimarisha msaada wa Norwei wa nchi na nchi kwa ajili ya kundi hili. Lengo kuu la miongozo hii ni kuisaidia Wizara ya Mambo ya Nje na balozi za Norwei kuzipanga hatua kiutaratibu na kuongeza juhudii za kuwasaidia watetezi wa haki za binadamu na kazi yao. Moduli kuhusu watetezi wa haki za binadamu kwa ajili ya kozi ya mafunzo ya elektroniki ya Taasisi ya Huduma za Nje kuhusu haki za binadamu pia imeanzishwa, kama hatua ya kujenga uwezo.

Chanzo:[http://www.regjeringen.no/en/dep/ud/  
Documents/veiledninger/2010/hr\\_defenders\\_  
guide.html?id=633052](http://www.regjeringen.no/en/dep/ud/Documents/veiledninger/2010/hr_defenders_guide.html?id=633052)

# Kiambatanishi cha 3

## Rasilimali kwa Watetezi wa Haki za Binadamu

### **Ulinzi na Usalama kwa Watetezi wa Haki za Binadamu**

#### **Kiongozi kipyä cha Ulinzi kwa Watetezi wa Haki za Binadamu *Ulinzi wa Kimataifa (2009)***

Madhumuni ya kiongozi hiki kipyä ni kuwaongeza watetezi wa haki za binadamu maarifa na nyenzo ambazo zinaweza kuwa za manufaa kwa kuboresha uelewa wao juu ya usalama na ulinzi. Kuna matumaini kwamba kiongozi hiki kitasaidia mafunzo juu ya usalama na ulinzi na kuwasaidia watetezi kufanya tathmini zao wenyewe za hatari na kufafanua kanuni na taratibu za usalama na ambazo zitaambatana na mazingira yao maalum. Kiongozi hiki ni matokeo ya uzoefu wa pamoja wa zaidi ya miaka 25 wa wajumbe wa Ulinzi wa Kimataifa katika kufanya kazi na haki za binadamu na sheria ya kibinadamu na katika ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu na makundi mengine yenye mazingira magumu. Uzoefu wa wajumbe wa Ulinzi wa Kimataifa unatokana na kujihusisha na kushiriki kwao kwa mara ya kwanza katika Vikosi vya Amani vya Kimataifa - kazi na muundo wa ugani wa Vikosi vya Amani vya Kimataifa. Tumekuwa na fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu na maarifa na mamia ya watetezi ugani, hali kadhalika katika warsha, mikutano na majadiliano juu ya usalama. Mengi ya maudhui ya kiongozi hiki tayari yameshatumika kwa vitendo, ama katika kazi ya ulinzi au katika warsha za mafunzo na watetezi. Kiongozi hiki ni matunda ya majadiliano yote haya, na tuna deni kubwa kwa watetezi walioshiriki kwa mchango wao.

Chanzo: <http://www.protectionline.org/New-Protection-Manual-for-Human>

#### **Kitabu cha mafunzo kuhusu usalama: Hatua thabiti kwa watetezi wa haki za binadamu walio hatarini *'Front Line' (2011)***

Kitabu cha mafunzo kuhusu Usalama kimebuniwa ili kuinua mwamko katika masuala ya usalama na kuwasaidia watetezi wa haki za binadamu kufikiria namna ya kupunguza vitisho. Kitabu hiki kinawasaidia watetezi wa haki za binadamu kujifunza hatua za kuunda mpango wa usalama - kwa watu binafsi na kwa mashirika. Kinafuata njia ya utaratibu wa kutathmini hali ya usalama wao na

kuendeleza mikakati na mbinu za kupunguza hatari na uwezekano wa kupata madhara.

Chanzo: [http://www.frontlinedefenders.org/files/Workbook\\_ENG.pdf](http://www.frontlinedefenders.org/files/Workbook_ENG.pdf)

#### **Usalama katika Kisanduku**

#### **'Front Line' na Mbinu za Pamoja za Teknolojia (2011)**

Usalama katika sanduku-ni juhudhi za Mbinu za Pamoja za Teknolojia na 'Front Line'. Iliundwa ili kutimiza mahitaji ya usalama na faragha ya mfumo wa kupokea na kutuma taarifa kwa tarakimu, ya mawakili na watetezi wa haki za binadamu. Usalama katika kisanduku ni pamoja na Jinsi ya kuandaa kijarida, ambayo inazungumzia masuala kadhaa muhimu ya usalama wa mfumo wa kupokea na kutuma taarifa kwa tarakimu. Pia hutoa mkusanyiko wa Miongozo-kwa-Vitendo kila mmoja ukiwa na programu fulani ya kompyuta isiyolipiwa au chombo cha programu ya kompyuta ya chanzo wazi, pamoja na maelekezo ya jinsi ya kutumia chombo hicho kulinda kompyuta yako, kulinda taarifa zako au kudumisha faragha ya mawasiliano yako ya Intaneti.

Chanzo Rasmi: <http://security.ngoinabox.org/>

Kiingereza: <https://security.ngoinabox.org/en>

Kifaransa: <https://security.ngoinabox.org/fr>

Kiarabu: <https://security.ngoinabox.org/ar>

#### **Mwongozo makini wa Kulinda Usalama wa Utambulisho wako na Dhamana ya Mtandao wa Intaneti Wakati wa Kutumia Simu za Mkononi (2011)**

Mwongozo huu umeandikwa kwa ajili ya raia wa Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini, ambao wanataka kutumia teknolojia kwa usalama kuwasiliana, kupanga, na kupeana data (taarifa mpya, habari, vyombo vya habari nk), lakini inaweza kutumiwa na mtu ye yeyote katika mtandao wa intaneti anayetaka kulinda faragha na usalama wake mahali popote. Umeandikwa kwa ajili ya hadhira kubwa iliyo na elimu ya wastani ya kompyuta, ambao wangependa kujua hatua wanazoweza kuchukua ili kuwa salama zaidi katika mtandao wa intaneti na wakati wa kutumia vyombo vya simu za mikononi. Mwongozo huu una vidokezo na nyenzo za

kupunguza uchunguzi na ufuatiliaji, kulinda faragha, na kushughulikia udhibiti. Unashughulikia: matumizi salama ya barua pepe na kupiga gumzo, tabia nzuri za neno la siri, jinsi ya kuweka kompyuta yako isipate virusi na taarifa zako zilizomo humo kuzipata mtu mwingine kwa njia ya wizi, jinsi ya kupata udhibiti wa mtandao wa intaneti wakati ukiwa hutumii majina, mbinu za kutumia simu za mkononi kwa usalama, na ukiwa na vyanzo kwa rejea za kina zaidi.

Chanzo: [http://www.protectionline.org/IMG/pdf/fcea379753a53a03bf\\_ofm6bnld6.pdf](http://www.protectionline.org/IMG/pdf/fcea379753a53a03bf_ofm6bnld6.pdf)

### **Usimamizi wa Usalama wa Utendaji katika mazingira ya ukatili (2010)**

#### **Mtandao wa Matendo ya Kibinadamu (2010)**

Tangu kuchapishwa kwa toleo la kwanza la Mapitio ya 8 ya Matendo Mema juu ya Usimamizi wa Usalama wa Utendaji katika mazingira ya ukatili muongo mmoja uliopita, mazingira ya usalama wa kimataifa yamebadilika kwa kiasi kikubwa. Mazingira mapya ya migogoro yameunda vyanzo vipyta vya tishio kwa utekelezaji wa kibinadamu kimataifa. Kuongeza ukatili dhidi ya wafanyakazi wanaotoa misaada na shughuli zao, zikiwemo utekaji nyara na mashambulizi ya kuua zaidi, yamekuwa na athari kubwa kwa kazi za kibinadamu zenyne unafuu katika mazingira yasiyo salama. Wakati huo huo, mashirika yenye yamekuwa makini zaidi kwa haja ya kutoa usalama na dhamana ya wafanyakazi wao. Ili kuongeza mabadiliko haya, Mtandao wa Matendo ya Kibinadamu umechapisha toleo jipya la GPR 8. Toleo jipya hili pia linarekebisha maelezo ya awali na pia kutoa mada mpya, kama vile mitazamo ya usalama wa kupanga programu za 'usimamizi wa mbali, utendaji bora katika uratibu wa usalama baina ya mashirika na jinsi ya kufuatilia, kupeana taarifa za usalama na kuzichambua. Toleo jipya pia linatoa njia panuzi zaidi ya kusimamia matukio muhimu, hasa katika utekaji nyara na uchukua jiteka, na kujadili masuala yanayohusiana na tishio la ugaidi.

Chanzo: <http://www.odihpn.org/hpn-resources/good-practice-reviews/operational-security-management-in-violent-environments-revised-edition>

### **Kamera kila mahali: Changamoto za sasa na Fursa katika Mahusiano ya Haki za Binadamu, Video na Teknolojia Ushahidi (2011)**

Taarifa hii huuliza maswali magumu kuhusu jinsi

ya kulinda na kuwawezesha wale wanaojaribu kuongeza wazi dhulma kwa njia ya video. Hutoa mapendekezo maalum kwa ajili ya hatua za haraka na za baadaye ambazo zinaweza kupunguza hatari kwa wale wanaohatarisha maisha yao. Taarifa hii ni hatua muhimu katika kuelewa jinsi tunavyowenza kuunganisha nguvu za video na teknolojia ili kuwawezesha wanaharakati kulinda na kutetea haki za binadamu. Hii ni enzi ya teknolojia ya kuleta mabadiliko.

Kiingereza: <http://witness.org/cameras-everywhere/report-2011/inquiry-form>

Kiarabu: [http://witness.org/sites/default/files/downloads/ce\\_exec\\_summary\\_arabic-final2.pdf](http://witness.org/sites/default/files/downloads/ce_exec_summary_arabic-final2.pdf)

### **Utaratibu Bora wa Watetezi wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Mafundisho Yaliyoyapatikana: Sheria, Sera ya Taifa na Vitengo vya Watetezi (Juzuu ya I)**

#### **Ulinzi wa Kimataifa (2009)**

Katika miaka ya karibuni serikali kadhaa zimeunda taratibu maalum za kitaifa za kuwalinda watetezi, wote katika nchi zenyne ukosefu mkubwa wa ulinzi kwa ajili ya watetezi wa haki za binadamu. Taratibu hizi (sheria, sera za utekelezaji, ofisi) zimeanzishwa kwa shinikizo kutoka (na kwa ushirikiano wa) mashirika ya kitaifa na kimataifa ya haki za binadamu, pamoja na msaada muhimu wa kisheria kutoka kwenye Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu.

Katika **Ulinzi wa Kimataifa**, hali hii imetufanya tujifunze juhudini za kitaifa: ni zipo hizo na zina nini ndani yake? Zilitokeaje, hufanyaje kazi na zina athari gani kwa ulinzi wa watetezi? Tulianzisha kikundi cha utafiti (kilichoundwa na wanasheria na wataalam wa ulinzi) na kufanya mahojiano mengi na watetezi wanaume na wanawake pamoja na viongozi wa serikali katika nchi 16 katika mabara matatu. Pia tulilingia katika mchakato wa kuandaa na kuchambua vyombo vya utekelezaji wa sheria katika ngazi ya kitaifa (wakati tukichunguza za kimataifa na za kikanda zilizopo). Wakati wa utafiti huu tuliona juhudini za kitaifa zisizo za kiserikali tu za aina hii katika Brazil, Colombia, Guatemala, Mexico na Peru (Marekani ya Kati na ya Kusini), Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Afrika) na Nepal (Asia). Wakati kunaweza kuwepo mashirika kadhaa yanayofanya kazi katika masuala yanayohusiana na ulinzi na kutoa michango muhimu, ni Guatemala (UDEFUGUA), Uganda (EHAHRDP) na Colombia (Somos Defensores Programu) tu walio na vitengo vitatu vya watetezi vilivyoanzishwa mahsusini na asasi

za kiraia. Wao ni waanzilishi katika uwanja huu na pamoja na Ofisi za Ulinzi zilizoanzishwa na Ulinzi wa Kimataifa na mashirika ya kutoa misaada (kama vile Vikosi vya Amani vya Kimataifa), ni mionganini mwa vikundi hivyo vya asasi za kiraia ambazo kazi yake ya pekee ni ya ulinzi wa watetezi wa mahali husika.

Chanzo: <http://focus.protectionline.org/-Protection-of-human-rights->

### **Utendaji Bora wa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu na Mafundisho Yaliyopatikana: Mitazamo ya Uendeshaji wa Ulinzi wa Watetezi (Juzuu ya II)**

***Ulinzi wa Kimataifa (2009)***

Juzuu hii ya pili, "Programu ya Ulinzi kwa Watetezi", huchambua mitazamo inayotekelzeza ya programu za ulinzi: hatua hizi ni pamoja na, jinsi ilivyoundwa, na matokeo yake. Kitabu hiki kinalenga nchi tatu ambazo ulinzi wake ulichunguzwa, yaani Brazil, Guatemala na Colombia.

Chanzo: [http://www.protectionline.org/Protection-of-human-rights\\_10400.html](http://www.protectionline.org/Protection-of-human-rights_10400.html)

Kiarabu: [http://www.protectionline.org/IMG/pdf/manual\\_arabic\\_pi\\_1st\\_edition\\_2009\\_web.pdf](http://www.protectionline.org/IMG/pdf/manual_arabic_pi_1st_edition_2009_web.pdf)

## **Kutetea Haki za Binadamu**

### **Kufuatilia na Kuchunguza Mauaji ya Kisiasa Shirika la 'Amnesty International' na 'CODESRIA' (2000)**

Utumiaji wa kanuni za jumla kwa ajili ya ufuatiliaji na uhifadhi wa nyaraka ulioelezwa bayana kwa masharti ya kufuatilia kesi ya mtuhumiwa wa mauaji ya kisiasa.

Chanzo: [http://www.protectionline.org/IMG/pdf/spa\\_killings.pdf](http://www.protectionline.org/IMG/pdf/spa_killings.pdf)

### **Ukweli - Kufuatilia na Kuhifadhi Taarifa za Ukiukwaji wa Haki za Binadamu katika Afrika Shirika la Amnesty International na CODESRIA (2000)**

Kitabu hiki na vijitabu vinavyoendana vilianzishwa ili kutekeleza madai ya mtazamo wa ufanisi zaidi, wa kitaalamu na wenyewe msingi wa mahali husika kwa ufuatiliaji, uhifadhi wa nyaraka na kutafuta ukweli wa haki za binadamu katika Afrika. Ukusanyaji huu

unalenga kuwezesha mashirika ya haki za binadamu na wanaharakati binafsi kufanya ufuatiliaji, uhifadhi wa nyaraka na kutafuta ukweli, na kufanya hivyo kwa kutumia utendaji bora na uzoefu wa watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika.

Chanzo: [http://www.protectionline.org/IMG/pdf/Ukweli\\_eng.pdf](http://www.protectionline.org/IMG/pdf/Ukweli_eng.pdf)

### **Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai - Taarifa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu 'Front Line'**

Watetezi wa 'Front Line' wamechapisha kitabu cha mwongozo kuhusu Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai kwa watetezi wa haki za binadamu. Mwongozo huu una taarifa muhimu juu ya jinsi Mahakama inavyofanya kazi, inavyoweza kufikiwa, na jinsi mtu binafsi anavyoweza kuitumia Mahakama.

Chanzo: <http://www.frontlinedefenders.org/manuals/the%20international%20criminal%20court>

### **Mbinu Mpya katika Haki za Binadamu: Kimbilio la Mhalifu**

***Mbinu Mpya katika Haki za Binadamu (2004)***

Top of Form

Duniani kote na katika ngazi zote, katika vijiji vidogo na katika serikali za kitaifa hali kadhalika katika ngazi za juu za haki ya kimataifa, watu wanajenga na kutumia mbinu za kiubunifu kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Mbinu Mpya katika Mradi wa Haki za Binadamu hudhibiti ubunifu wa mbinu hizi na kushirikiana nazo na wengine wanaojitahidi kuendeleza haki za binadamu.

Chanzo: <http://www.newtactics.org/ToolsforAction/TheNewTacticsWorkbook/Readordownloadfiles>

Kiarabu: <http://www.newtactics.org/ar/tools/new-tactics-human-rights-resource-practitioners>

Kifaransa: <http://www.newtactics.org/fr/tools/new-tactics-human-rights-resource-practitioners-french>

Kiswahili: <http://www.newtactics.org/sw/tools/new-tactics-human-rights-resource-practitioners>

**Utekelezaji wa Uhuru wa Kujieleza: Orodha ya Kuzingatia kwa Utekelezaji wa Azimio la Kanuni kuhusu Uhuru wa Kujieleza barani Afrika**  
**Kifungu cha 19 (2006)**

Orodha hii ya kuzingatia imetungwa mahsus i kwa ajili ya mashirika ya vyama vya kiraia katika Afrika na mahali pengine kwa wale wanaotaka kufanya uchambuzi wa kina wa hali ya utekelezaji wa Azimio la Kanuni kuhusu Uhuru wa Kujieleza katika nchi yoyote ya Afrika. Orodha hii inaruhusu mashirika ya vyama vya kiraia vinavyofanya kazi kuhusu masuala yanayohusiana na uhuru wa kujieleza na kupata taarifa ili kuthibitisha mapungufu kwa kigezo cha masharti thabiti kwa ajili kya kutimiza na kulinda uhuru wa kujieleza. Kwa sababu hiyo, baadhi ya maswali huhusu maeneo makubwa zaidi ya suala lenyewe la uhuru wa kujieleza. Orodha ya kuzingatia hutafiri kila kifungu cha Azimio kwa kina, hutoa maelezo ya kutosha juu ya jinsi uhuru wa kujieleza unavyoweza kutekelezwa na kutolewa.

Chanzo: <http://www.article19.org/data/files/pdfs/tools/africa-foe-checklist.pdf>

**Ufuatilaji wa vurugu zilizofadhiliwa na Serikali katika Afrika**  
**Kifungu cha 19 (2000)**

Mwongozo huu una lengo la kufuatilia vurugu zilizofadhiliwa na serikali katika Afrika na, hasa, kile tunachokiita "ukandamizaji usio rasmi": hutupia macho shughuli ambazo mkono wa serikali umefichwa au kugeuziwa mgongo. Hata hivyo, ujuzi mwangi unaweza kutumika katika mazingira mbalimbali ya aina tofauti. Ingawa umelenga wanaharakati wa haki za binadamu nchini Kenya, Nigeria na Afrika Kusini, ni matumaini yetu itakuwa ya manufaa katika kuwapa mafunzo wafuatilaji katika Afrika nzima na hata mahali pengine. Wanaharakati wa haki za binadamu wanapaswa kujisikia huru kurahisisha au kutumia sehemu za mwongozo huu ili kutimiza mahitaji yao maalum, ikiwa ni pamoja na kutafsiri katika lugha za kienyeji.

Chanzo: <http://www.article19.org/data/files/pdfs/tools/monitoringviolenceafrica.pdf>

**Mwongozo wa Haki za Uchumi, Kijamii na Kiutamaduni kwa Mtandao wa Intaneti**  
**'Front Line' (2003)**

'Front Line' iliamuru Kituo cha Utekelezaji wa Haki za Kijamii na Kiuchumi kutengeneza mwongozo kupitia

mtandao wa intaneti ukilenga hasa haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.

Chanzo: <http://www.frontlinedefenders.org/manuals/eco-soc-cul>

**Mwongozo wa Haki za Kiraia na Kisiasa**  
**'Front Line' (2003)**

'Front Line' iliamuru Washauri wa Haki za Binadamu kutengeneza mwongozo unaoruhusu kuathiriana kupitia mtandao wa intaneti kwa ajili ya watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi ya Haki za Kiraia na Kisiasa.

Chanzo: <http://www.frontlinedefenders.org/manuals/frontline-civil-political-rights>

Kiingereza: <http://www.frontlinedefenders.org/manual/en/>

Kiarabu: <http://www.frontlinedefenders.org/manual/ar/>

Kifaransa: <http://www.frontlinedefenders.org/manual/fr/>

**Uandishi wa habari, vyombo vya habari na changamoto ya utoaji taarifa za haki za binadamu**

**Sera ya Baraza la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu (2002)**

Madhumuni ya taarifa hii ni kujadili matatizo ya kutoa taarifa za masuala ya haki za binadamu na kuthibitisha mafundisho yanayoweza kupatikana kutohakana na uzoeufu mbalimbali ili kutoa mapendekezo thabiti kwa taaluma ya uandishi wa habari, watunga sera, na watetezi wa haki za binadamu. Lengo ni kuboresha ubora na uthabiti wa kazi katika eneo hili.

Chanzo: [http://www.ichrp.org/files/reports/14/106\\_report\\_en.pdf](http://www.ichrp.org/files/reports/14/106_report_en.pdf)

## **Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu**

**Mwitikio wa Haraka kwa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu walio Hatarini: Kupanga na Tathmini ya Awali  
Chama cha Haki za Wanawake katika Maendeleo (2011)**

Chama cha Haki za Wanawake katika Maendeleo na Muungano wa Kimataifa wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu walifanya marekebisho makubwa mbalimbali ya mwitikio wa haraka unaopatikana kwa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu walio hatarini duniani kote. Taarifa hii inaeleza aina ya nyenzo na mikakati inayopatikana ili kukabiliana na hali ya dharura ya vurugu dhidi ya Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu na pia baadhi ya mashirika ambayo huwapatia.

Chapisho hili ni sehemu ya mfululizo mpya ambao Chama cha Haki za Wanawake katika Maendeleo hutoa pamoja na Muungano wa Kimataifa wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu. Malengo ya mfululizo huu wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu ni kuongeza ufahamu wa nyenzo zilizopo kusaidia na kutetea Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu na kuhakikisha kuwa wanawake wanaharakati wa haki duniani kote wana taarifa muhimu kwa kupata nyenzo hizi kwa urahisi.

Kiingereza: <http://www.awid.org/Media/Files/WHRD-Urgent-Responses-ENG>

Kiarabu: <http://www.awid.org/Media/Files/urgent-responses-arabic>

**Kuzifanya haki kuwa uhalisia – Mfuko wa vifaa kwa ajili ya warsha kuhusu kukomesha ukatili dhidi ya wanawake**

***Shirika la 'Amnesty International' (2004)***

Mwongozo wa wajibu wa mataifa kuzifanya haki za wanawake kuwa halisia - kutekeleza majukumu yao chini ya sheria ya kimataifa ya mikataba na mila ili kuheshimu, kulinda na kutekeleza haki za binadamu katika sheria na vitendo.

Chanzo: <http://www.amnesty.org/fr/node/867>

**Kitabu cha rejea kuhusu Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu**

***Ushauri wa kimataifa kuhusu Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (2005)***

Ukusanyaji wa makala zilizowasilishwa katika vikao vya kwanza vya mkutano wa Ushauri wa Kimataifa

kuhusu Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu uliofanyika Colombo, Sri Lanka kati ya tarehe 29 mwezi Novemba – tarehe 2 mwezi Desemba, 2005. Makala hizi zimepangwa katika sehemu tano: maelezo ya muktadha na mantiki ya kampeni, historia na dhana ya istilahi, masuala muhimu yanayowakabili wanawake watetezi wa haki za binadamu, mapendekezo kwa ajili ya mikakati ya ulinzi, na uwajibikaji kwa wanawake wanaofanya kazi katika kutafuta haki.

Chanzo: <http://www.forum-asia.org/?p=5422>.

## **Mapendekezo ya Utekelezaji Mahsusni wa Jinsia wa Mwongozo wa Umoja wa Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu**

Waraka huu wa rasimu unaonyesha mapendekezo thabiti kwa ajili ya Balozi za wananchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (ikiwa ni pamoja na wajumbe wa balozi mbalimbali na balozi ndogo za nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya na Tume ya Ulaya) katika utekelezaji wa "Kuhakikisha ulinzi - Miongozo ya Umoja wa Ulaya kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu" (Miongozo ya Umoja wa Ulaya). Imekusudiwa mahsusni kuhakikisha msaada stahiki na ulinzi wa wanawake watetezi wa haki za binadamu.

Chanzo: <http://www.omct.org/violence-against-women/statements/2006/11/d18321/>

**Mikakati ya Usalama ya Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu: Msisitizo, Msimamo, Upinzani, Uwepo**

***Mfuko wa 'Urgent Action Fund' (2008)***

Upinzani hutuletea sauti za wanawake watetezi wa haki za binadamu kutoka duniani kote. Kila mwanamke anaongea kutokana na uzoefu wake binafsi juu ya kupambana na ukatili na ubaguzi katika mazingira magumu - katika hali ya migogoro dhahiri au ya kificho, vurugu zilioandaliwa za kutumia silaha pamoja na kuongezeka kwa imani kali ya kidini nchini Iran, Colombia, Nepal, Burma, Thailand, Algeria, Tunisia, Bosnia, Serbia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Upinzani ni safari na sherehe ya ujasiri. Mikakati ya kushangaza ambayo huwawezesha wanawake watetezi wa haki za binadamu kuishi, kustawi na kufanikiwa - licha ya changamoto na hatari za kazi hii, na ufinyu mkubwa wa nyenzo na msaada. Upinzani hutambulisha dhana ya 'usalama unganishi' – iliyobuniwa na wanaharakati wa Colombia na kuungwa mkono na wanawake watetezi wengine wa haki za binadamu duniani kote: dhana ambayo hutupa changamoto sisi kutafsiri upya dhana ya 'usalama' iliyo fanywa

kama jeshi, ikatenganishwa na kutambua kwamba usalama unganishi ni kuhusu kujisikia salama katika nyanja zote za maisha yetu - kutoka kwenye uwezo wetu wa kulisha familia zetu hadi kuzungumza kwa uhuru juu ya serikali zetu.

Chanzo: <http://urgentactionfund.org/index.php?id=144>

Kiingereza: <http://urgentactionfund.org/assets/files/Resiste/Resiste-Final-Web.pdf>

Kifaransa: [http://urgentactionfund.org/assets/files/uafpubs/FINAL\\_WEB\\_French\\_Insiste\\_Persiste.pdf](http://urgentactionfund.org/assets/files/uafpubs/FINAL_WEB_French_Insiste_Persiste.pdf)

Kiarabu:<http://urgentactionfund.org/assets/files/Resiste/Insiste%20Persiste%20Resiste%20Existe%20Arabiska.pdf>

## **Watetezi wa Kundi la Wachache**

**Haki za Wasagaji, Mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenye jinsi mbili:**

***Mtazamo wa Haki za Binadamu (2000)***

Mitaala hii inakusudiwa kuendeleza uchunguzi makini zaidi na hatua ya busara mionganoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari kuhusu masuala ya wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenye jinsi mbili. Hata hivyo, tofauti na mitaala miingine, mjadala huu si katika mazingira ya haki za kiraia au kisiasa bali katika mukhtadha mpana wa haki za binadamu. Haki hizi, kama zilivyoolezwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, mionganoni mwa nytingine, ni pamoja na haki ya elimu, utambulisho, usalama, mkusanyiko, kujieleza, ajira, afya, na 'family' muhimu kwa mjadala wa sasa wa haki za wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenye jinsi mbili.

Chanzo: <http://www1.umn.edu/humanrts/edumat/hredusers/TB3/toc.html>

***Mwongozo wa Ulinzi kwa Watetezi wa Wafanya mapenzi kinyume cha desturi Ulinzi wa Kimataifa (2010)***

Ulinzi wa Kimataifa umekuwa ukifanya kazi katika ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu kwa miaka kadhaa. Hadi sasa kazi yetu imelenga zaidi juu ya watetezi wa haki za binadamu wa kawaida wanaofanya kazi katika hali ya migogoro ya wazi. Katika mazungumzo na watetezi mbalimbali

wanaofanya kazi juu ya haki za wanovutiwa na aina mbalimbali za kufanya mapenzi, yaani na jinsi yake, tofauti au zote na utambulisho wa kijinsia ikawa dhahiri kwamba tunahitajika kupanua mtazamo wetu na kazi yetu ili kujumuisha na maelezo ya kina ya mada hii inayoikabili sekta hii ya jamii ya haki za binadamu. Majadiliano mengi juu ya aina ya muundo wa kutumia kwa hili ilitokea katika kipindi cha miezi kadhaa yaliyoshirikisha mazungumzo na aina zote mbalimbali za watetezi, wa kawaida na "wasio wa kawaida". Ulinzi wa Kimataifa ulizifanya kazi hoja na maoni ya ukosoaji yaliyofanywa kuhusu vitabu vyake vya awali vya miongozo kwa ajili ya ulinzi wa watetezi na kuanza kuangalia jinsi ya kushughulikia haja ya kuzungumzia maelezo ya mada hii. Kwa kutumia kazi yake na watetezi wa wafanya mapenzi kinyume cha desturi nchini Nepal na kuthibitishwa na watetezi wengine kote duniani ilianza kubaini masuala ya kawaida ambayo yaliathiri jamii yetu na wale wanaoitetea. Utafiti wa kina ulifanya, vyanzo vikuu na pia vidogo vilitakwa ushauri na Ulinzi wa Kimataifa ulianza kutumia mfumo wake kuendana na watetezi wa kawaida.

Mwongozo huu ni matokeo ya mchango wa watu wengi si tu kwa utafiti na kitengo cha mafunzo cha Ulinzi wa Kimataifa. Umeundwa uwe wa vitendo, umeundwa kutia changamoto, kuzua mjadala katika mashirika na labda kuhamasisha zaidi katika mfumo wa ulinzi wetu kwa ujumla. Ina maana gani kuingiza Vifupisho zaidi na zaidi bila kurekebisha mazungumzo na ajenda yetu, na zaidi ya hivyo kurekebisha hatua zetu za usalama ili kuhakikisha kuwa mfumo wetu kweli unafanya kazi yake ya ulinzi? Mwongozo huu umepimwa, umekubaliwa na Ulinzi wa Kimataifa unatumaini kuwa utaendelea kukua na kwa matumaini kuendelea kufaa katika maudhui yake kwa jamii ya wafanya mapenzi kinyume cha desturi. Inaweza tu kufanya hivyo ikiwa watetezi hao watashiriki katika mchakato huu ulioanza.

Chanzo: <http://www.protectionline.org/Protection-Manual-For-LGBTI.html>

***Haki za Binadamu za Watu Wasagaji, Mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili, wenye jinsi mbili: Utangulizi wa kufanya kazi na Vyombo vya Umoja wa Mataifa vya Ufutiliaji Mikataba na Taratibu Maalum za Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa***

***Shirika la Amnesty International (2005)***

Madhumuni ya waraka huu ni kutoa mwongozo wa msingi juu ya jinsi asasi zisizo za kiserikali zinavyoweza kutumia vyombo vya Umoja wa

Mataifa vya Ufutiliaji Mikataba (inajulikana kama "Vyombo vya Mikataba") na Taratibu Maalum za Tume ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu (Tume) kuibua masuala juu ya kuendeleza na kulinda haki za binadamu za watu ambao ni wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili au wenyе jinsi mbili. Waraka huu unatoa ushauri wa vitendo juu ya jinsi ya kutumia vyombo hivi kuinua masuala binafsi pamoja na hali ya jumla ya ukiukwaji wa haki za binadamu za watu wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenyе jinsi mbili.

Chanzo: <http://www.amnesty.org/en/library/info/IOR40/004/2005>.

### **Kanuni za Yogyakarta (2006)**

Mwaka 2006, katika kukabiliana na mifumo ya unyanyasaji iliyothibitishwa vizuri, kundi la wataalamu wa kimataifa wa haki za binadamu wenyе sifa walikutana Yogyakarta, Indonesia na kueleza kwa muhtasari kanuni za kimataifa zinazohusiana na tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi na utambulisho wa kijinsia. Matokeo yake yalikuwa Kanuni za Yogyakarta: mwongozo wa jumla wa haki za binadamu unaothibitisha viwango vya kisheria vya kimataifa vyenye masharti ambavyo mataifa yote lazima kuyazingatia. Zinaleta matumaini tofauti kwa siku zijazo ambapo watu wote waliozaliwa huru na wenyе utu na haki sawa wanaweza kupata haki hiyo ya thamani kutokana na uzawa wake.

Chanzo: <http://www.yogyakartaprinciples.org/>

# Kiambatanisho cha 4

## Mashirika yanayofanya kazi na watetezi wa Haki za Binadamu Mashirika

### Amnesty International (Msamaha wa Kimataifa)

Shirika lisilo kwa ajili ya kujitengenezea faida, lililoko Uingereza, linalomtetea kila mtu kunufaika na haki zote za binadamu zilizopo kwenye Azimio la kimataifa la Haki za Binadamu na viwango vingine vya kimataifa vya haki za binadamu.

Chanzo Rasmi: <http://www.amnesty.org>

### Article 19 (Kifungu cha 19)

Shirika lisilo kwa ajili ya kujitengenezea faida, lililoko Uingereza, linalotetea uhuru wa kujieleza kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 19 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu.

Chanzo Rasmi: <http://www.article19.org>

### Avocats Sans Frontières (Watetezi Wasio na Mipaka)

‘Avocats Sans Frontières’ wanaingilia nchi ambayo haki za binadamu haziheshimiwi, ambapo vurugu za kisiasa na utawala wa migogoro ya kutumia silaha, na ambapo kanuni za kisheria zimekiukwa. Haki katika nchi hizo, mara nyingi ni za kiholela, hazihakikishii usalama wa watu. Migogoro haitatuliwi kwa kiwango cha kuridhisha katika mahakama za nchi. Watu ambaeo haki zao zimekiukwa hukimbilia kwa wanaajaribu kuleta haki kwa kupambana na uhalifu katika nchi zao, ambayo huendelea kuwa sheria yenye nguvu au madhubuti zaidi, na kuchangia kwa hali ya ghasia.

Chanzo Rasmi: <http://www.asf.be/>

### Committee to Protect Journalists (Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari)

Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari ni shirika lisilo kwa ajili ya kujitengenezea faida, linalojitegemea, linalokuza uhuru wa habari duniani kote kwa kutetea haki za waandishi kutoa taarifa za habari bila hofu ya kulipiziwa kisasi.

Chanzo Rasmi: <http://www.cpj.org>

### Commonwealth Human Rights Initiative (Jitihada za Haki za Binadamu za Jumuiya ya Madola)

Commonwealth Human Rights Initiative (CHRI) ni shirika la kimataifa lisilo la kiserikali, linalojitegemea, kisilokuwa la kisiasa, lililo na madaraka ya kuhakikisha utekelezaji wa vitendo wa haki za binadamu katika nchi za Jumuiya ya Madola. Mwaka 1987, vyama kadhaa vya kitaalam vya Jumuiya ya Madola vilianzishwa. Waliamini kuwa wakati Jumuiya ya Madola inazipa nchi wanachama maadili ya pamoja na kanuni za kisheria za kuzingatia katika kufanya kazi na kuendesha mkutano ambaeo utaendeleza haki za binadamu, kulikuwa na uzingativu mdogo juu ya masuala ya haki za binadamu katika Jumuiya ya Madola.

Chanzo Rasmi: [www.humanrightsinitiative.org/](http://www.humanrightsinitiative.org/)

### European Centre for Development Policy Management (Kituo cha Usimamizi wa Sera ya Maendeleo cha Ulaya)

Kituo cha Usimamizi wa Sera ya Maendeleo cha Ulaya husaidia kupunguza uundaji wa sera ‘zisizo pacha’ kati ya Afrika, Caribbean na Pacific na Umoja wa Ulaya. Hii hufanyika kwa kuimarisha uwezo wa mashirika ya umma, binafsi na mashirika yasiyo kwa ajili ya kujitengenezea faida katika nchi za Afrika, Caribbean na Pacific ili kusimamia vizuri sera za maendeleo yao wenyewe na ushirikiano wa kimataifa. Kituo cha Usimamizi wa Sera ya Maendeleo cha Ulaya pia hufanya kazi na serikali na mashirika katika Ulaya ili kufanya sera na nyenzo za maendeleo kuwa za ufanisi zaidi.

Chanzo Rasmi: <http://www.ecdpm.org/>

### ‘Front Line’ (Mstari wa Mbele)

Front Line ilianzishwa kwa lengo maalum la kuwalinda watetezi wa haki za binadamu, watu wanaofanya kazi, bila vurugu, kwa haki yoyote au zote zilizotajwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu. Front Line ni Taasisi ya Kimataifa kwa ajili ya ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu. Tunafanya kazi ya kufanya utekelezaji wa haraka na

wenye ufanisi katika kusaidia kuwalinda watetezi wa haki za binadamu walio hatarini ili waweweze kuendelea na kazi yao kama wakala muhimu wa mabadiliko ya kijamii.

Chanzo Rasmi: [www.frontlinedefenders.org](http://www.frontlinedefenders.org)

### **Human Rights First (Haki za Binadamu Kwanza)**

'Human Rights First' inaamini kujenga heshima kwa ajili ya haki za binadamu na utawala wa sheria, kutasaidia kuhakikisha utu amba, kila mtu anastahili na itapunguza udhalimu, vitendo visivyokubalika, kutovumilia, na vurugu. 'Human Rights First' ina tovuti kuhusu watetezi wa haki za binadamu ambayo huonyesha kesi, taarifa na maelezo ya nchi.

Chanzo Rasmi: <http://www.humanrightsfirst.org/>

'Human Rights First' pia ina programu ya watetezi wa haki za binadamu ambayo kati ya mambo mengine huzingatia kusaidia watetezi wa haki za binadamu wanaoteswa na watetezi wa haki za binadamu walio hatarini:

Barua pepe: [defenders@humanrightsfirst.org](mailto:defenders@humanrightsfirst.org)

### **Human Rights House Network (Mtandao wa Nyumbani wa Haki za Binadamu)**

Sisi hulinda, kuwawezesha na kuunga mkono mashirika ya haki za binadamu ndani ya nchi na kuungana nao katika mtandao wa kimataifa wa 'Human Rights Houses'.

Chanzo Rasmi: <http://humanrightshouse.org/>

### **Human Rights Watch (Uangalizi wa Haki a Binadamu)**

'Human Rights Watch' ni shirika lisilo la kiserikali, linalojitegemea, linaloungwa mkono na michango kutoka kwa watu binafsi na taasisi mbalimbali duniani kote. 'Human Rights Watch' imejitolea kulinda haki za binadamu za watu duniani kote. 'Human Rights Watch' hutuma habari na taarifa kuhusu hali ya watetezi wa haki za binadamu duniani kote.

Chanzo Rasmi: [www.hrw.org/](http://www.hrw.org/)

### **Interights (Haki mbalimbali)**

'Interights' inakusudia kutekeleza haki za binadamu kwa kutumia sheria, ikitoa ulinzi na ufumbuzi, katika kanda maalum na juu ya masuala yenye lengo la mkakati; na kuwawezesha washirika halali na kuwahamasisha kwa matumizi ya sheria yaliyo na manufaa ili kulinda haki za binadamu. Huwasaidia wanasheria, majaji, mashirika yasiyo ya kiserikali na waathirika walio katika maeneo hayo kwa shughuli zilizolenga kushughulikia mahitaji ya kila kundi na kanda. Hufanya kazi katika mataifa yanayoendelea na yaliyoendelea.

Chanzo Rasmi: <http://www.interights.org>

### **International Commission of Jurists (Tume ya Kimataifa ya Wanasheria)**

Tume ya Kimataifa ya Wanasheria imejitolea kwa uwezo wa kiwango cha juu, mshikamano, na utekelezaji wa sheria na kanuni za kimataifa zinazoendeleza haki za binadamu. Tume ya Kimataifa ya Wanasheria hutoa utaalamu wa kisheria katika ngazi zote za kimataifa na kitaifa ili kuhakikisha kuwa maendeleo katika sheria ya kimataifa inazingatia kanuni za haki za binadamu na kwamba viwango vya kimataifa vinatekelezwa katika ngazi ya kitaifa.

Chanzo Rasmi: <http://www.icj.org>

### **International Federation for Human Rights (Shirikisho la Kimataifa la Haki za Binadamu)**

Shirikisho la kimataifa la Haki za Binadamu hutetea haki zote za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, zilizowekwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu. Linafanya kazi katika uwanja wa kisheria na kisiasa, kuunda na kuimarisha nyenzo za kimataifa kwa ajili ya ulinzi wa Haki za Binadamu na utekelezaji wake.

Chanzo Rasmi: <http://www.fidh.org>

### **International Lesbian and Gay Association (Chama cha Kimataifa cha Wasagaji na Mashoga)**

Chama cha Kimataifa cha Wasagaji na Mashoga ni mtandao wa makundi ya kitaifa na ya mahali husika duniani kote kilichojitolea kufanikisha haki sawa

kwa wasagaji, mashoga, wanaovutiwa kimapenzi na watu wa jinsia zote mbili na wenyе jinsi mbili, kila mahali. Chama cha Kimataifa cha Wasagaji na Mashoga, kilichoanzishwa mwaka 1978, mpaka sasa ni shirikisho pekee la kimataifa lisilo la kiserikali na lisilokuwa kwa ajili ya kujitengeneza faida, la kijamii lililolenga katika kuwasilisha ubaguzi kwa misingi ya tabia ya mwenendo wa kufanya mapenzi kama suala la kimataifa.

Chanzo Rasmi: <http://ilga.org>

### **International Service for Human Rights (Huduma ya Kimataifa ya Haki za Binadamu)**

Huduma ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ni chama cha kimataifa kinachowahudumia watetezi wa haki za binadamu. Huhamasisha maendeleo, uimarishaji, matumizi ya ufanisi na utekelezaji wa sheria za kimataifa na kikanda na taratibu za ulinzi na uendelezaji wa haki za binadamu.

Chanzo Rasmi: <http://www.ishr.ch>

### **New Tactics for Human Rights Project (Mbinu mpya za Mradi wa Haki za Binadamu)**

Tangu mwaka 1999, 'New Tactics for Human Rights Project' imefanya kazi kwa kutoa nyenko kwa watetezi wa haki za binadamu wanaotoa ufumbuzi wa mbinu bunifu kwa ajili ya kupambana na changamoto maalum. Nyenko hizi huwawezesha wanaharakati kupanga changamoto maalum za kipekee kwa maeneo yao wanayoshughulikia,, kutambua njia ambazo zimefaa katika mazingira mengine ili kuzirekebisha na kutekeleza mbinu hizo katika maeneo husika.

Chanzo Rasmi: <http://www.newtactics.org/>

### **Norwegian Ministry of Foreign Affairs (Wizara ya Mambo ya Nje ya Norway)**

Kulinda haki za binadamu ni kipaumbele kikuu katika sera za Norway za haki za binadamu. Lengo la jumla ni kwamba juhudhi za kuendeleza na kutetea haki za binadamu katika maeneo yote ya dunia ziweze kufanyika bila vikwazo au vitisho kwa watetezi wa haki za binadamu au familia zao. Katika mashirika ya Umoja wa Mataifa na mengine ya kimataifa, Norway huendeleza kikamilifu juhudhi za kuunga mkono

watetezi wa haki za binadamu.

Katika ngazi ya kitaifa, balozi nyangi za kidiplomasia za Norwei zina jukumu la kuchukua hatua mbalimbali na kuendesha kampeni za pamoja na watendaji wengine wa kimataifa ili kusaidia kazi yao. Watetezi wa haki za binadamu ni washirika muhimu wa ushirikiano kwa balozi za kidiplomasia.

Chanzo Rasmi: <http://www.regjeringen.no/en/dep/ud.html?id=833>

### **Observatory for the Protection of Human Rights Defenders (Uangalizi kwa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu)**

Taasisi ya Kimataifa ya Haki za Binadamu iliunda 'Uangalizi wa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu', ikiungana na Shirika la Dunia Dhidi ya Mateso. Uangalizi huo una mtazamo wa mbinu mbili: kuingilia kati ili kuzuia au kupata ufumbuzi katika hali za ukandamizaji na mchango wa uhamasishaji wa kimataifa kutambua shughuli za watetezi wa haki za binadamu na haja ya ulinzi wao katika ngazi ya kikanda na kimataifa.

Chanzo Rasmi: [http://www.fidh.org/rubrique.php3?id\\_rubrique=180](http://www.fidh.org/rubrique.php3?id_rubrique=180)

Barua pepe: Appeals@fidh-omct.org

### **Protection International (Ulinzi wa Kimataifa)**

Watetezi wa Haki za Binadamu ni mmoja wa watendaji wakuu wa mapambano dhidi ya kutoadhibu kwa ajili ya haki. Wao ni watu muhimu wenyе malengo katika kujenga na kuimarisha amani na demokrasia bali hujikuta wakiishia katika mashambulizi na vitisho vy'a mara kwa mara. Ulinzi wa Kimataifa unachangia kuimarisha usalama na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu na kuhamasisha jamii ya kitaifa na kimataifa (bunge, serikali, Umoja wa Mataifa, raia wa kawaida, vyombo vy'a habari). Vile vile huwapatia maarifa na nyenko muhimu pande husika na walengwa ili waweze kushirikisha ulinzi wa mahali husika na watu wake katika mipango na programu za kazi. Programu hii pia huwesheza ubadilishanaji wa uzoefu ndani ya nchi na kuendeleza matendo bora kati ya watetezi wa haki za binadamu

Chanzo Rasmi: <http://www.protectioninternational.org/>

## **Reporters Without Borders (Waandishi Wasiokuwa na Mipaka)**

Waandishi Wasiokuwa na Mipaka huwatetea waandishi wa habari na wasaidizi wa vyombo vya habari waliofungwa au kuteswa kwa kufanya kazi yao na huonyesha wazi wanavyotendewa vibaya na mateso yao katika nchi nyingi. Hupambana dhidi ya udhibiti na sheria ambazo hudhoofisha uhuru wa habari, hutoa misaada ya fedha kila mwaka kwa waandishi wa habari 300 au vyombo vya habari vilivyo na hali ngumu (kuwalipa wanasheria, huduma ya matibabu na vifaa) na pia kwa familia za waandishi wa habari waliofungwa, na hufanya kazi kuboresha usalama wa waandishi wa habari, hasa wale wanaotoa taarifa katika maeneo ya vita.

Chanzo Rasmi: <http://en.rsf.org>

## **Urgent Action Fund (Mfuko wa Utekelezaji wa Haraka)**

‘Urgent Action Fund’ ni mfuko pekee wa kimataifa wa wanawake duniani ulioundwa kushughulikia taarifa za muda mfupi. Moja ya maeneo yao muhimu ya kushughulikia ni ulinzi wa watetezi wa wanawake wa haki za binadamu.

Chanzo Rasmi: <http://www.urgentactionfund.org/>

Tawi la Afrika (Nairobi): <http://www.urgentactionfund-africa.or.ke/>  
Simu: (254) 020 2,301,740  
Faksi: (254) 020 2,301,740  
Simu ya Ofisi: +254 726577560  
Barua pepe: [info@urgentactionfund-africa.or.ke](mailto:info@urgentactionfund-africa.or.ke)

## **Witness (Shuhudia)**

‘Witness’ ni shirika la kimataifa lisilojizalishia faida ambalo hutumia nguvu ya video na usimulajji wa hadithi kuufungua macho ulimwengu juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Shirika hili liliundwa kwa ushirikiano ulioanzishwa mwaka 1992 na mwanamuziki na mtetezi wa haki za binadamu, Peter Gabriel, asasi za ‘Human Rights First’ na ‘Reebok Human Rights Foundation’.

Chanzo Rasmi: <http://www.witness.org/>

## **World Organization Against Torture (Shirika la Dunia Dhidi ya Mateso)**

Sekretarieti ya Kimataifa ya Shirika la Dunia Dhidi ya Mateso ikiwa na makao yake jijini Geneva, hutoa msaada wa tiba binafsi, kisheria na/au kijamii kwa mamia ya wahanga wa mateso na kuhakikisha usambazaji wa kila siku wa rufaa za haraka duniani kote, ili kuwalinda watu binafsi na kupambana na kutoadhibiwa. Programu maalum huiwezesha kutoa msaada kwa makundi maalum ya watu walio na uwezekano wa kudhurika, kama vile watetezi wa haki za binadamu. Katika mfumo wa shughuli zake, Shirika la Dunia Dhidi ya Mateso, pia huwasilisha mawasiliano binafsi na taarifa zisizokuwa za kawaida kwa taratibu maalum za Umoja wa Mataifa, na kushirikiana kikamilifu katika maendeleo ya desturi za kimataifa kwa ajili ya ulinzi wa haki za binadamu.

Chanzo Rasmi: <http://www.omct.org>

Mradi wa Watetezi wa Haki za Binadamu Afrika ya Mashariki na Pembe ya Afrika (EHAHRDP) unajaribu kuimarisha kazi ya watetezi wa haki za binadamu katika kanda ndogo nzima kwa kupunguza uwezekano wao wa kuathiriwa na hatari ya mateso na kwa kukuza uwezo wao ili waweze kutetea haki za binadamu kwa ufanisi.

EHAHRDP ni sekretarieti ya Mtandao wa Mradi wa watetezi wa Haki za Binadamu Afrika ya Mashariki na Pembe ya Afrika (EHAHRD-Net), mtandao wa mashirika zaidi ya 75 ya haki za binadamu katika nchi kumi na moja za kanda ndogo: Burundi, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Somalia (pamoja na Somaliland), Sudan Kusini, Sudan, Tanzania na Uganda.



East and Horn of Africa Human Rights Defenders Project  
Human Rights House, Plot 1853, Lulume Rd., Nsambya  
P.O Box 70356 Kampala Uganda  
Phone: +256-312-256-820  
Fax: +256-312-256-822  
Email: program@defenddefenders.org, hshire@yorku.ca  
Web : <http://www.defenddefenders.org>

Produced with the support of:



[facebook.com/humanrightsdefendersproject](https://facebook.com/humanrightsdefendersproject)



@EHAHRDP